

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

#### MKUTANO WA PILI

**Kikao cha Pili – Tarehe 3 Februari, 2021**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

#### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulla Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Tukae. Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

#### MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, sasa aulize swalii lake.

Na. 16

**Ujenzi wa Barabara za Lami - Mji wa Mafinga**

**MHE. COSATO D. CHUMI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza Ujenzi wa Barabara za lami na kufunga taa za barabarani katika Mji wa Mafinga chini ya Mpango wa Uendelezaji Miji nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA  
MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia mimi na Waheshimiwa Wabunge wote afya njema na kutuwezesha kuwa wawakilishi wa wananchi kuitia Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa imani kubwa aliyonipa kwa kunitfea kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Wanging'ombe kwa kunichagua na kuchagua mafiga matatu ya Chama cha Mapinduzi na niwahakishie utumishi uliotukuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naomba sasa kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, nijibu swali la Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Miji ya Kimkakati (*Tanzania Strategic Cities Projects -TSCP*) umetekelezwa katika Halmashauri za Majiji ya Tanga, Dodoma, Mbeya, Arusha na Mwanza na Halmashauri za Manispaa za Mtwara-Mikindani, Illemela na Kigoma-Ujiji kwa gharama ya Dola za Kimarekani milioni 355.5 sawa na shilingi bilioni 799.52.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Kuendeleza Miundombinu katika Miji 18 (*Urban Local Government Strengthening Programme - ULGSP*) umetekelezwa katika Halmashauri za Manispaa za Morogoro, Tabora, Moshi, Sumbawanga, Shinyanga, Songea, Iringa, Mpanda, Lindi, Singida, Musoma na Bukoba na Halmashauri za Miji Kibaha, Babati, Geita, Korogwe, Bariadi na Njombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Miji ya Kimkakati (*TSCP*) pamoja na Mradi wa Kuendeleza Miundombinu katika Miji 18 (*ULGSP*) ilimalizika muda wake Mwezi Desemba, 2020. Serikali inaendelea na mazungumzo na Benki ya Dunia kwa ajili ya kuanza kutekeleza Programu nyingine ya kuendeleza miundombinu itakayohusisha Halmashauri 26 zilizokuwepo kwenye Programu zilizomalizika pamoja na Halmashauri nyingine 19 za Miji ikiwemo Mafinga.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cosato David Chumi, swalil la nyongeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa niaba ya wananchi wa Mafinga, nafarijika kwamba katika zile Halmashauri 19 za Miji, Mafinga nayo itakuwemo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na jibu la msingi, naomba Serikali iweze kuwaambia wananchi wa Mafinga, mazungumzo haya na Benki ya Dunia kwa ajili ya kuanza kutekeleza *program* nyingine ya kuendeleza miundombinu katika hiyo Miji 26 na 18 yatakamilika lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalil la pili, kwa kuwa hali ya barabara zetu wakati huu ambapo mvua sasa zimeanza kunyesha kwa wingi, maeneo mengi nchi nzima barabara zimekatika baina ya eneo moja na nyingine: Je, Serikali kupitia *TARURA* iko tayari kutenga fedha za *emergence* na fedha hizi zikaka kule kule Wilayani kuliko ilivyo sasa ambapo Wilaya au Mji kama Mafinga inabidi tuombe *Emergency Fund* kutoka *TARURA* Makao Makuu; sasa *when it is emergence*, imaanishe kweli ni *emergence*: Je, Serikali iko tayari kutenga *Emergency Fund* kwa ajili ya barabara ambazo zimeleta matatizo wakati kama huu wa mvua nyingi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu

Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafingi Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mazungumzo kati ya Serikali na Benki ya Dunia kuhusu miradi hii ya kuendeleza Miji inaendelea. Niseme kwamba maongezi haya yanaendelea na tunaamini kwamba mipango iliyoko na mwelekeo wa haya mazungumzo haitachukua muda mrefu kukamilisha mazungumzo haya. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira kwamba Serikali inakwenda kutekeleza suala hili kwa ufanisi iwezekanavyo mara baada ya mazungumzo haya kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusiana na miundombinu ya barabara na je, kama Serikali iko tayari kupeleka fedha za dharura kupitia *TARURA* katika Wilaya kwa ajili ya kuhudumia barabara zilizoharibika. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kupitia *TARURA* imejipanga ku-*respondkwa* wakati kutatua changamoto za miundombinu ambayo itatokana na uharibifu wa mvua ambazo zinaendelea kunyeshaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mara tu changamoto hizi zitakapoonekana katika maeneo husika, naomba nimhakikishie kwamba Serikali iko tayari na tutahakikisha tunatatua changamoto hizo kwa wakati. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Name naomba nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa miradi hii ya kimkakati ambayo tunaizungumzia imekuwa na msaada mkubwa sana kwenye Halmashauri zetu na hasa kuisaidia *TARURA* kwenye kuhakikisha miradi inafanikiwa zaidi, tunao mradi mwingine mkubwa wa *Tacticambao* Serikali imeshauanzisha ikiwemo Jiji la Mbeya pamoja na Jiji la Mwanza na Manispaa nytingine.

Je, ni nini sasa mpango wa Serikali kuhakikisha mradi huu unaanza haraka ili tuone matokeo yake makubwa kama TSCP?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya maswali ya awali. Pia naomba nimpongeze ndugu yangu, mtani wangu Mheshimiwa Stanslaus Mabula Bin Jongo wa kutoka Pwani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika Jiji ambalo tumefanya kazi kubwa sana ni Jiji la Mwanza. Kwa hili, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa waliyofanya kwa kushirikiana na TAMISEMI kubadilisha Jiji la Mwanza kuonekana katika sura iliyokuwepo. Hata hivyo, mpango wetu kama nilivyosema wakati natoa budget speech yangu katika mwaka uliopita kwa mwaka wa Fedha 2021, kwamba tumekuwa na ile miradi ya *Tactic*, ambapo matarajio yetu makubwa ni kwamba tutakwenda kugusa maeneo 45 zikiwepo Halmashauri za Miji, Mafinga ikiwa ni mojawapo, Nzega, Kasulu, Handeni Mjini na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge wawe na subira tu, kazi inakwenda vizuri. Ni imani yetu kwamba mradi huu unakwenda kubadilisha kabisa nchi yetu. Katika miaka mitano ijayo, Tanzania miji yake yote itakuwa ni ya ajabu kutokana na kazi kubwa tunayokwenda kuifanya. Kwa hiyo, msihofu, kazi inafanyika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza kuna Wabunge wanaleta vikaratasi kwa ajili ya kuomba kuchangia hotuba, naomba wapeleke kwa Viongozi wao wa Chama ili

iwe rahisi kuratibu. Ndiyo utaratibu wa kikanuni unavyosema. Orodha italetwa hapa mbele na Viongozi wa Vyama husika waliopo humu ndani.

Tuendelee na maswali. Pia naomba tuulize kwa kifupi ili wengi mpate fursa ya kuuliza maswali. Tunaendelea na swalii la Mheshimiwa Dkt. Pindi Hasara Chana, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 17

### **Kuboresha Mifuko ya Halmashauri za Wilaya**

**MHE.DKT. PINDI H. CHANA** aliuliza:-

Serikali imekuwa ikisaidia sana vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu nchini kupitia Halmashauri za Wilaya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha Mifuko hiyo ili kutoa viwango vikubwa zaidi vya mikopo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibuu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu inayotokana na asilimia 10 ya mapato kutokana na vyanzo vya ndani vya halmashauri inatolewa na halmashauri zote nchini kutokana na fedha zilizokusanywa na halmashauri kwa kipindi husika baada ya kutoa vyanzo lindwa kama vile fedha za uchangiaji wa Huduma za Afya, ada za taka na ada za Shule za Sekondari Kidato cha Tano na Sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha kiwango cha mikopo inayotolewa na halmashauri Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kuzisimamia halmashauri kutekeleza Sheria ya Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, kuzijengea uwezo Kamati za Huduma za Mikopo za Kata na Halmashauri ili ziwe na ujuzi wa kutosha wa kuanzisha na kuendeleza vikundi nya wajasiriamali pamoja na ujuzi wa kusimamia utoaji na urejeshwaji wa mikopo, kutoa elimu ya ujasiriamali kwa wanufaika wa mikopo kabla ya utoaji wa mikopo kupitia Maafisa Maendeleo ya Jamii pamoja na kuzielekeza halmashauri kuendelea kubuni vyanzo vipyta nya mapato.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, swalii la nyongeza.

**MHE. DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, kaka yangu Dkt. Dugange kutoka Wanging'ombe, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu la msingi tumesema kwamba inatokana na mapato ya kipindi husika asilimia 10, napigia mstari neno kipindi husika. Naomba kupendekeza maboresho kwamba halmashauri zinapokusanya pesa, *let say*, ya 2020; baada ya yale marejesho, inapokwenda 2021, ichukuliwe ile ya 2020 ichanganywe na 2021, ule Mfuko uwe *Cumulative Revolving Fund* na fedha ziwe nyingi. Halafu tunapokwenda 2022 tunachanganya ile miaka miwili, yaani Mfuko unakuwa mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la kwanza, je, hatuoni sasa wakati umefika wa kukusanya ule Mfuko wa kukopesha ukawa ni *Revolving Fund?*

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, hatuoni kama wakati umefika, maafisa wanaosimamia mikopo hii wakapata elimu kama Maafisa Mikopo katika benki zetu

ambao mara nyingi ni Maafisa Maendeleo ya Jamii kama *Loan Officer*?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Chana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na mikopo ya asilimia 10 kutolewa kwa kipindi husika, kama ambavyo jibu la msingi limesema, ni kweli kipindi husika cha makusanyo ndicho ambacho tumesitiza kama Serikali kuhakikisha halmashauri zinatenga asilimia 10 kwa ajili ya mikopo kwa makundi hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo hiyo ni ile ambayo inahusisha wajasiriamali ambao fedha zile ambazo zinakopeshwa zinatakiwa kurejeshwa ili kutoa fursa kwa vikundi vingine kuweza kukopa fedha hizo. Kwa hiyo, napokea ushauri mzuri wa Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana kwamba tutaendelea kusimamia, kuhakikisha kwamba mapato yanayokusanywa kwa kipindi husika, asilimia 10 inatengwa na kupelekwa kwenye vikundi hivyo ili kuwawezesha kuendesha shughuli zao za ujasiriamali kwa ufanisi mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Mfuko huu kuwa *Revolving Fund*, kimsingi Mfuko huu ni *Revolving Fund* mpaka sasa, kwa sababu baada ya kukopeshwa, vikundi vinarejesha kiasi cha fedha kilichokopwa bila riba kwa ajili ya kuwawezesha wakopaji wengine waweze kunufaika na mfuko huo. Kwa hiyo, tutaendelea kuelimisha jamii yetu na vikundi vyta wajasiriamali kuweza kurejesha mikopo hiyo ili na wengine wapate fursa hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na mchango na ushauri wa kuwa na maofisa ambao wanapata mafunzo mbalimbali ya mifumo hii katika benki na maeneo mengine, tunauchukua ushauri huo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tunza Malapo, swalii la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mikopo hii inahusu watu wenyewe ulemavu; na swalii langu ni kwamba, inapotoka mtu mwenye ulemavu ambaye hawezi kufanya shughuli yoyote, lakini ana mlezi ambaye anamlea. Je, Serikali sasa haioni kuna sababu ya kumkopisha yule mtu ambaye anamlea mtu mwenye ulemavu ili aweze kufanya shughuli itakayomwezesha yule mtu kuweza kumlea vizuri yule mtu mwenye ulemavu? (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mikubwa mpaka tulipofikia hapa. Tukumbuke kihistoria kwamba Mfuko huu ulikuwa haufanyi vizuri, lakini kwa taarifa tulyoitaa mwaka 2020, zaidi ya shilingi bilioni 124 ziliweza kuelekezwa katika makundi haya. Mpaka leo taarifa yetu ya miezi sita mpaka mwezi Desemba, zaidi ya shilingi bilioni 22.45 zimeelekezwa katika makundi haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, nazishukuru Kamati za Bunge hasa Kamati ya TAMISEMI na Kamati ya LAAC katika kutoa ushauri wa uboreshaji wa Kanuni na hasa makundi ya watu wenyewe ulemavu. Hivi sasa tume-review kanuni zetu za kuhakikisha, hata kama mlemau ni mmoja, aweze kupata mkopo ambapo hayo yalikuwa ni maelekezo ya Bunge. Hata hivyo, tumeenda katika suala zima la uboreshaji katika eneo hilo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, nia yetu ni kwamba Mfuko huu uende kufanya vizuri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dada Malapo, hilo ni jambo ambalo Serikali hivi sasa inalifanyia kazi, lengo likiwa, walemavu waweze kushiriki vizuri katika shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Vunjo, sasa aulize swalii lake.

Na.18

#### **Mwongozo kwa *Tour Operators***

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kunakuwepo na Mwongozo kwa *Tour Operators* wanaopandisha watalii Mlima Kilimanjaro wanaojiri Wapagazi, Wapishi na Waongoza Misafara kwa kuwalipa ujira stahiki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nami kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge lako Tukufu, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii kusimama mbele ya Bunge hili. Vile vile namshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli pamoja na chama changu kwa kuniamini na leo hii nasimama mbele ya Bunge lako Tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba sasa nijibu swalii la Mheshimiwa

Dkt. Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Jimbo la Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka 2015 ilitoa Mwongozo kwa Mawakala wa Utalii wa Mlima Kilimanjaro *Tour Operators* wa kuwalipa ujira stahiki Wapagazi, Wapishi na Waongoza Watalii waliowaajiri kwa ajili ya kuwahudumia watalii wanaopanda Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwongozo huo, Serikali iliagiza kuwa mwongoza watalii alipwe dola za Kimarekani 20 kwa siku, sawa na Sh.40,000 kwa siku, mpishi alipwe dola za Kimarekani 15 sawa na shilingi 30,000 na mpagazi alipwe dola za Kimarekani 10 sawa na Sh.20,000 kwa siku. Wastani wa siku za kupanda mlima hadi kileleni na kushuka ni kuanzia siku 5 hadi 7.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 12 Disemba, 2015, wadau wa utalii wa Mlima Kilimanjaro ambaao ni mawakala wa utalii, viongozi wa wawakilishi wa vyama vya waongoza watalii, wapagazi na wapishi walikutana na kusaini mwongozo huo wa malipo ambapo pande zote ziliridhia viwango hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Mwongozo huu na makubaliano hayo. Katika utekelezaji wa mwongozo, kulijitokeza changamoto ya baadhi ya mawakala wa utalii kutokulipa viwango hivyo na kwa hivyo Serikali iliweka mikakati kadhaa ya kuhakikisha kuwa viwango hivyo vinalipwa kama ilivyoagizwa. Baadhi ya mikakati hiyo ni pamoja na:-

(i) Kushirikiana na Wizara ya Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu kuandaa mikataba ya kisheria ambapo mawakala wa utalii husaini pamoja na waongoza watalii, wapagazi na wapishi wanaoaajiriwa kabla ya kuanza kazi. Mkataba huo umeainisha kiwango cha malipo na idadi ya siku atakazofanya kazi na jumla ya malipo anakayostahili kulipwa. Nakala moja ya mkataba huu hukabidhiwa kwenye

lango la kupandia mlima, nakala nyingine hupewa waajiriwa (waongoza watalii, wapishi na wapagazi) na nakala moja hubaki kwa wakala wa Utalii.

(ii) Idara ya Kazi imekuwa ikihimiza waajiriwa kutokuanza kazi bila ya kuwa na mikataba. Pia, Idara imekuwa ikifanya ukaguzi wa karibu na wa mara kwa mara katika malango ya hifadhi, ofisi za mawakala wa utalii ili kujiridhisha kuwa utaratibu huo unazingatiwa wakati wote; na

(iii) Changamoto zinazotokana na waajiriwa kutokulipwa kiwango stahiki, kuchelewa kulipwa au kutokulipwa kabisa zimekuwa zikishughulikiwa kwa karibu na Idara ya Kazi na vyama vya waongoza watalii na wapagazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutoa wito kwa waongoza watalii, wapishi na wapagazi kuendelea kujituma katika utekelezaji wa majukumu yao kwa manufaa ya Taifa. Pia, Serikali inaendelea kutoa wito kwa mawakala wote wa utalii kuhakikisha kuwa wanatoa ujira stahiki kwa wahusika ili waendelee kupata motisha ya utendaji kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba niulize maswali mawili mafupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nashukuru sana kwamba nimepewa jibu la kina na naamini tutaendelea kulifuatilia suala hili. Zaidi ni kwamba hawa *operators* wanakuja na watu kutoka sehemu nyingine ambao hawajui hii mikataba. Kwa hiyo, hawaajiri wale vijana ambao wanatoka kwenye vijiji karibu na ule mlima, wao hawaelewi mikataba hiyo hivyo wanalipwa kidogo sana. Je, hatuwezi kuweka uwiano fulani hasa kwa zile shughuli ambazo hazihitaji taaluma kwamba hawa *operators* waweze kuajiri au kuchukua vijana kutoka kwenye kundi la wale ambao wanatoka karibu na mlima kwa sababu hiyo ni njia mojawapo ya kuwapa motosha? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili ni nyeti kidogo ni hili suala la nusu *mile*. Kwa vile tunajua kwamba watu wanaolinda ule mlima ni wale wanavijiji walio karibu na hifadhi ya mlima ule inakuwaje sasa suala la nusu *mile*. Nusu *mile* ni suala nimezungumza na Mheshimiwa Waziri na ni nyeti kidogo lakini nafikiri kwamba tusiliangalie kama watu wanaomba kuingia msituni isipokuwa ni ku-reviewile mipaka ya msitu na kuongeza sehemu ndogo ambayo inaweza ikasaidia wale wananchi wanaoishi karibu kuweza kupata kuni na kupata malisho ya wanyama bila kuathiri miti. Siyo suala la kuingia isipokuwa ni suala la kupanua...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa, swalii limeshaeleweka. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, Mbunge wa Jimbo la Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kumekuwa na changamoto ya wageni kupata ajira kwenye maeneo ya hifadhi hasa kwenye Mlima Kilimanjaro. Hata hivyo, katika mwongozo wa waongoza utalii kuna kiwango ambacho wamewekewa waongoza utalii ambapo hawa watumishi kwa maana ya wanaoomba ajira wanaomba kwa kuzingatia mwongozo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na changamoto pia kwenye upande wa kiwango kwamba mtu anapokuwa anahitaji ajira basi anapunguza kiwango kinakuwa chini ya mwongozo uliopo. Waongoza utalii (*tour operators*) wao wanazingatia zaidi kupata faida kwenye biashara zao. Kwa hiyo, huyu mtumishi anapokuwa akiomba ajira na kwa kuzingatia kwamba waombaji wa ajira wanakuwa ni wengi basi anapunguza kiwango ili aweze kupata ajira. Kwa hiyo, kumekuwa na changamoto hii lakini tunawashauri watumishi wanaokutana na changamoto hizi waende kwenye Tume

ya Usuluuhishi (Mahakama ya Kazi) ambayo inasimamia haki za mtumishi yeote anapokuwa amedhulumiwa haki yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lingine ni kuhusu nusu *mile*, naomba itambulike kwamba maeneo ya hifadhi yanapokuwa yametangazwa kuwa hifadhi hairuhusiwi kufanya kitu chochote zaidi ya uhifadhi. Nimuombe sana Mheshimiwa Dkt. Kimei, sisi kama Serikali tunapokuwa tunahifadhi maeneo haya tunatunza ili yawe kivutio na kwa ajili ya kutuletea mapato.

Kwa hiyo, tunapokuwa tunatunza, hairuhusiwi kufanya kitu chochote ndani ya eneo la hifadhi, hata kama ni kuokota kuni hairuhusiwi. Kuna maeneo mengine ambayo huwa tunawatengea wananchi kwa ajili ya kuendelea na shughuli zingine kama ufugaji, uvuvi pamoja na kilimo lakini maeneo yanayotunzwa kama hifadhi hairuhusiwi kufanya kitu chochote.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, swali hili peke yake limechukua dakika 12. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifupi sana kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, kwa kweli nampongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ambayo imeletwa na Mheshimiwa Dkt. Kimei inahusika pia na masuala ya mikataba ya ajira na stahiki za wafanyakazi na mfumo mzima wa uratibu wa ajira katika eneo la Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Waziri ameliweka vizuri, tayari Wizara ya Maliasili na Wizara yetu tumeweke ule mwongozo. Tunawaomba sana wafanyakazi wote wanapokutana na changamoto zozote ambazo pia zinahusiana na Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, 2004, wajitahidi kuwa wanatoa taarifa mapema sana kwenye ofisi zetu za Idara ya Kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sasa imeamua kufungua kliniki maalum. Kila Ijumaa ya mwisho wa mwezi wafanyakazi wote ambaao wanaona wana changamoto zinazohusiana na sheria za kazi watakuwa wanaripoti kwenye ofisi zetu za kazi ili wakaeleze zile changamoto wanazozipata kama ni za mishahara, mikataba na mambo mengine yoyote ili ofisi ya Waziri ya Waziri Mkuu iweze kuchukua hatua haraka ili kuondoa migogoro katika maeneo ya kazi kati ya mfanyakazi na mwajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunamuomba sana Mheshimiwa Kimei kama ana mambo ya ziada aonane pia na ofisi yetu na tutaweza kulifanyia kazi na tutaagiza utaratibu na mwongozo usimamiwe vizuri. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii na Naibu Waziri, kuna changamoto kubwa sana huko kwa sababu mimi mwenyewe nimeshapanda ule mlima. Hivi viwango viiviyowekwa na ile kazi iliyopo ya kupanda mlima na mizigo mgongoni siyo kazi nyepesi. Kwa hiyo, pia wale watu hawapandi kule kila siku, ili upangiwe zamu lazima uwe ni mwajiriwa ambaye una mahusiano mazuri na yule mwajiri wako. (*Makofii*)

Sasa mazingira kama hayo sio rahisi sana kwao kuja kusema mimi nimelipwa hivi kwa sababu hatapangisha tena kupanda mlima na hivyo kukosa fedha. Nadhani ni jambo ambalo mnatakiwa kulitazama kwa mapana sana kwa sababu mazingira yake ni tofauti na hizi kazi nyingine za kawaida.

Nawashawishi na kuwapa moyo Waheshimiwa Wabunge wakapande Mlima wa Kilimanjaro. (*Makofii*)

Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo sasa aulize swalii lake.

Na. 19

### **Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla**

**MHE. MARGARET S. SITTA** aliuliza:-

Serikali imeanzisha Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugalla Wilayani Urambo:-

(a) Je, ni lini Serikali itatoa elimu elekezi kwa wananchi wa maeneo hayo juu ya matumizi ya eneo husika baada ya mabadiliko yaliyotokea?

(b) Kutokana na ongezeko la watu, je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia wananchi maeneo kwa ajili ya ufugaji nyuki, mifugo na kilimo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Sitta, Mbunge wa Urambo lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla ina ukubwa wa kilomita za mraba 3,865. Hifadhi hii ilianzishwa kwa Azimio la Bunge la tarehe 10 Septemba, 2019 na Tangazo la Serikali Na. 936 la tarehe 29 Novemba, 2019. Hifadhi ipo katika Wilaya ya Urambo na Kaliua Mkoani Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya kuanzishwa kwa hifadhi hii ni kuimarisha uhifadhi ili kuunganisha mfumo wa ikolojia wa Malagarasi - Muyowosi amba ni ardhi oevu yenye umuhimu wa kitaifa na kimataifa pamoja na kuongeza pato la Taifa kutokana na ongezeko la idadi ya watalii, kuwezesha jamii kunufaika na fursa za utalii na kutunza vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na Mpango kutoa Elimu ya Uhifadhi ambao unalenga kujenga uwezo na uelewa kwa wananchi, viongozi na wadau wengine wa uhifadhi ambao wanapakana na Hifadhi za Taifa. Utekelezaji wa mpango huo, ulianzia kwenye Wilaya ya Kaliua, ambapo ulihuisha Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya na vijiji 12. Hatua inayofuatia ni kuendelea na programu hiyo kwenye Wilaya ya Urambo, ambapo zoezi litaanza kwenye Kata ya Nsendo ambako vijiji nane (8) vitahusishwa. Nia kubwa ya uhamasishaji huo ni kujenga uelewa kuhusu sheria, kanuni na taratibu za uendeshaji wa Hifadhi za Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka 2021/2022, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuendelea kutekeleza mpango wa kutoa elimu ya uhifadhi na kuweka mkazo kwenye kuandaa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya husika, pamoja na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi; kuendelea kuhakiki mipaka ya maeneo ya hifadhi kwa kuweka alama za kudumu na mabango elekezi ili mipaka ionekane kwa urahisi; na kuendelea kutoa huduma za ugani kwa ushirikiano na wadau wa uhifadhi katika maeneo mbalimbali ili kutunza mazingira, vyanzo vya maji na misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 6 (1) cha Sheria ya Hifadhi za Taifa Tanzania, Sura 282 iliyofanyiwa Mapitio mwaka, 2002 kinabainisha kuwa Mheshimiwa Rais akishatangaza eneo la ardhi yoyote kuwa Hifadhi ya Taifa, haki zote za awali zikiwemo hati miliki zilizokuwa juu ya eneo husika zinakoma. Wizara yangu itawasiliana na Mamlaka za Mikoa na Halmashauri ili kupata maeneo nje ya Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla kwa ajili ya shughuli za ufugaji nyuki, mifugo na kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe wito kwa wananchi wote wanaozunguka Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla kuunga mkono juhudzi zinazofanywa na Serikali katika kuzuia na kupambana na ujangili na hatimaye kuboresha utalii kwa

ajili ya maendeleo endelevu katika jamii husika na nchi kwa ujumla.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Margaret Sitta, swali la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kujibu maswali vizuri kwa mara ya kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini napenda Serikali itambue kwamba wananchi wa Urambo wanashukuru kupata hifadhi lakini kwa kuwa kulikuwa na mgogoro wa muda mrefu tangu 2013/2014 kuhusu mipaka, je, Serikali haikuona kwamba kuna haja ya kumaliza ile migogoro kabla ya kuwa na hifadhi ili wananchi waendelee na maisha yao ya kufuga nyuki ambao sasa hivi hawaruhusiwi kufuga mifugo na kulima?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, lini Mheshimiwa Waziri atakuja ajionee mwenyewe kwa sababu mpaka sasa hivi wameshakuja Naibu Mawaziri wawili, alishakuja Mheshimiwa Ramo wakati ule, Mheshimiwa Naibu Waziri Angelina Mabula alikuja na pia alikuja Mheshimiwa Kiwangalla aliyekuwa Waziri lakini bahati mbaya mvua ilinyesha hakuweza kufika maeneo yale. Je, ni lini Serikali inakuja ione jinsi ambavyo wananchi wanataka maeneo waendelee kuendesha maisha yao kwa kilimo, kufuga nyuki na mifugo pia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuhusiana na suala la mgogoro, Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi siku zote imekuwa ikishirikiana na wananchi wake katika

kutatua changamoto mbalimbali. Migogoro ya ardhi imeshapatiwa suluhisho kuptitia Tume ya Mheshimiwa Rais ya Mawaziri Nane Ilyoongozwa na Mheshimiwa Lukuvi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Margaret Sitta kwamba suala hilo nalo limeshapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili kuhusiana na lini tutakwenda? Nimhakikishie Mheshimiwa Margaret Sitta mara baada ya Bunge hili nitaambatana naye kwenda jimboni Urambo kuhakikisha tunatatua suala hili. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tuelekee Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Ali Hassan King, Mbunge wa Jang'ombe, sasa aulize swali lake.

Na. 20

**Hatma ya Fedha za Wananchi Katika Benki Zilizozuiwa  
Kuendesha Shughuli zao Nchini**

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING** aliuliza:-

Je, Serikali imefikia hatua gani katika kufuatilia fedha za wananchi zilizopo katika Benki ambazo zimezuliliwa kuendesha shughuli zao hapa nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu tangu niteuliwe kuwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kuchukua nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kuijaalia nchi yetu amani na utulivu na kutujaalia sisi sote uzima na afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais wangu, Dkt John Pombe Joseph Magufuli kwa kuniamini na kunitua katika nafasi hii. Aidha, nitoe shukrani kwa familia yangu kwa kuendelea kunitia moyo hivyo kunipa nguvu na kuendelea kutekeleza majukumu yangu kiufanisi. Vilevile niwashukuru viongozi wangu wa CCM pamoja na UWT kuanzia ngazi ya Mkoa hadi Taifa kwa kuniamini na kunipa nafasi hii kuwa mwakilishi wao hapa Bungeni. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Ali Hassan King, Mbunge wa Jang'ombe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2017 na 2018, Benki Kuu ya Tanzania ilizifutia leseni ya kufanya blashara ya kibenki benki saba kwa mujibu wa vifungu vya 11(3)(i), 41(a), 58(2)(a), na 61(1) vya Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006. Benki zilizofutiwa leseni ya kufanya biashara nchini ni pamoja na: *FBME Bank Limited; Mbinga Community Bank Plc, Njombe Community Bank Limited, Kagera Farmers' Cooperative Bank Limited, Meru Community Bank Limited; Efatha Bank Limited; na Covenant Bank for Women (T) Limited.*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzifutia leseni benki hizo Benki Kuu ya Tanzania iliteuwa Bodi ya Dhima ya Amana (*Deposit Insurance Board*) kuwa Mfilisi. Katika kutimiza wajibu wake wa msingi Bodi ya Bima ya Amana ilianza zoezi la kulipa fidia ya bima ya amana ya Sh.1,500,000 kwa waliostahili kulipwa bima ya amana na zoezi hili bado linaendelea kwa wateja ambao hawajajitokeza kuchukua fidia. Sanjari ya zoezi hili *DIB* inaendelea na zoezi la ufilisi wa benki hizo tajwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Desemba 2020, Sh.9,440,305,975.88 zimeshalipwa kwa wateja ambao wenye amana katika Benki sita za Wananchi (*Community Banks*) kama zilivyotajwa hapo juu ukiiondoa

Benki ya *FBME*. Malipo hayo ni sawa na asilimia 77.27 ya kiasi cha Sh.6,393,690,743.89 zilizotengwa kwa ajili ya kulipa fidia. Aidha, jumla ya wateja waliolipwa ni 21,675 kati ya wateja 57,076 ikiwa ni asilimia 37.98 ya wateja waliokuwa na amana zilizostahili fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Benki ya *FBME*, hadi mwishoni mwa mwezi Desemba 2020, jumla ya Sh.2,428,779,092.11 zimelipwa kwa wateja wenye amana ambazo ni sawa na asilimia 52.13 ya kiasi cha Sh.4,659,011,005.76 zilichotengwa. Aidha, jumla ya wateja waliolipwa ni 3,443 kati ya wateja 6,628 ambao ni sawa na asilimia 51.95 ya wateja waliokuwa na amana zinazostahili fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, wateja waliokuwa na amana inayozidi Sh.1,500,000/= watalipwa kiasi kilichobakia chini ya zoezi la ufilisi ambalo kwa mujibu wa sheria na taratibu za ufilisi kitakacholipwa kitategemea fedha zitakazopatikana kutokana na kuuza mali za benki husika. Zoezi hilo la kukusanya madeni na mali za benki hilo linaendelea ili kupata fedha za kuwalipa wateja wenye amana zenye thamani zaidi ya Sh.1,500,000/=. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ali Hassan King, swalii la nyongeza.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha kwa majibu yake mazuri na amenipa mwongozo na yametoa matumaini, lakini nina maswali mawili mdogo ya nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la kwanza, kwa kuwa ni wengi walioweka amana zao pale walitumia viinua mgongo vyao kuweka amana katika Benki ya *FBME*, hasa kule kwetu Zanzibar nilikotoka. Amesema wamelipwa wateja nusu na waliobakia bado hawajalipwa na watakaolipwa watalipwa kutokana na fedha ambazo watapata *amount* ambayo haitazidi 1,500,000/=; na kwa kuwa hii benki ni ya

nje; na kwa mujibu wa Sheria ya Benki na *Financial Institutions*, *BOT* ndio wenyе dhamana ya kukaribisha mabenki ndani, swali langu; 'je, ni lini watalipwa fedha zao zote kwa sababu, benki hii hajafilisika *FBME*?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni lini Benki Kuu ya Tanzania itaacha kuingiza benki hovyo hovyo kama hizi za kutoka nje zikaleta madhara katika nchi yetu? Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Hassan King kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza alilouliza Mheshimiwa King amesema kwamba, lini wateja hao ambao wana amana zao katika benki ya *FBME* watapatiwa fedha zao. Kama nilivyoeleza katika jibu la msingi, wateja waliokuwa na amana zaidi ya shilingi 1,500,000 watalipwa kiasi kitakachobaki chini ya zoezi la ufilisi wa benki ambapo kwa mujibu wa sheria na taratibu kiasi kitakacholipwa kitategemea fedha zitakazopatikana kutokana na kuuza mali za benki husika. Suala hili liko chini ya mujibu wa sheria, kwa hivyo sheria zitakapomalizika Mheshimiwa King basi, wateja wote wenyе amana katika benki hiyo watalipwa pesa zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; anaulizia lini benki zitatoa ukomo wa kuchukua benki ambazo hazina faida katika nchi yetu. Mheshimiwa King jibu lako la pili naomba nilichukue ili nikalifanyie kazi na nitakujibu kwa barua ili uelewe maelezo zaidi katika Serikali yetu, uweze kupata ufanuzi zaidi wa kupata jibu lako sahihi. Ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa. Nataka tu niongezee kakipengele kadogo kale ambako kanaongelea lini hawa watu watapata fedha. Kwa benki hii ambayo Mheshimiwa Mbunge ameuliza utaratibu huu ambao ameuelezea Mheshimiwa Naibu Waziri umekuwa mrefu kwa sababu benki hii ilikuwa ina-*operate* katika nchi mbili. Kwa maana hiyo, ule utaratibu wa mufilisi kuweza kukusanya madeni na kukusanya na mali zote ili azibadilishe ziwe fedha ili aweze kuwalipa wale wateja ambao amana zao zilikuwa zinazidi kile kiwango cha awali ambacho wanapewa pale benki inapokuwa kwenye mufilisi, kikamiliike. Kwa hiyo, hicho kikishakamilika hapo ndipo ambapo mufilisi ataweza kufanya hiyo kazi ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameisema na hawa wateja waweze kupata hizo fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la pili ambalo Mheshimiwa muuliza swalii ndugu yangu King amesema ni lini Benki Kuu itaacha kuruhusu mabenki yaingine hovyo hovyo. Nimhakikishie kwamba, mabenki hayaingii hovyo hovyo na Serikali inafanya *due diligence* kwa kila benki inapotaka kufanya kazi hapa nchini na ndio maana Benki Kuu iliingilia kati ilipoona baadhi ya mabenki hawaendi sawasawa na vile ambavyo yanatakiwa yafanye kwa mujibu wa sheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe rai tu kwa wananchi wetu kwa sababu, huwa kuna *report* zinazotolewa kila miezi mitatu na kunakuwepo na mukutano mkuu wa wadau wa benki na sisi tuwe tunafuatilia ili tuweze kuona mienendo ya benki. Tusingubirie tu Benki Kuu ambaye ni msimamizi aweze kufanya jukumu hilo ambalo linawahusu pia, wadau wadau wa benki ambao wanatakiwa watoe muongozo kwa benki yao. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalii lake.

Na. 21

## **Mashamba Yasiyoendelezwa Kata za Daa na Oldeani**

**MHE. CECILIA D. PARESSO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuyagawa kwa wananchi mashamba makubwa yanayomilikiwa na wawekezaji katika Kata za Daa na Oldeani, Wilayani Karatu ambayo hayaendelezwi huku wananchi wakikosa ardhi kwa ajili ya makazi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, ni mara yangu ya kwanza kusimama toka Bunge la Kumi na Mbili limeanza, naomba unipe fursa na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema, lakini nimshukuru sana Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuniamini tena katika kipindi hiki cha pilii, kunipa dhamana ya kuwa Naibu Waziri katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Aidha, niwashukuru Wanailemela wote walionipa fursa hii ya kuweza kuwatumikia kwa miaka mingine mitano na kwa leo nitoe pole kwa msiba mkubwa wa Mkuu wa Shule ya Bwiru, shule ya ufundi, Ndugu Elias Kuboja ambaye amefariki dunia. Nawapa pole Wanailemela.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresto, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikifanya kazi ya uhakiki na ukaguzi wa mashamba makubwa nchini ili kubaini uzingatiwaji wa masharti ya umiliki yaliyotolewa. Hatua zilizochukuliwa na Serikali ni pamoja na kubatilisha milki

za mashamba ambayo wamiliki wamekiuka masharti ya uendelezaji. Katika kipindi cha miaka mitano (2015 – 2020) jumla ya mashamba 45 yenye jumla ya ekari 121,032.243 yalibatilishwa kutokana na waliokuwa wamiliki kushindwa kutekeleza masharti ya umiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kata za Daa na Oldeani Wilaya ya Karatu, kuna mashamba 25 ambayo yalimilikishwa kwa wawekezaji kwa ajili ya shughuli mbalimbali hususan kilimo na ufugaji. Taarifa za awali za uhakiki zinaonesha kuwa mashamba hayo yameendelezwa kwa viwango tofauti ambapo mashamba tisa yameendelezwa kwa wastani wa asilimia 50. Sehemu nyingine ya mashamba hayo imejengwa miundombinu ya barabara na huduma za jamii kama vile shule, nyumba za kulala wageni, viwanda, vituo vya watalii na kadhalika. Kwa sasa Serikali inaendelea kufanya uhakiki wa kina wa mashamba yote na kuchukua hatua kwa wamiliki ambao wameshindwa kutimiza masharti ya umiliki.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, katika kata husika nilizozitaja katika swali langu la msingi kuna baadhi ya mashamba wawekezaji wamehifadhi mapori ambayo hawayaendelezi. Mapori hayo yanahifadhi pia wanyama ambao ni hatarishi kwa wakati katika maeneo hayo.

Je, Serikali sasa wako tayari kwa kushirikiana na halmashauri kwa sababu, imekuwa ni changamoto ya muda mrefu, kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Karatu kuhakikisha wanayatambua haya maeneo na kufanya *partial revocation* na yale maeneo yarudi kwa wananchi ili wananchi wanaozunguka maeneo hayo pamoja na wanafunzi wanaoenda shule waishi katika maeneo salama bila kuathiriwa na maisha yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, katika mashamba hayo hayo niliyoyataja, kuna shamba mojawapo linaitwa Shamba la Benduu, mwekezaji alishafariki, nitamwandikia Mheshimiwa vizuri kwa karatasi; mwekezaji alishafariki, lile shamba wafanyakazi wake hawajalipwa takribani miezi nane na hawaruhusiwi kwenda kufanya kibarua kwenye mashamba mengine, hawajui hatima ya haya maslahi yao na hawajui hatima ya nini wafanye kwa sababu, wakitoka kwenda kufanya kazi kwenye shamba lingine anafukuzwa asirudi kwenye lile shamba. Je, sasa Serikali wako tayari kwenda kutatua mgogoro uliopo katika shamba hilo, ili wananchi wanaofanya kazi na vibarua wanaofanya kazi katika eneo hilo wapate haki zao na pia waruhusiwe kufanya kazi katika maeneo mengine, ili waendelee kujipatia kipato? Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazih majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Paresto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza ameongelea kwamba, baadhi ya mashamba yamefanywa mapori na yanafuga wanyama kule amba pengine ni hatarishi kwa watu na anaomba pengine yaweze kufanyiwa *partial revocation* kwa maana ya kwamba, ile sehemu ambayo pengine haitumiki basi iweze kuondolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, siwezi kutoa jibu la moja kwa moja kwa sababu, ni mpaka anachokisema hicho kiwe na uhakika kwa sababu, unapopewa shamba kuna muda wake wa kuweza kuliendeleza, ndani ya miaka mitano unatakiwa kuwa umeendeleza angalau moja ya nane ya hilo shamba. Sasa kama mashamba hayo hayajaendelezwa kwa kiwango hicho kwa sababu, tumeshasema uhakiki unaendelea kufanyika basi, tutapita pia kuona hilo shamba likoje, lakini

kama nilivyosema mwanzo mashamba yote 25 ya Wilaya ya Karatu yamefanyiwa uhakiki na kwa sehemu kubwa yameendelezwa zaidi ya asilimia 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili anaongelea Shamba la Benduu, nadhani atanipa karatasi, kwamba, mwekezaji alikwishafariki na watumishi wale wanadai hawana malipo. Nadhani hili ni suala la kisheria zaidi kwa sababu, kama mtu amefariki kuna mtu ambaye anatakiwa kuwa *administrator* wa mali ya yule aliyefariki. Kama atakuwa ameteuliwa msimamizi wa mirathi katika eneo lile basi, huyo atabeba dhamana pia ya kuweza kulipa wafanyakazi ambao wanadai, wanayemda alishafariki na tayari kuna mtu ambaye anasimamia mirathi ile atashughulikanao katika suala zima la kuweza kupata haki zao.

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mbunge wa Viti Maalum, kwa niaba yake.

Na. 22

### **Ongezeko la Wagonjwa wa Afya ya Akili**

**MHE. LUCY T. MAYENGA (K.n.y. MHE. MARIAM N. KISANGI)** aliuliza:-

Nchi yetu imekuwa na ongezeko kubwa la wagonjwa wa Afya ya Akili:-

- (a) Je, nini chanzo cha ugonjwa huo?
- (b) Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuwasaidia wagonjwa hao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,  
WAZEE NA WATOTO alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, afya ya akili ni ile hali ya mtu kuwa na uwezo wa kukabiliana na changamoto za kimaisha ikiwemo utambuzi, uzalishaji wa mali, kutunza familia na kumudu shughuli za kijamii. Magonjwa ya akili ni pale mtu anaposhindwa kukabiliana na changamoto za kimaisha ikiwa ni pamoja na kushindwa kumudu shughuli za kijamii, kujitunza, hisia na utambuzi ambapo sababu za magonjwa haya ni mchanganyiko wa sababu za kibailolojia, kisaikolojia na kimazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na ongezeko la magonjwa haya, Serikali imefanya yafuatayo:-

(1) Kuandaa Sheria ya Afya ya Akili ya Mwaka 2008 ambapo sheria hii inatoa mwongozo na utaratibu wa namna ya kuwapokea na kuwashudumia watu wenye ugonjwa wa akili.

(2) Kuandaa Sera na miongozo ambapo wagonjwa wa afya ya akili ni mionganoni mwa makundi maalum ambayo huduma zake zinaweza kutolewa kwa msamaha kwa watu ambaao hawana uwezo.

(3) Serikali inahakikisha kuwa huduma hizi zinatolewa katika ngazi zote za huduma za afya kuanzia kwenye jamii, ngazi ya afya ya msingi, mkoa, kanda, mpaka hospitali maalum ya Taifa ya afya ya akili.

(4) Kuhakikisha upatikanaji wa dawa muhimu za afya ya akili kwenye vituo vyote vya huduma za afya.

(5) Kuongeza udahili wa wanafunzi wa uzamivu (*Masters*) katika masomo ya wagonjwa wa akili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Mayenga, swalii la nyongeza.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa muda mrefu kwenye kundi hili la watu wenye matatizo ya akili baadhi yao wamekuwa wakipata matatizo ya kisheria na kuweza kuchukuliwa hatua mbalimbali ikiwemo kufungwa, lakini kwa sababu tiba hii na ugunduzi wa watu wa aina hii huwa inachukua muda mrefu sana, kwa maana ya kwamba, mtu anakuwa na matatizo ya akili, lakini uthibitisho kwamba, huyu anakuwa na matatizo ya akili unachukua muda mrefu. Je, Serikali sasa iko tayari kwa kundi hili maalum kwa matatizo haya walijonayo wakaongeza muda wa jinsi ya kuwahudumia watu hawa, hasa wafungwa, lakini zaidi waweze kuwa na kitengo maalum cha kuhudumia watu hawa, ili badala ya kuteseka muda mrefu kwenye jela na mahabusu, basi waweze kupata huduma mapema ili kuweza kuchukuliwa hatua mapema?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swalii la Mheshimiwa la nyongeza, lakini naomba kuongezea kidogo pale mwanzo kwenye vyanzo vya sababu zinazosababisha ugonjwa wa afya ya akili, ili ikibidi na sisi wenyewe tuwe mabalozi wa kuweza kudhibiti hivi vyanzo maana vingine ni vya kawaida kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, zimetajwa sababu za kibaolojia ambazo ni vinasaba vile ambavyo mtu amekuwa ameumbwa navyo. Unaweza ukawa unavyo lakini usifikie stage ya kuweza kupata huu ugonjwa kutokana na mazingira unayoishi nayo katika jamii yako na wewe mwenyewe yanavyokuandaa kupata au kutokupata. Naweza nikatoa mifano hai hapa kuhusu matumizi ya vilevi kupita kiasi mfano

bangi au pombe kupita kiasi, kama mwili wako katika maumbile yake unavyo vile vinasaba unaweza ukajikuta unaangukia kwenye ugonjwa wa kukosa akili. Kwa hiyo, inabidi jamii yetu tunakokwenda huko tuishi vizuri, matumizi ya kila kitu ni kwa kiasi, yasije yakakusindikiza kwenye kupata ugonjwa huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tuna watu wanawafanyia wenzao ukatili. Ukatili ukianza kufanyika kwenye maisha ya binadamu katika hatua zake zote siyo jambo jema. Sisi kama Waheshimiwa Wabunge ni mabalozi wazuri wakuweza kukemea vitendo vyta ukatili maana vinaweza vikawapeleka kupata msongo hatimaye kupata ugonjwa huu wakawa hatari kwenye taifa letu na kwenye jamii yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna masuala jinsi gani mwanadamu anachukulia maisha yake, zile changamoto, watu wanasema wana ugumu wa maisha, hili nalo ni suala la kukaa na jamii iweze kuchukulia *positive* changamoto mbalimbali na siyo kujivekea msongo wa mawazo kufika huko kusikotakiwa. Dunia imeendelea sana nayo ni shida kwa watoto wetu wanapoangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala lile lingine la pili naomba nilipokee, kweli umuhimu huo upo. Tutajipanga kama Wizara kuona jinsi gani tunatoa huduma hiyo ya kuharakisha hayo mashauri yaishe yanayotokana na afya ya akili. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Maji, Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, sasa aulize swalilake.

Na. 23

**Mradi wa Maji-Same-Mwanga-Korogwe**

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID** aliuliza:-

Upatikanaji wa maji katika Mji mdogo wa Same ni asilimia 34; na mradi mkubwa wa maji Same – Mwanga – Korogwe umechelewa kwa zaidi ya mwaka mmoja sasa:-

(a) Je, ni kitu gani kilichochelewesha mradi huo na ni hatua gani zimechukuliwa kwa watu waliohusika na ucheleweshaji huo?

(b) Je, ni lini sasa mradi utakamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa mema yote ambayo amenijalia hata siku ya leo nami nimekuwa mmoja wa Wabunge katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa imani kubwa aliyoonyesha juu yangu kwa sababu Bunge la Kumi na Mbili ni Bunge ambalo hakika Wabunge wote wako imara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Mbeya kwa kunipa imani kubwa na kuona naweza kuja kuwawakilisha na kulisukuma gurudumu la maendeleo. Nakushukuru wewe binafsi Naibu Spika kwa sababu nawe ni mpiga kura wangu halali na mwaminifu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kushukuru familia yangu, hasa mume na baba yangu mzazi pamoja na watoto wangu waliofanikisha kuwa hivi nilivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swalii la Mhe. David Mathayo David,

Mbunge wa Same Magharibi, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza Mradi Mkubwa wa Maji wa Same-Mwanga-Korogwe kwa gharama ya shilingi bilioni 262. Mradi huu unahusisha ujenzi wa miundombinu ya chanzo cha maji, ulazaji wa bomba kilomita 71, vituo vya kusukuma maji 3 na matanki 7 yenye ujazo kuanzia lita laki tatu hadi milioni tisa na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji kilomita 204. Katika utekelezaji mradi huu mkataba wa mwisho ultarajija kukamilika Machi, 2021. Hata hivyo, kumekuwepo na kasi ya utekelezaji usiyoridhisha hadi Serikali imefikia hatua ya kusitisha mikataba na wakandarasi mwezi Desemba, 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inafanya juhudii kuhakikisha taratibu za kupata wakandarasi wapya wa kumalizia kazi za mifumo ya umeme na ulazaji wa bomba kuu kilomita 34.

Aidha, kazi za ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji zinatekelezwa na wataalam wa ndani wa Wizara wakishirikiana na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kwa kumtumia mkandarasi wetu Seprian Lwemeja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatarajia mradi huu ukamilike Desemba 2021 na utanufaisha wananchi wapatao 438,820 kwa Mji wa Same-Mwanga pamoja na vijiji 38 vya Wilaya ya Same, Mwanga na Korogwe. Awamu ya kwanza itahudumia wananchi 168,820 katika miji ya Same na Mwanga. Awamu ya pili ambayo utekelezaji wake utaanza mwaka wa fedha 2021/2022 utanufaisha wananchi 270,000 katika vijiji vilivyo eneo la mradi ambapo Wilaya ya Same ni Hedaru, Mabilioni, Gavao, Makanya, Mgiasi, Bangalala, Chanjo, Mwembe, Njoro, Majengo, Bendera, Mkonga, Ijinyu na Mgandu; Wilaya ya Mwanga ni Kifaru, Kiruru Ibwejewa, Kisangara, Lembeni, Kivegere, Mbambua, Kileo, Kivilini, Kituri na Mgagao; na Wilaya ya Korogwe ni Bwiko, Mkomazi, Nanyogie, Manga-Mtindilio na Manga-Mikocheni.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii niulize maswali mawili ya nyongeza lakini kwanza nipende kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuweka msukumo kwenye mradi huu. Pia nipongeze Serikali kwa maana ya Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kufanya kazi vizuri na kufuatilia vizuri mradi huu na kuondoa wakandarasi ambao ni wazembe ambao wanachelewesha huduma kwa wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza la nyongeza, kwa kuwa Desemba ni mbali kwa mahitaji ya maji katika Mji Mdogo wa Same kata za Njoro, Kisima, Stesheni pamoja na Same Mjini; na kwa kuwa Serikali hivi sasa inachilmba visima viwilli virefu, je, visima hivii vitakamilika lini ikiwa ni pamoja na kuweka *pump* kusudi wananchi hawa waweze kupunguza makali ya ukosefu wa maji kabla ya Desemba kufika?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuongozana nami baada ya Bunge hili ili twende tukakague kata kwa kata, kijiji kwa kijiji, kitongoji kwa kitongoji kuhusiana na utekelezaji wa mradi huu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu kwa maswali haya.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli tunafahamu kwamba Desemba ni mbali na maisha lazima yaendeleee. Sisi Wizara ya Maji tuko imara kabisa kuhakikisha kwamba tatizo sugu la maji tunakwenda kulishughulikia kwa haraka sana. Wizara tumejjipanga vyema chini ya Jemedari wetu Mheshimiwa Jumaa Aweso ambapo katika Mji wa Same kisima kipywa kimeshachimbwa eneo la Stelingi chenye kina

cha mita 200. Kazi hii ilianza Oktoba 2020 na itakamilika mwezi huu Februari 2021. Kama *Quick-win program* ya kuongeza uzalishaji wa maji katika Mji wa Same utahudumiwa na visima virefu viwili vilivyopo Stelingi na Kambambungu pamoja na chemichemi mbili za Mahuu na Same Beach.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa suala la kuongozana na wewe Mheshimiwa Mbunge usiwe na hofu, hiyo ndiyo shughuli yangu. Mheshimiwa Mbunge nitampa upendeleo mara baada ya Bunge hili tutakwenda, tutahakikisha wananchi wa Same Magharibi wanapata maji ya kutosha na hilo tatizo litabaki kuwa historia. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na napenda kumjulisha tu Mheshimiwa David kwamba timu kubwa ya *club* kubwa ya pale Msimbazi iko humu ndani basi na kesho tunakukaribisha. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mmesimama wengi lakini maswali yetu bado ni mengi sana, kwa hiyo, mtuwie radhi majibu yamekuwa marefu kidogo siku ya leo.

Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Meatu, sasa aulize swalilake.

Na. 24

### **Upungufu wa Maji Safi na Salama Mwanhuzi –Meatu**

**MHE. LEAH J. KOMANYA** aliuliza:-

Mji wa Mwanhuzi unakabiliwa na tatizo kubwa sana la maji safi na salama kutokana na chanzo chake cha maji cha bwawa la Mwanyahina kujaa tope:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha wananchi wa Mji wa Mwanhuzi na vitongoji vyake wanapata maji safi na salama ya kutosha kwa mwaka mzima?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Jimbo la Meatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Mwanhuzi, Wilayani Meatu unategemea chanzo kimoja cha Maji ambacho ni Bwawa la Maji la Mwanyahina. Bwawa hilo lilijengwa mwaka 1999 lenye uwezo wa kuhifadhi maji mita za ujazo millioni 1.6. Bwawa hili kwa sasa limejaa tope jingi na kusababisha kupungua kina cha kuhifadhi maji kutoka kina cha mita 9 hadi mita 5 zinazohifadhi maji kwa matumizi ya wakazi wa Mji wa Mwanhuzi na vijiji jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha huduma ya maji katika mji wa Mwanhuzi na vitongoji vyake, Serikali imekamilisha utafiti, usanifu na kuanza kutekeleza ujenzi wa chanzo mbadala cha ukusanyaji na usafirishaji wa maji kutoka bonde la Mto Semu hadi kwenye matanki yanayotumika kusambaza maji katika Mji wa Mwanhuzi. Gharama za mradi huo shilingi milioni 742. Tayari Serikali imetuma kiasi cha shilingi milioni 276.6 kwa ajili ya kazi hizo za ujenzi wa mradi mbadala wa kutoa maji katika bonde la Mto Semu na kuyapeleka mjini Mwanhuzi. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa lengo la kutatua tatizo la muda mrefu katika mji wa Mwanhuzi na vitongoji vyake, Serikali ipo katika hatua za awali za kutekeleza mradi mkubwa wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria unaolenga kumaliza changamoto za huduma za maji katika mkoa wa Simiyu zikiwemo Wilaya za Busega, Bariadi, Maswa, Itilima na Meatu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, swalii la nyongeza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Mradi huu ulizinduliwa mwaka 2009 na baadaye ulikabidhiwa katika Mamlaka ya Maji Mwanhuzi lakini ulipokabidhiwa usambazaji wa maji haukufanyika kama ulivyokusudiwa. Nataka kujua Serikali ina mkakati gani kuhakikisha vitongoji vya Mwambegwa, Bulianaga, Jileji na Vibiti vinasambaziwa maji ikiwemo kujengewa tanki kuititia Wakala wa Maji Vijijini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba maji ya Bwawa la Mwanyahina yamefikia kiwango cha mwisho, yakitibiwa hayawezi kutakasika na wananchi tumekuwa tukiwatumanisha kuhusu ujio wa mradi wa wa maji wa Ziwa Victoria. Nataka kujua Serikali katika utekelezaji wake wa hatua za awali umefikia hatua zipi? Nashukuru. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Komanya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Ziwa Victoria tayari utekelezaji wa awali unaendelea. Vilevile ili kuendelea kuhakikisha vijiji hivyo alivyovitaja vinaendelea kupata huduma ya maji wakati tukisubiri mradi ule wa muda mrefu tayari wataalam wetu wameweza kufanya usanifu na kuweza kuweka mkakati wa kuchimba visima 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa tayari visima vitatu vimechimbwa na viwili angalau vimeonyesha kwamba vina maji ya kutosha. Pale Mwandoya lita 40,000 kwa saa itaweza kupatikana katika moja ya visima ambavyo vimechimbwa.

Vilevile Mwankoli kisima kimeweza kupatikana chenye uwezo wa kutoa maji lita 8,500 kwa saa. Kwa hiyo, Wizara itaendelea kuhakikisha kuona kwamba maeneo yote tunayashughulikia na maji yanapatikana bombani.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaenda Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, sasa uliza swali lake.

Na. 25

**Hitaji la Umeme – Vijiji 32 vya Jimbo la Lushoto**

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuvipatia umeme vijiji 32 vya Jimbo la Lushoto ambavyo havina umeme?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto na tabibu wetu humu ndani, kwa wale ambao tunaamini kikombe, kama ifuatavyo:- (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) inatekeleza miradi ya kusambaza umeme vijijini kwa awamu kadri ya upatikanaji wa fedha. Malengo ya Serikali ni kufikisha umeme katika vijiji vyote vya Tanzania Bara ifikapo Desemba, 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iko katika hatua za mwisho kukamilisha maandalizi ya ujenzi wa mradi wa kusambaza umeme vijijini awamu ya tatu mzunguko wa pili (*REA III round two*). Kwa Wilaya ya Lushoto Mradi wa REA III mzunguko wa pili unapeleka umeme katika maeneo ya vijiji vyote 32 vya Jimbo la Lushoto ambavyo havikupata umeme kupitia miradi ya kusambaza umeme ya awamu ya pili na awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za mradi ya kusambaza umeme kwa Wilaya ya Lushoto zinajumuisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33; urefu wa kilomita 131.8; njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 0.4 umbali wa kilomita 381.9; ufungaji wa transfoma 99 za 50kVA; pamoja na kuwaunganishia umeme wateja wa awali 1,984. Mradi unakadiriwa kugharimu shilingi bilioni 16.8. Utekelezaji wa mradi utaanza Februari, 2021 na kukamilika ifikapo Desemba, 2022.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shabani Shekilindi, swalii la nyongeza.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimshukuru Waziri kwa majibu yake mazuri. Kwa kuwa mradi wa REA utaanza Februari hii ambapo leo ni tarehe 3 na katika Jimbo la Lushoto kuna vijiji vimerukwa kwa muda mrefu sana hasa katika Vijiji vya Kilole, Ngulu, Gale, Miegeyo, Handei, Magashai, Tambwe, Mazumbai, Ngwelo, Milungui na kata nzima ya Makanya. Je, Serikali haionii kwamba sasa vijiji hivi lazima vipewe kipaumbele kwa ajili ya kupata umeme kwa sababu wamesubiri kwa muda mrefu sana?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, Jimbo la Lushoto lina vitongoji zaidi ya 32 na Mheshimiwa Waziri Kalemani yeye ni shahidi ametembelea Lushoto na akaona Wilaya nzima ya Lushoto hakuna nyumba ya nyasi hatia moja na wananchi wote wameshafanya *wiring* wanasubiri umeme. Je, ni lini sasa vitongoji vile vya Wilaya ya Lushoto vitapata umeme kwa wakati ili wananchi wapate huduma stahiki kama wenzao wanavyopata huduma?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, *commitment* ya Serikali ni kwamba, ifikapo tarehe 15 Februari, 2021 vijiji vyote vilivyobakia 2,150 ambavyo havikuwa

vimepata umeme katika *REA* Awamu I, II na III mzunguko wa kwanza vitapelekewa umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu uliofanyika sasa hivi ni kuhakikisha kwamba mkandarasi mmoja hapewi kazi kubwa sana. Kwa hiyo, tutaona maajabu makubwa katika kipindi hiki ambapo tutaanza kupeleka umeme katika maeneo mengi kwa wakati mmoja kwa sababu mkandarasi mmoja pengine inaweza ikawa anapeleka umeme au jimbo moja. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Shekilindi, kwamba huduma anayotupatia ya dawa na sisi tutapeleka huduma ya umeme kwenye kwa kadri tulivyoelekeza katika kipindi hiki hiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swalii la pili la kupeleka umeme kwenye vitongoji, Wizara ya Nishati kwa maelekezo ya Serikali inatekeleza mradi unaoltwa *densification* na sasa tuko katika *densification* 2B amba ni mradi jazilizi kwa ajili ya kupeleka umeme katika vitongoji na kufikia mwezi Mei tutakuwa tayari tumesaini mikataba kwa ajili ya kupeleka umeme kwenye vitongoji zaidi ya 2,800 katika nchi yetu ya Tanzania. Kwa hiyo, tunaamini katika upanuzi huo wa miradi jazilizi, basi Jimbo la Lushoto pia litapata maeneo kadhaa ya kuwekewa umeme katika maeneo ya vitongoji vyake. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tuendelee na swalii la Mheshimiwa Augustine Vuma Holle, Mbunge wa Kasulu Vijijini, swalii lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Assa Makanika, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, hata kama yupo nimeletewa ujumbe kwamba atauliza huyo Mbunge wa Kigoma Kaskazini.

**MHE. VUMA A. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, hapana nipo.

**NAIBU SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Vuma aliyeleta ujumbe ni wewe au amejieletea yule Mheshimiwa Assa Makanika?

**MHE. VUMA A. HOLLE:** Alikuwa anaomba swalii la nyongeza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Augustine Holle Vuma.

Na. 26

### **Kigoma Kuunganishwa na Umeme Grid ya Taifa**

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE** aliuliza:-

Je, ni lini Mkoa wa Kigoma utaunganishwa na umeme wa Gridi ya Taifa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Augustine Vuma Holle, Mbunge wa Kasulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kigoma unapata umeme kuititia mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia mafuta ya *diesel*/ambayo ni gharama kubwa kwa TANESCO na Serikali kwa ujumla. Katika hatua ya haraka, Serikali inatekeleza mradi wa kuunganisha Mkoa wa Kigoma katika Gridi ya Taifa kutoka Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu utahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 132 kutoka Tabora hadi Kigoma kuititia Urambo na Nguruka umbali wa kilomita 395, pamoja na ujenzi wa vituo vya kupozea umeme wa msongo wa kilovoti 132 kwenda 33 vya Urambo, Nguruka na Kidahwe Mkoani Kigoma. Gharama za mradi huu ni shilingi bilioni 142.7 na mradi ulianza ujenzi mwezi Juni, 2020 na unatarajia kukamilika mwezi Juni, 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua nyingine Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa njia kuu za kusafirisha umeme, msongo wa kilovoti 400 yenye urefu wa kilomita 280 ya kutoka Nyakanazi Mkoa Kagera hadi Kidahwe Mkoani Kigoma. Mradi huu unahuishisha ujenzi wa vituo viwili vyta kupoza umeme msongo wa kilovoti 400 kuja 220 kwenda 132 mpaka 33 na 400/132/33 vyta Nyakanazi vyenye transfoma mbili zenyte ukubwa wa *MVA* 120.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa mradi huu pia ulianza mwezi Januari mwaka 2020 na utakamilika mwezi Juni, 2022. Gharama ya mradi ni dola za Kimarekani milioni 187 chini ya ufadhili wa Serikali ya Tanzania, Benki ya Maendeleo ya AfDB pamoja na Benki ya Maendeleo ya Korea.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Augustine Vuma Holle, swali la nyongeza.

**MHE. VUMA A. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, Wilaya ya Kasulu kuna mgao mkubwa sana wau meme. Yako maeneo hasa maeneo ya Makele, kila ikifika jioni lazima umeme ukatike na wananchi wanakosa huduma ya kuangalia tarifa ya habari, lakini na maeneo mengine mengi ya Wilaya ya Kasulu. Nataka kujua majibu ya Serikali nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba tena wa muda mfupi, kwamba unakomesha mgao huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Mkoa wa Kigoma, *REA* awamu ya III imeanza kwanza kwa kuchelewa lakini pili maeneo mengi hayajafikiwa na mradi, lakini pia mradi huo unasuasua. Je, Waziri yupo tayari kutuma wataalam wake au ye ye mwenyewe kuja Mkoa wa Kigoma hasa Kasulu Vijijini ili kuhakikisha kwamba anakutana na wakandarasi ili waweze ku-speed up utekelezaji wa mradi? Nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati, majibu.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri wangu, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Vuma, Mbunge wa Kasulu Vijijini, kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Vuma pamoja na Wabunge wengine wote kutoka Kigoma, kwa kazi kubwa walizofanya katika kufuatilia Mkoa wa Kigoma kupata Gridi ya Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kulikuwa na changamoto kubwa sana ya kiumeme katika Mkoa wa Kigoma na Mkoa wa Katavi, lakin kama ambavyo limejibowi kwenye swali la msingi, Serikali imeanza kutekeleza mradi wa kupeleka umeme wa Gridi katika Mkoa wa Kigoma kutoka Tabora. Tumeanza kujenga toka mwakajana mwezi Januari, kutokea Urambo, tunajenga *sub-station* na tumeshaanza kujenga na tumeshaanza kujenga *sub-station* ya pili tunajenga Nguruka na ujenzi unaendelea na *sub-station* ya tatu tunajenga Kidahwe Mjini Kigoma, nako ujenzi unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunajenga njia ya kusafirisha umeme mkubwa kilovoti 400 kutoka Kigoma na kusambaza maeneo yote ya Wilaya ya Kigoma ikiwemo, Kasulu, Kibondo, Kakonko na maeneo mengine na ujenzi umeshaanza. Naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Vuma, Mheshimiwa Profesa Ndalichako na Waheshimiwa Wabunge wengine wa Kigoma kwamba tunatarajia kukamilisha mwakani mwezi Desemba, shughuli zote na Gridi ya Taifa itakuwa imefika kwenye Mkoa wa Kigoma.

Pia kwa upande wa matumizi pia ya umeme Kigoma kwa sasa wanatumia mashine za mafuta ni vema nikawaambia Waheshimiwa Wabunge ili wajue, ingawa uendeshaji kwa kweli ni mkubwa na kwamba tunatambua mahitaji ya umeme, hatuna namna mbali na kuwalisha umeme kwa utaratibu huo kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya wananchi wa Kigoma kwa siku ni *megawatt* 5.2 pamoja na kwamba mashine tulizonazo pale ni *megawatt* 2.6 na tunazidisha mara nne zinifikisha kama *megawatt* 8 lakini kwa sababu ya njia kuwa ndefu na umeme unachotwa kwenye mafuta bado umeme ule unakuwa hauna nguvu. Ndio maana mnaona mara nyngi umeme unakatika sio mgao isipokuwa umeme unakatika kutokana na njia kuwa ndefu na *source* yake ni mafuta. Nimeona niliweke vizuri suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, maeneo ya *REA* yaliyobaki ni kweli katika Mkoa wa Kigoma na hasa Kasulu kwa Mheshimiwa Vuma, Mheshimiwa Vuma ana vijiji 61 na tumeshapeleka umeme kwenye vijiji 42 bado vijiji 19 na tulizindua pale Lusesa na Lusesa kazi inaendelea. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Vuma anavyofuatilia masuala haya na kwa sababu utekelezaji wa umeme katika vijiji vyote kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri unaanza tarehe 15 mwezi huu na tunarajia ndani ya miezi 18 kukamilisha vijiji vyote katika nchi yetu, vijiji vyote vya Mheshimiwa Vuma vitapata umeme mapema sana. Hata hapo Makere umeme unaokwenda kutoka pale mpaka mpakani mwa Rwanda na Burundi tutaunganisha na majirani zetu wa Rwanda na Burundi kuititia mradi wa Rusumo ili maeneo ya mipakani mwa Tanzania, Rwanda na Burundi nayo yapate umeme. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Abubakary Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero, sasa aulize swali lake. Simuoni kwa niaba yake Mheshimiwa Kunambi.

Na. 27

#### **Ujenzi wa Barabara ya Kidatu – Ifakara**

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI (K.n.y MHE. ABUBAKAR D. ASENGA)** aliuliza:-

Je, ni lini Ujenzi wa Barabara ya Kidatu hadi Ifakara utakamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Abubakar Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Kidatu – Ifakara ni sehemu ya Barabara Kuu ya Mikumi - Kidatu - Ifakara - Malinyi - Kilosa kwa Mpepo – Londo – Lumecha yenye urefu wa jumla ya kilometra 547. Barabara hii ni mionganoni mwa barabara muhimu katika Taifa kwa kuwa inaunganisha Mkoa wa Morogoro na mikoa yenye uzalishaji mkubwa wa mazao ya chakula na biashara ya Njombe, Ruvuma na Lindi kuitia Wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa barabara kati ya Kidatu hadi Ifakara yenye urefu wa kilometra 66.9 pamoja na Daraja la Ruaha Mkuu vinajengwa na Mkandarasi *M/S Reynolds Construction Company Limited (Nigeria)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali, kuitia Wizara ya Fedha na Mipango na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) inaendelea na Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii kwa gharama ya *Euro 40,441,890.81* takribani sawa na shillingi bilioni 113.13 bila VAT. Mradi ulitegemea kukamilika tangu tarehe 29 Septemba, 2020. Mradi huu umechelewa kukamilika kwa sababu za kimenejimenti kwa upande wa Mkandarasi. Hata hivyo, Serikali inaendelea kumsimamia Mkandarasi kwa karibu ili akamilishe mradi kama ilivyopangwa. Mradi huu umepangwa kukamilika mwezi Oktoba, 2021.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Godwin Kunambi, swalii la nyongeza.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize swalii moja la nyongeza. Kama alivyojibu Mheshimiwa Waziri, barabara hii ni barabara ya kitaifa yaani *National Road* na ni barabara inayounganisha Mkoo wa Njombe na Morogoro. Kutoka hapo Ifakara sehemu moja mpakani mwa Njombe na Morogoro, Mto Mfaji kuna kilomita takribani 225 na kwa kuwa barabara hii ni muhimu na ni barabara ya kitaifa, je, ni lini sasa Serikali itaanza ujenzi wa barabara kutoka Ifakara ng'ambo ya mto Lumemo kwenda kupita Mlimba, kwenda Mfaji, Madeke Njombe?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kuna haja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu...

**NAIBU SPIKA:** Hilo ni swali la pili? Au hilo hilo la kwanza?

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, la pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyahidi kufanya ziara Jimbo la Mlimba na katika ziara yake aliahidi ujenzi wa kilomita 60. Je, ni lini sasa Serikali itaanza ujenzi wa barabara hii walau kwa kilomita hizo 60?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri swalii la pili kama utakuwa huna majibu mtampelekea Mheshimiwa kwa maandishi, swalii la kwanza lina uhusiano na swalii la msingi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Asenga kwa juhudii ambazo anazifanya katika kufuatilia barabara hii ili kuhakikisha kwamba wananchi wa Kilombero wanafaidika na barabara hii ya lami ambayo wanaifuatilia. Baada ya maneno hayo, nitoe tu jibu la jumla,

kwamba katika hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati wa kuzindua Bunge hili la Kumi na Mbili, ukurasa wa 26 na 27, Mheshimiwa Rais ameahidi kwamba barabara zenyе urefu kilomita 2500 ambazo zinaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami zitakamilishwa katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ameenda mbali zaidi kwenye hotuba kwamba pia barabara zingine ambazo zitaanza kujengwa zenyе urefu wa kilomita 6006 ikiwepo barabara hii pia zitakamilishwa ambazo ni zile ambazo ziko kwenye ilani lakini na ahadi zake mwenyewe. Kwa hiyo, nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba hizi barabara Serikali itazikamilisha kama iliyooahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa tunaendelea na swali la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, swali hilo litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Jacquiline Ngonyani Msongozi.

Na. 28

#### **Kukamilisha kwa Uwanja wa Ndege Sumbawanga**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI (K.n.y MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA)** aliuliza: -

Je, ni lini ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Sumbawanga Mjini utakamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga ni mionganini mwa viwanja vya ndege vinne (4) ambavyo ni Kigoma, Tabora, Sumbawanga na Shinyanga vinavyotarajiwa kujengwa na kukarabatiwa kwa ufadhilli wa Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (*European Investment Bank – EIB*).

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu za makubaliano ya mkataba wa miradi hiyo baina ya Serikali (kupitia Wizara ya Fedha na Mipango) na Mfadhilli (Benki ya Uwekezaji ya Ulaya – *EIB*) tayari zimekamilika na idhini (*No Objection*) ya kuanza utekelezaji wa miradi yote minne (4) imetolewa na Mfadhilli wa miradi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa Mkandarasi (*M/s Sino Shine Overseas Construction & Investment East Africa Limited*) na Mshauri Elekezi (*SMEC International PTY Limited*) ikishirikiana na Kampuni ya *SMEC International Tanzania Limited* kwa ajili ya kutekeleza kazi hii, wamepatikana. Hivyo hivi sasa, Serikali iko katika hatua za awali za kuanza utekelezaji wa mradi huu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jacqeuline Msongozi, swali la nyongeza.

**MHE. JACQEULINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, kwa niaba ya Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum Rukwa, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Rukwa ni mkoa wenyewe vivutio vya utalii, lakini pia Mkoa wa Rukwa unajishughulisha na masuala ya uvuvi katika Ziwa Tanganyika. Mkoa wa Rukwa ni mkoa ambao umeshika nafasi ya tatu kitaifa katika uzalishaji wa mazao ya nafaka. Pamoja na hivyo Serikali bado hajijengwa uwanja huo. Swali la kwanza, je, Serikali haioni kama ucheleweshaji wa ujenzi wa uwanja huu unasababisha udumavu wa ukuaji kiuchumi wa Mkoa wa Rukwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, wananchi wa Mkoa wa Rukwa wamekaa muda mrefu sana hawajapata uwanja wa ndege; je, ni lini Serikali itaanza kujenga uwanja wa ndege wa Mkoa wa Rukwa ili kuwafanya wananchi wa Mkoa wa Rukwa wanufaika na matunda mazuri ya Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia kuhakikisha kwamba uwanja huu unajengwa. Katika swalii la kwanza la nyongeza ameeleza kwamba kuna vivutio vya utalii tunakubali uvuvi, lakini pia ni kati ya mkoa unaozalisha. Serikali tayari imeshapata fedha, sasa hivi kilichopo tu ni kuanza ujenzi. Kwa hiyo, kwa sababu hiyo Serikali imelitambua hili, hivyo, hakutakuwa na sababu ya kuwa na udumavu kwa sababu tayari uwanja huo utaanza haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itaanza kujenga uwanja huo? Katika jibu langu la msingi nimesema kila kitu kimeshakamilika, ni taratibu tu za mwisho za kibenki ambazo lazima zifanyike ili uwanja huo uanze. Kama mkandarasi tayari ameshapatikana kwa hiyo, tuna hakika ujenzi utaanza mara moja. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge twende kwenye swalii la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijiini.

Na. 29

**Ujenzi wa Barabara Karatu – Dongobesh – Haydom Singida**

**MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa barabara ya Karatu – Dongobesh – Hydom hadi Singida iliyotengewa fedha katika bajeti iliyopita utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WAJIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala kama hili lilijitokeza, swalii namba 7 ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Mbulu Mjini, kwa hiyo, inaonyesha ni kwa kiasi gani barabara hili ni muhimu na majibu yangu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mbulu – Haydom yenye urefu wa kilometra 70.5, ni sehemu ya barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti – Lalago – Maswa (km 398) inayohudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*). Kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Awali (*Preliminary Design*) wa barabara hii (kupitia mradi wa *Serengeti Southern Bypass*) ili kuijenga kwa kiwango cha lami, umekamilika. Kazi hii illifanywa na kampuni iitwayo H.P. Gauff Ingenieure GmbH & Co. KG – JBG mwaka 2016 kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa barabara hii ambayo itawezesha wananchi wa Mbulu kupata huduma katika Hospitali ya Haydom, Serikali ilianza kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya Mbulu – Haydom (km 50) kwa kiwango cha lami; ambapo katika mwaka wa fedha 2020/2021, shilingi bilioni tano zilitengwa. Utekelezaji wa mradi huu upo katika hatua za manunuzi na ujenzi wake utafanywa kwa njia ya Kusanifu na Kujenga (*Design and Build*). Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali imetenga fedha shilingi milioni 401 kwa ajili ya kuifanya

matengenezo mbalimbali barabara hii ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay, swalii la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kwa kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la kwanza, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri mwenyewe kwamba barabara hii ina umuhimu na sasa kwa miaka miwili imekuwa ikiwekwa kwenye bajeti na haikujengwa na amesema imetegwa shilingi bilioni 5, je, atuambie ni lini atatangaza tenda ili barabara hii ianze kujengwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, kwa kuwa anajua wazi kwamba bilioni 5 haiwezi kujenga barabara na barabara hii iko kwenye llani ya uchaguzi mwaka 2015-2020 na 2020-2025 na Mheshimiwa Rais ameahidi kwenye kampeni juzi hapa, je, yupo tayari kuweka fedha kwenye bajeti ya mwaka 2021/2022 ili kumaliza kilomita zingine 20 kufika 70 kufikia eneo la Haydom?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kwa pamoja ya Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Gregory Massay Mbunge wa Mbulu Vijijini jana pia aliuliza swalii la nyongeza lakini leo pia ameleta swalii la msingi, kwa hivyo, natambua jinsi anavyofuatilia barabara hii kwa ajili ya wananchi wa Wilaya ya Mbulu. Nimhakikishie kwamba kwa kuwa tayari fedha za awali zimeshatengwa hizo shilingi bilioni 5, kwa hiyo, taratibu za awali zitaanza ikiwa ni pamoja na

kutangaza tenda na kufanya shughuli za awali za kuanza ujenzi wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu swalii namba 28 kwamba Serikali imeahidi barabara zote ambazo imezitolea ahadi katika Ilani lakini pia ni ahadi za Rais katika kipindi cha miaka hii mitano zitatekelezwa ikiwa ni pamoja na barabara hii ya Karatu – Dongobesh - Haydom ambayo Mheshimiwa Massay Mbunge wa Mbulu Vijijini anaiulizia. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumalizie swalii la mwisho Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mbunge wa Mbinga Vijijini.

Na. 30

**Ujenzi kwa Kiwango cha Lami wa Barabara ya  
Kitai – Lituhi (Nyasa)**

**MHE. BENAYA L. KAPINGA** aliuliza:-

Je, ni lini barabara ya Kitahi – Lituhi kupitia Ruanda itaanza kujengwa ili kurahisisha usafirishaji wa makaa ya mawe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii liloulizwa na Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mbunge wa Mbinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, magari yote makubwa yanatakiwa yachukue makaa ya mawe katika eneo la Amani Makoro kwa ajili ya kupeleka maeneo mbalimbali nchini. Makaa ya mawe huchukuliwa na magari yenye uzito usiozidi tani 15 kutoka Mgodini (eneo la Ngaka) hadi Amani Makoro.

Ili kurahisisha uchukuaji wa makaa ya mawe kutoka Amani Makoro kwenda maeneo mengine nchini, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Ujenzi) kuititia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) imeanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kitahi – Lituhi (km 84.5) kwa awamu ambapo mpaka sasa km 5 kuanzia Kitahi hadi Amani Makoro (*Coal Stockpile*) zimekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetenga kiasi cha shillingi milioni 9,000 katika mwaka wa fedha 2020/2021 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa kiwango cha lami kwa kilometa tano nydingine. Kazi za ujenzi kwa sehemu hii zinatarajia kuanza mwishoni mwa Aprili, 2021. Aidha, ili kuhakikisha barabara yote inapitika kipindi chote cha mwaka, Serikali imetenga kiasi cha shillingi milioni 1,800 za matengenezo mbalimbali katika mwaka wa fedha 2020/2021.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Benaya Kapinga, swalii la nyongeza.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kufanya marekebisho, Naibu Waziri amesema Mbunge wa Mbinga Mjini mimi ni Mbunge wa Mbinga Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri yanayotia moyo. Pia nashukuru katika bajeti inayokuja ametutengea kilometra 5. Hofu yangu ni kwamba ikiwa mpango utakuwa ni wa kilometra tano tano barabara hii tunaweza kuikamilisha kwa muda wa miaka kumi na sita na kidogo. Je, Serikali ipo tayari kuongeza kasi ya ujenzi wa barabara hii ambayo imesubiriwa kwa muda mrefu na wananchi wa Jimbo la Mbinga Vijijini, Jimbo la Nyasa na wananchi wa Mkoa wa jirani wa Njombe?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, kwa kuwa hali ya barabara zinazohudumiwa na TANROADS kwa jimbo la Mbinga Vijijini sasa hivi hazipitiki ama zinapitika kwa shida sana. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuzifanya barabara hizi zipitike msimu mzima?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mbunge wa Mbinga Vijijiini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimuombe radhi sana Mheshimiwa Mbunge kwamba huyu ni Mbunge wa Mbinga Vijijiini na si Mbinga Mjini. Kwa hiyo, hata wananchi huko wanajua kwamba Mheshimiwa wao wa Mbinga Vijijiini yupo anatetea barabara zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo, sasa nijibu maswali yake mawili ya nyongeza. Mheshimiwa Mbunge anafahamu mara baada ya kuteuliwa hii barabara ni kati ya barabara ambazo mimi nimebahatika kwenda kuzitembelea, kwa hiyo, ninafahamu vizuri sana. Hata hivyo, tukubali tu kwamba ni jitihada za Serikali kwamba fedha inapopatikana hata kama ni kiasi kidogo zile barabara ziendelee kutengenezwa. Hata hizi kilometra 5 zilizotengenezwa zimesaidia sana kurahisisha usafirishaji wa makaa ya mawe, kwa hiyo, magari makubwa yanayopita pale hayawezi kukwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini tutatenga fedha zote, Serikali inafanya jitihada fedha zitakazopatikana naamini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kukamilisha barabara hii. Kwa sasa kadri tunavyopata fedha tutaendelea kutengeneza barabara kwa awamu na ndiyo maana hata hizi kilometra tano zilizotengenezwa zimetoa msaada mkubwa sana. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Nitaleta kwenu matangazo kabla hatujaendelea na ratiba nyingine, ninayo matangazo ya wageni. Wageni waliopo asubuhi hii tutaanza na wageni waliokaa katika jukwaa la Mheshimiwa Spika.

Kundi la kwanza ni wageni 6 wa Mheshimiwa Spika kutoka Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Yupo Mheshimiwa Jaji (Mst) Mathew Maimu ambaye ni Mwenyekiti wa Tume, karibu sana. Ameongozana na Mheshimiwa Mohamed Hamad ambaye ni Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Fatma Khalfan - Kamishna wa Tume; Mheshimiwa Thomas Masanja - Kamishna wa Tume; Mheshimiwa Amina Ali - Kamishna wa Tume; Ndgr. Fatuma Muya - Kaimu Katibu Mtendaji. Karibuni sana Viongozi wetu kutoka Tume za Hakiza Bianadamu na Utawala Bora (*Makofi*)

Kundi la pili ni wageni wa wengine wengine 34 wa Mheshimiwa Spika ambao ni wachezaji, viongozi... (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, msubiri basi kidogo tu tusome matangazo. (*Kicheko/Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, imetosha basi. Sasa mtulie kwa sababu mashabiki wa Yanga waliopo humu ndani wamekusudia kuwashangilia pia sasa mkishangilia peke yenu wanakuwa hawajaelewa tangazo. (*Makofi*)

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, inatosha tuendelee na wengine. (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Wageni 34 wa Mheshimiwa Spika, ambao ni wachezaji, viongozi na benchi la ufundu la Timu ya *Simba Sports Club* wakiongozwa... (*Kicheko/Makofi/Vigelegele*).

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwigulu acha vivu.

**NAIBU SPIKA:** Sasa wageni wetu muendeleee kusimama hivyo hivyo ili nimalize ili tangazo.

**MBUNGE FULANI:** Wana machungu ya Zanzibar.

**NAIBU SPIKA:** Wakiongozwa na Afisa Mtendaji Mkuu wa kwanza mwanamke kuongoza Club kubwa Barani Afrika na huyu ni Ndgr. Barbara Gonzalez. (*Makofi/Vigelegele*)

Ndugu Barbara ameongozana na Msemaji Mkuu wa Mabingwa wa Nchi, Ndg. Haji Manara, 'De La Boss, BUGATTI, nasikia yote ni majina yake. Hapa nimeletewa ujumbe na Mheshimiwa Mwingulu anasema huyo anaitwa *the most valued spokes person* kwa vilabu vyote vya soka ulimwenguni. (*Makofi/Vigelegele*)

Karibuni sana *Simba Sport Club* na viongozi wenu. Sasa mnawenza kukaa tuendelee na matangazo mengine. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wageni 39, hawa ni wageni wangu kutoka Chuo Kikuu cha Teofilo Kisanji Kilichopo Jijini Mbeya wakiongozwa na Mwalimu Mlezi Ndg. Edson Jisandu, Wachungaji wanenye, Rais wa Serikali ya Wanafunzi Ndg. Mussa Mgwassa na Ndg. Halima Magumba ambaye ni Mwenyekiti wa Vyuo Vikuu Mbeya. Karibuni sanasana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge. Tutaanza na wageni wa 3 wa Mheshimiwa Mwanaidi Khamisi ambaye ni Naibu Waziri wa Fedha na Mipango ambao ni Mume wake Ndg. Seif Daudi, kaka yake Ndg. Khamis Ali na mtoto wake Ndg. Ali Mohamed. Karibuni sana. (*Makofi*)

Sasa wengine mkae ili tujue shemeji yetu ni yupi katika hao. Karibu sana shemeji. Waheshimiwa Wabunge mmemuona shemeji yetu. (*Makofi/Kicheko*)

Tunao pia wageni 50 wa Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Dkt. Paulina Nahato ambaye pia ni Mbunge wa Viti Maalum ambao ni viongozi wa Serikali za Vyuo Vikuu mbalimbali Tanzania wakiongozwa na Mwenyekiti wao ndugu Peter Niboye. Karibuni sanasana. Hawa ni viongozi wa Serikali za Vyuo Vikuu, hapo kuna watu wanaitwa Marais, Mawaziri Wakuu na Makamu wa Marais wote wako hapo. Kwa hiyo, karibuni sana ila msiwe na mpango wa kuchukua nafasi za

Wabunge hivi karibuni, ndiyo kwanza wameanza kazi.  
*(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Elias Kwandikwa ambaao ni Katibu wa CCM Wilaya ya Kahama, ndugu Emmanuel Mamange na Mjumbe wa Halmashuri Kuu ya CCM Wilaya ya Kahama, Ndg. Joseph Nyanda. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Nusrat Hanje ambaye ni Mwanamitindo kutoka Jijini Dar Es Salaam Ndg. Ally Hassan Kheri maarufu kama Daxx Cruz. Mheshimiwa Nusrat Hanje yupo upande gani? Hebu simama tuone mitindo ambayo anakushonea. Ahsante sana. Waheshimiwa mnaweza kumuona Mheshimiwa Nusrat hapo akawaelekeza kwa huyu mwanamitindo, tuwatie moyo wanamitindo yetu jamani. *(Makofi)*

Wapo pia wageni 14 wa Mheshimiwa Nashon Bidyanguze ambaao ni Wenyeviti wa Vijiji na wavuvi na viongozi wao kutoka Kigoma Kusini, Mkoa wa Kigoma wakiongozwa na Mwenyekiti wao ndugu Emmanuel Karaenga. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Iddi Kassim ambaye ni Katibu wa Mbunge, Jimbo la Msalala Mkoa wa Shinyanga na huyu ndugu Dotto Ramadhan. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Hawa Mwaifunga ambaao ni familia yake kutoka Mkoani Arusha. Yupo mume wake ndugu Ally Bananga, yupo ndugu Tumaini Mtei na ndugu Gerald Pangani, karibuni sana. Shemeji asimame, karibu sana shemeji yetu. Humu ndani wewe pia ni shemeji yangu kwa sababu umeoa kule nani, yupo salama usiwe na wasiwasi. *(Makofi/Kicheko)*

Wapo pia wageni waliopo kwa ajili ya mafunzo ambaao ni wageni wawili kutoka Jijini Dar es Salaam ndugu Neema Ungani na ndugu Nathanael Makusanya. Wamekuja kujifunza namna Bunge linavyofanya shughuli zake. Sijui wamekaa

upande gani hawa, ama pengine hawakupata nafasi wataingia mchana. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo pia kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, anaomba Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wajumbe wa Kamati hii basi tukishamaliza matangazo hapa, waende Ukumbi wa Msekwa.

Tunalo pia tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mtakatifu Thomas Moore hapa Bungeni, Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge na Wanajumuiya wote kwamba kutakuwa na Ibada ya Misa Takatifu leo saa saba mchana itakayofanyika katika Kanisa la Bunge katika Ukumbi wa Msekwa. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo lingine hapa; Maafisa wa Idara ya Uhamiaji wanatarajiwa kuwepo Bungeni Jengo la Utawala, Ghorofa ya Chini, Ukumbi Na. 9 kuanzia tarehe 3 mpaka tarehe 10 Februari, 2021 kwa ajili ya kutoa huduma ya kupata *passport* zenyé hadhi ya kidiplomasia kwa Waheshimiwa Wabunge. (*Makof*)

Kwa Wabunge ambao wanamiliki *passport* za kawaida za kielektroniki watatakiwa kujaza fomu za maombi ya *passport* na kuambatanisha nakala ya *passport* husika, kitambulisho cha Mbunge na barua ya utambulisho kutoka Ofisi ya Bunge. Huduma hii ya barua inapatikana chumba Na. 301, Ghorofa ya Tatu.

Waheshimiwa Wabunge ambao wanamiliki *passport* ya zamani na ambao hawana kabisa *passport* na wanahitaji kupata *passport* yenyé hadhi ya kidiplomasia watatakiwa kujaza fomu za maombi ya *passport* na kuambatanisha cheti cha kuzaliwa, vyeti au hati za viapo vya kuzaliwa wazazi, kitambulisho cha Taifa au namba ya kitambulisho na nakala ya *passport* ukurasa wenye taarifa binafsi za mwenye *passport*.

Namba nne, fomu za maombi ya *passport* zinatakiwa kujazwa *online* kuitia tovuti ya Idara ya Uhamiaji. Wasaidizi wa Katibu nadhani tangazo hili wawawekee Wabunge kwenye *tablets* zao ili iwe rahisi kufuatilia huko.

Naambiya wameshaweka kwenye ile sehemu ya taarifa za kiofisi, kwa hiyo unaweza kuisoma pale Mheshimiwa Mbunge uone vitu vinavyohitajika ili unapokwenda pale uwe umejandaa na kama kuna maswali yoyote basi pia hayo yataulizwa hiyo sehemu ambayo mmeshatangaziwa hapa sehemu ya kwenda.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na Ratiba yetu; Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**HOTUBA YA MHESHIMIWA RAIS, DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI, ALIYOITOAWAKATI WA UFUNGIZI WA BUNGE LA KUMI NA MBILI, TAREHE 13 NOVEMBA, 2020**

**NAIBU SPIKA:** Katibu subiri kidogo, kuna Mheshimiwa Mbunge amesimama; Mheshimiwa Leah Komanya.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba niongee kwa Kanuni ya 76. Swali langu la leo namba 24, swali la msingi utekelezaji wake uko Jimbo la Meatu, majibu niliyopewa na Serikali ni majibu ya miradi inayotekelzwa Jimbo la Kisasa; naomba mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Hayo yalikuwa ni majibu ya swali la msingi au swali la nyongeza?

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni maswali ya nyongeza yanayohusiana na swali la msingi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nitatoa mwongozo baadaye nikishajiridhisha majibu yaliyotoka na swali lililokuwa limeulizwa, kwa hiyo jioni ya leo nitatoa mwongozo huo.

Waheshimiwa Wabunge tutaendelea; Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

**HOTUBA YA MHESHIMIWA RAIS, DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI, ALIYOITOAWAKATI WA UFUNGIZI WA BUNGE LA KUMI NA MBILI, TAREHE 13 NOVEMBA, 2020**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, nimeshaletewa majina hapa na vyama vyenye Wabunge hapa Bungeni. Tutaanza uchangiaji ambapo tutaanza na Mheshimiwa Godwin Kunambi, atafuatiwa na Mheshimiwa Kasalali Mageni na Mheshimiwa Juliana Shonza ajiandae.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanzo kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, aliyenijalia afya njema hata siku ya leo nikawa hapa. Pia naomba niunge mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma hotuba zote mbili za Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais kuitia Serikali yake ya Awamu ya Tano anapojenga *SGR* maana yake anafanya *capital investment*, anapojenga Bwawa la Kufua Umembe la Nyerere anafanya *capital investment*; anapojenga na kuimarisha bandari zote anafanya *capital investment*; anavyonunua ndege anafanya *capital investment*. Hii tafsiri yake ni nini? Nchi hii miaka ijayo hatuna tena changamoto kwenye suala zima la ukuaji wa uchumi wa nchi yetu kwa sababu Mheshimiwa Rais ameshatuwekea misingi bora ya kukua kwa uchumi wetu na Taifa letu. Kwa hiyo itoshe kusema

katika hili nampongeza sana Mheshimiwa Rais na namwombea Mungu amjalie Maisha mema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi Serikali ya Awamu ya Tano imefanya mambo makubwa sana kwenye sekta mbalimbali. Ushauri wangu ni eneo moja ambalo linahusu mgawanyo wa huduma hizi kitaifa. Tukifanya tathmini ya ujenzi wa barabara, huduma ya afya, elimu, kitaifa utaona kwamba kuna baadhi ya watu lugha hii hawailewi. Nikisema tumejenga vituo vya afya kadhaa kitaifa, mwananchi wa Jimbo la Mlimba ambaye hana kituo cha afya haelewi lugha hii. Ukitisema tumejenga lami kiwango cha urefu kadhaa, maana yake mwananchi wa Mlimba ambaye tangu azaliwe hajaona lami hawezi kuelewa lugha hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa rai yangu na ushauri wangu na kwa sababu jukumu langu kama Mbunge ni kuishauri Serikali na kwa kuwa tunakwenda kufanya maandalizi ya Mpango wa Taifa, nashauri Wizara husika, hasa Wizara ya Fedha na Wizara nyingine za kisekta, umefika wakati sasa tutazame mgawanyo na uwiano wa huduma hizi kitaifa ili lugha hii kila mwananchi Mtanzania aielewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu kama walipa kodi ni Watanzania wote. Sasa inaleta changamoto kidogo mwananchi wa Mlimba anayelipa kodi ikaenda kujenga Dar es Salaam na yeye kimsingi ni mwananchi ambaye ana haki ya kupata huduma zote mbalimbali. Kwa hiyo nishauri tunapokwenda kuandaa na ni rai yangu na naamini kuititia Mawaziri hawa mahiri kabisa, hii hoja wataichukua, kwamba tunakwenda kupanga mpango wa kitaifa sasa, tutazame mgawanyo wa huduma hizi kitaifa ili Watanzania wote wanufaikie na rasilimali za nchi hii, kwa sababu Serikali yetu siyo Serikali ya majimbo, Serikali ya majimbo ndiyo inahamasisha *uneven development*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijikite katika eneo lingine la pato ghafi la Taifa. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Profesa Palamagamba Kabudi, Waziri mwenye dhamana ya Wizara ya Mambo ya Nje; hakika

anafanya kazi kubwa sana. Ana spidi kali sana, lakini jamani wakati sisi wengine *we are lagging behind. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unapozungumzia maendeleo ya Taifa letu lazima Wizara zote tuwe na muunganiko wa pamoja, tuzungumze lugha moja, ili tuhakikishe nchi yetu inakuwa kwa maendeleo kwa kasi zaidi. Kwa mfano, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje anashughulika sana na kuimarisha mahusiano ya nchi yetu na nchi zingine, kupata wawekezaji wa kigeni. Hata hivyo, inapofika Wizara husika kuharakisha mchakato huo ili mwekezaji wa kigeni awekeze kuna masuala ya nenda rudi, njoo kesho, unajua muda pia ni mali; muda ni mali. Leo siyo kesho, siku ya leo haitapatikana tena kesho. Kwa hiyo ni rai yangu kwamba Wizara zingine zina kila sababu sasa ya kuona zinachangia kasi hii ya Wizara ya Mambo ya Nje, hasa kwenye suala zima la uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema nini hapa; ukisoma hotuba ya Mheshimiwa Rais ukurasa wa tisa utaona ameeleza namna ya ukuaji wa pato la Taifa kutoka triliuni 94.3 kwa mwaka 2015 hadi triliuni 139.9 mwaka 2019. Tunampongeza Mheshimiwa Rais, lakini swali langu na hoja yangu ya msingi hapa, tunapopima ukuaji wa uchumi wa nchi turudi tujikite kuona hasa kwenye suala zima la *export* na *import*. Tuone ni kwa kiwango gani tunauza bidhaa zetu nje na kiwango gani tunaagiza bidhaa ndani ya nchi. Kwa mfano, *import* ikiwa kubwa kuliko *export* matokeo yake unakuwa na *unfavorable balance of payment*. Hoja yangu; tuongeze uzalishaji kwenye sekta za kilimo, kwenye sekta za mifugo, kwenye sekta mbalimbali ili tuweze kukuza pato letu la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijikite kwenye Sekta ya Ardhi. Ardhi tuna fursa kubwa; nishauri tu, tuna kila sababu ya kupima nchi hii kwenye hal mashauri zote na jambo lenyewe ni dogo sana. Watanzania wakipata hatimiliki Serikali itaongeza *tax base* na mwananchi wa kawa idha anaweza kukopesheka benki na hii ikasaidia uchumi wa nchi yetu kukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapokwenda kuhitimisha naomba niende moja kwa moja kwenye Sekta ya Barabara. Bado nisisitize Mkoa wa Morogoro ni mkoa wa kimkakati, ni mkoa ambao unalisha Taifa letu, hasa Jimbo la Mlimba. Barabara inayounganisha Mikoa ya Morogoro na Njombe kutoka Ifakara, kilometra 125, ni barabara ya muhimu sana kitaifa. Kwa hiyo rai yangu barabara hii ikijengwa itafungua uchumi wa nchi yetu, lakini pia wananchi wa Mlimba watanufaika na barabara hii. Kwa hiyo kwa kuwa barabara hii imeelezwa kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi Ibara ya 76, ombi langu, Wizara husika ya Ujenzi tunapokwenda kwenye Mpango sasa wa Taifa ni vyema kwenye bajeti yetu tukaanza ujenzi wa barabara hii ili Watanzania hawa wanufaika na barabara hiyo kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalize kwenye Sekta ya Elimu. Jana mzee wangu, Mheshimiwa Dkt. Kimei ameeleza hapa, lakini changamoto kubwa hatuwezi kuboresha elimu, hasa kwenye Sekta ya Ufundu kwa kuanzia kwenye *tertiary education*. Wenzetu Wachina wana kitu kinaitwa *industrial culture* na kupitia All Chinese Youth Federation, ukisema uanzie kwenye *tertiary education* kuimarisha elimu ya ujuzi au ufundu mchundo, hatuwezi; tuanze na *level* ya shule ya msingi. Kuanzia shule ya msingi kuwe na *study* maalum tuwekeze kwa watoto wadogo, anapokua anakuba na *industrial culture*, anavyokua inamsaidia yeye kukuza kipaji chake. Tunapoendelea kuwekeza kwenye sekta ya elimu ya juu, sisemi haina umuhimu, lakini maana yake tunatengeneza Taifa lenye mameneja wengi kuliko wazalishaji. Matokeo yake hawa mameneja hawana wa kuwasimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe tu kwamba tujikite, Wizara ya Elimu mama yangu yupo hapa, naomba atusaidie. Ikiwezekana vyuo vya VETA nayo iwe elimu bure, wasilipe chochote na ujenzi wa vyuo vya VETA, vijengwe kwenye ngazi ya tarafa, hasa Jimbo langu la Mlimba, Tarafa za Mngeta na Mlimba. Naeleza haya ili kuona namna gani tunaweza kuona Taifa letu linakwenda mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hoja moja ya mifugo. Ni kweli tumekuwa nchi ya pili kwa ufugaji, lakini Mheshimiwa Rais ameeleza kwenye hotuba yake kwamba hataki kuona wafugaji, wakulima, wanahangaika. Leo hii unaona mfugaji anayefuga mifugo anaambiwa apunguze mifugo badala ya kumpa njia mbadala kwenye mifugo yake anayofuga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kilimo hali kadhalika; kilimo chetu bado kinahitaji kuongezeka thamani. Kwa mfano pale Mlimba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Kengele ya pili?

**MBUNGE FULANI:** Endelea.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kaka yangu, Mheshimiwa Bashe nisikilize hapa kidogo...

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umeshaisha Mheshimiwa.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Umeisha?

**NAIBU SPIKA:** Ndiyo. Ahsante sana.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kasalali Mageni, atafuatiwa na Mheshimiwa Juliana Shonza, Mheshimiwa Anatropia Theonest Lwehikila ajiandae.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa uzima na afya njema na kuniwezesha kufika hapa nilipofika. Kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuzungumza kwenye Bunge hili, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru

wananchi wa Jimbo la Sumve kwa ushindi mkubwa waliokipatia Chama Cha Mapinduzi katika uchaguzi uliopita. Nikishukuru Chama Cha Mapinduzi kwa kunipitisha na kunisimamia na kuhakikisha nashinda kwa kishindo katika uchaguzi uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa njielekeze katika hoja iliyoko Mezani. Katika Nchi ya Tanzania, baada ya mimi kuangalia hizi hotuba, hotuba ya Mheshimiwa Rais ya kulifungua Bunge na nimepitia hotuba ya mwaka 2015 alioitoa wakati akilifunga Bunge la Kumi na Moja, nimeona kwamba Nchi yetu ya Tanzania inayo bahati kubwa. Tumempata Rais ambaye anayo maono, tumempata Rais ambaye ana nia ya dhati ya kulitumikia Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa la Tanzania ni moja ya mataifa machache yenye bahati ya kuwapata viongozi wa aina ya Dkt. John Pombe Magufuli. Ukiangalia mipango yote na namna ambavyo Serikali ya Awamu ya Tano imejipanga na ilivyokuwa imejipanga katika kipindi cha kwanza na ilivyojipanga katika kipindi cha pili, unayaona matumaini ya Tanzania itakayokuwa ni nchi yenye uchumi mkubwa. Kwa hiyo ninayo sababu ya msingi ya kujivunia kwamba Watanzania tunaye Rais mwema, mwenye maono na ambaye anataka kutuvusha, anataka twende sehemu ambayo wote tumekuwa tukitamani kufika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengi yamefanywa na Serikali yetu, tunaweza tukazungumza hapa lakini muda usitoshe. Nitajaribu kuzungumza machache ambayo yamefanyika na kushauri nini tufanye vizuri zaidi. Serikali ya Awamu ya Tano katika jambo kubwa ambalo imelifanya ambalo dunia nzima inaona na tunajivunia ni kuhakikisha inasimamia vizuri uzembe, ujisadi na ubadhirifu wa mali za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu imeweka utaratibu kuanzia Mheshimiwa Rais akisimama, ukiwaona Mawaziri wake wamesimama, wote wanakemea namna yoyote ya uzembe, namna yoyote ya ubadhirifu na ujisadi

wa mali za umma. Serikali ya Awamu ya Tano imefanya vizuri sana kwenye jambo hilo; majizi, mafisadi wameshughulikiwa vizuri na kila namna ambayo Serikali imeona inaweza kufanya kuhakikisha mali zetu, mapato yetu tunayoyakusanya yanakuwa salama, Serikali ya Awamu ya Tano imefanya vizuri sana na matunda tumeyaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwenye ukusanyaji wa mapato kupitia *TRA* na halmashauri zetu, tumefika kiwango cha kuongeza mapato ya mwezi kutoka bilioni 800 mpaka mwezi uliopita tumeweka rekodi ya kukusanya trillioni mbili, mwezi Desemba; Serikali imefanya vizuri sana kwenye hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini yapo mambo ambayo yanahitaji kuangaliwa kwa undani zaidi. Katika kusimamia ubadhilifu wa mali za umma na matumizi mabaya ya fedha za Serikali, Serikali yetu katika kiwango cha Kitaifa, katika taasisi zilizoko karibu na Serikali kama maeneo ya bandari na maeneo mengine tumefanya vizuri sana. Hata hivyo, kwenye maeneo ya chini, kama kwenye Halmashauri za Wilaya kazi kubwa inahitajika kufanyika. Fedha nyingi za matumizi zinazopelekwa kwenye Halmashauri zetu hazitumiki inavyotakiwa. Bado kuna miradi hewa, kuna usimamizi mbovu wa fedha na fedha nyingi zinapotea. Hata viwango vya majengo na miradi inayosimamiwa na Halmashauri zetu hazijafikia viwango vinavyotakiwa. Kwa hiyo, Wizara husika, ambayo ni TAMISEMI, wanatakiwa kuziangalia Halmashauri kwa jicho la pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanya vizuri sana kwenye sekta ya kilimo kufufua ushirika na mambo mengine, lakini bado kuna mambo ya kufanya kwenye ushirika. Naweza nikakupa mfano, katika Wilaya yetu ya Kwimba kuna shida kubwa sana sasa hivi inaendelea. Kuna mazao ambayo Serikali imeyaweka kusimamiwa na ushirika ambayo kiuhalisia hayakupaswa kusimamiwa na ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna zao la choroko na mazao mengine kama ufuta, yamewekwa kwenye ushirika

Iakini mazao haya siyo kama mazao mengine yaliyoko kwenye ushirika kama pamba. Mazao haya ni ya chakula, ni mazao ambayo uuzaaji na usimamizi wake unapaswa uwe wa kawaida na usitegemee *AMCOS*na ushirika. Katika Wilaya Kwimba, moja ya jambo ambalo linatutesa sasa hivi ni mazao yetu ya choroko kupelekwa kwenye ushirika na tunalazimishwa mazao ambayo ni ya chakula, mazao ambayo sisi muda wote tunayategemea, tukitaka kuuziana ni lazima twende kwenye *AMCOS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niiombe Serikali kwamba umefika wakati wa kuangalia ushirika wetu. Tumeuimarisha ushirika, unafanya vizuri lakini tunauongezea majukumu ambayo ni magumu kuyafanya. Moja ya jukumu ambalo ushirika unapata shida kulifanya ni hili la ununuzi wa choroko, dengu na mazao mengine ambayo ni mazao yetu ya chakula na blashara, kuna wakati tunahitaji kuyatumla kama mazao ya chakula. Mimi siwezi kuhitaji kununua choroko ikabidi niende kununua *AMCOS*, nitanunua kwa mtu mwenye choroko. Naomba sana katika suala hili Serikali kuititia Wizara ya Kilimo ione namna ya kuhakikisha mazao yaliyoongezwa kwenye ushirika yanarudishwa, tunaanza kuyanunua kwa njia zetu za kawaida. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naomba niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamwitwa Mheshimiwa Juliana Shonza, atafuatiwa na Mheshimiwa Anatriopia Theonest Lwehikila na Mheshimiwa Agness Mathew Marwa ajiandae.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nami nakushukuru kwa kunipa nafasi, lakini kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu katika Bunge hili la Kumbi na Mbili, naomba niruhusu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia wote

uzima na afya njema na vile vile kwa kuniwezesha mimi mtoto wake kuweza kurejea katika Bunge hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee, nataka niwashukuru sana wanawake wenzangu wa Mkoa wa Songwe kwa imani yao kubwa walionionyesha, vilevile kwa kura za heshima walizonipatia na hatimaye nimeweza kurudi tena katika Bunge lako Tukufu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, sasa naomba nianze kujadili Hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiitazama Hotuba ya Mheshimiwa Rais, nami nimepata muda wa kuipitia na kulsoma; ni hotuba nzito na imebeba matumaini ya Watanzania. Ni hotuba ambayo ina taswira mbili; taswira ya kwanza, ni hotuba ambayo inaeleza namna gani Serikali ya Awamu ya Tano imeshatekeleza masuala mbalimbali na kutatua changamoto mbalimbali za Watanzania. Pia ni hotuba ambayo imeeleza kwa kina sana namna gani ambavyo Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli amejipanga katika kipindi hiki cha pili kuhakikisha kwamba zile changamoto ambazo zilibaki kwenye awamu ya kwanza, zinaweza kumalizika katika awamu yake hii ya pili. Hotuba hii ni nzito na imebeba matumaini ya Watanzania. Ni hotuba inayota dira na taswira ya Tanzania tunayoitaka na namna gani ambavyo tutafikia Tanzania hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile hotuba ile ni maelekezo rasmi kwa viongozi wote wa Serikali pamoja na taasisi zake, namna gani ambavyo wanapaswa kufanya kazi kwa kuzingatia ile hotuba ambayo Mheshimiwa Rais ameitoa. Yapo masuala mengi sana ambapo ukifuatilia ndani ya ile hotuba yameweza kuelekezwa kwa kina zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nijadili suala moja la afya kwa sababu tunatambua katika nchi yoyote, msingi wowote wa maendeleo ni afya ya watu wake. Hakuna

namna ambavyo Tanzania inaweza ikapata maendeleo kama watu wake hawana afya ambayo ni *stable*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika hotuba hii Mheshimiwa Rais ameeleza namna gani ambavyo miaka mitano ameshuhulikia changamoto za afya kwa Watanzania. Kwa kuwa mimi ni mwanamke, natambua namna gani ambavyo sisi wanawake tulikuwa tunapata changamoto wakati wa kujifungua lakini ndani ya miaka mitano changamoto hizo zimeweza kufanyiwa kazi sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ameemelekeza namna gani ambavyo kwa hii miaka mitano, kwa kupitia Sera ya Afya ambayo inasema kwamba kutakuwa na Kituo cha Afya katika kila Kata, kutakuwa na Zahanati kwenye kila Kijiji, Hospitali za Wilaya kila Wilaya, Hospitali za Mkoa kila mkoa; na hilo tumeliona ilmetekelezeka kwa kishindo kweli kweli. Nimesimama hapa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo amefanya katika miaka mitano. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma hotuba vizuri, ameemeleza namna gani ambavyo ameweza kujenga Zahanati 1,198, siyo kazi ndogo. Pia amejenga Vituo vya Afya vipatavyo 900, siyo kazi ndogo. Vilevile amejenga Hospitali za Wilaya 90, amejenga Hospitali za Mikoa 10 na Hospitali za Kanda tatu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tafsiri yake ni nini? Nachotaka kuongea hususani kwenye afya ya msingi, kwa sababu tunatambua asilimia kubwa ya Watanzania huwa wanaanza kwanza kule chini kwenye afya za msingi, kwa maana ya vituo vyetu vya afya, ukiangalia Vituo vya Afya ambavyo vimejengwa, hoja siyo kwamba vimejengwa vituo 478, hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ni kwamba vituo hivi ambavyo vimejengwa, ukiangalia maeneo mbalimbali ya nchi yetu, vimekuwa na hadhi sawa na Hospitali ya Wilaya. Ukiangalia *facilities* zote zinazopatikana kwenye hivi Vituo vya Afya, havitofautiani sana na Hospitali zetu za Wilaya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naona kwamba ni wakati muafaka sasa kuviiita hivi Vituo vya Afya siyo sawa, tutakuwa hatumtendei haki Mheshimiwa Rais. Hivi vinapaswa viiwe Vituo vya Rufaa vya Kata. Kwa sababu ndivyo ambavyo vinachukua wananchi kutoka kule chini kwenye Zahanati wanakuja kutibiwa kwenye hivi Vituo vya Kata. Nataka nitoe ushauri kwa Serikali, kwa sababu tumeona kwamba vituo hivi vimejengwa vizuri, nasi pale kwetu kwenye Jimbo la Tunduma, tunacho Kituo cha Afya kimoja ambacho kimejengwa vizuri kiasi kwamba ukifika pale unashindwa kuelewa kwamba hiki ni Kituo cha Afya au ni Hospitali ya Wilaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vitu vichache ambavyo nadhani kama vikifanyika kwenye hivi Vituo vyetu vya Afya vitasaidia sana kuvipa hadhi sawa na Hospitali ya Wilaya. Nataka nitoe ushauri kwa Wizara ya Afya na pia ushauri kwa Serikali kwamba ni wakati muafaka sasa waangalie, kama kuna uwezekano kwenye hivi Vituo vyetu vya Afya, yaongezewe majengo mawili, kwa maana ya jengo la jumla la wanawake na jengo la jumla la wanaume. Kwa sababu ni Vituo vya Afya viko pale lakini vinahudumia mama pamoja na mtoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini Serikali ikitenga fedha tukapata hayo majengo mawili pale, moja kwa moja tutakuwa tumevipa hadhi ya kuwa Hospitali ya Wilaya. Nasema hivyo kwa sababu, kwa kufanya hivyo, itasaidia sana kuweza kupunguza msongamano kwenye hospitali zetu zile za Wilaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo pia nataka nilizungumzie ni suala la maji. Kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Rais, ameleeza vizuri sana namna gani ambavyo Serikali imeweka pesa za kutosha zaidi ya shilingi trilioni 2.2 ndani ya miaka mitano, zimepelekwa kwenda kutatua changamoto ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais amesema kwamba imejengwa miradi zaidi ya 1,422 katika nchi nzima ya Tanzania. Hata hivyo, ni ukweli ulio wazi kwamba jitihada

za Serikali ziko wazi na tumeona namna gani ambavyo Wizara ya Maji imekuwa ikifanya kazi usiku na mchana kuhakikisha kwamba inatatua changamoto za maji, lakini bado changamoto ya maji ni kubwa katika Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Rais amesema na hotuba ya Mheshimiwa Rais ni maelekezo; nataka nishauri kwamba pamoja na mambo yote ambayo tutaongea ndani ya hili Bunge, lakini bado changamoto itabaki pale pale kwa sababu Mfuko wa Maji chanzo chake bado hakitoshi. Ukiangalia miradi ya maji ni mingi lakini yote inategemea Mfuko mmoja wa Maji ambao fedha zake ni ndogo. Hili suala ndani ya Bunge lako Tukufu tumekuwa tukilizingumza hata kipindi kilichopita kwamba pamoja na jitihada ambazo zitakazofanyika lakini kuna umuhimu na haja kuhakikisha kwamba Serikali inaongeza fedha kwenye Mfuko wa Maji ili kuweza kutatua tatizo la maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anatropia Theonest atafuatiwa na Mheshimiwa Agness Mathew Marwa na Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe ajiandae.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nitaanza namna hii; nasoma Hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati akilifungua Bunge mwaka 2015 alisema: "Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mchakato wa Katiba, Serikali yangu imepokea kiporo cha mchakato wa Katiba ambao haukuweza kukamilika katika awamu iliyopita. Akaahidi kwamba anatambua na kuthamini kazi kubwa ya kizalendo iliyofanywa na wananchi walioshiriki, hivyo ataiendeleza".

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ni mwaka wa sita, nataka nimwulize au niulize Serikali, mchakato wa Katiba mpya umefikia wapi? Habari ya Katiba mpya siyo yangu, siyo yako, wala siyo ya Rais, ni ya Watanzania wote ambao walishiriki mchakato mzima. Wimbi la kutaka Katiba mpya

lilionekana kabla ya kuanza mchakato mzima ina maana ni hitaji la wananchi ambao wamekuwa wakilitaka muda wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme, *demand* ni kubwa, hauwezi ku-resist. Unaweza ukawa-suppress watu wasiongee lakini ukweli ni kwamba ahadi aliyoahidi Mheshimiwa Rais kwamba amepokea mchakato wa Katiba, ni lazima aitekeleze. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini nimeanza na Katiba? Ni kwa sababu tumeona changamoto kubwa. Mheshimiwa Rais katika hotuba yake ya 2015 na 2020 mara kadhaa ameongelea mchakato wa uchaguzi; ameongelea kushukuru na kuona mchakato ulivyoendelea, lakini mchakato wa Katiba ni mchakato wa wadau. Wadau wa Katiba ni Vyama vya Siasa, ni wananchi, lakini ni Tume. Sasa inafikiaje tunakuja kuona mdau mmoja ndiyo anaona kwamba mchakato ulikuwa ni huru na haki? Ukweli ni kwamba wananchi wanalamika, wanaona mambo yalienda ndivyo sivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais anaipongeza Tume kwamba imeweza kubakiza fedha kati ya bajeti ya shilingi bilioni 331 iliyotengwa, ilitumia shilingi bilioni 232, kwa hiyo, ilibana matumizi. Tume ilibana matumizi kweli, lakini tuliona kwa vitendo Tume ambavyo haikuweza kufanya kazi sana.

*(Hapa kengele ya kwanza ililia)*

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, muda wangu naona umepunguzwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume haikuweza kufanya kazi kubwa kama ambavyo ilitarajiwa. Tume ilikabiliwa na changamoto kubwa; huko chini tuliona maafisa au wasaidizi wa Tume wakigeuka na kuvala nguo ya kijani badala ya kuwa wadau. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeingia katika uchaguzi ambao Tume ya Uchaguzi anapaswa kuwa *referee*. Hakuna mchezo ambao unakuwa huru na haki ambao *player* mmoja kama Simba au Yanga ione kwamba haki imetendeka. Siku zote watu wanamwangalia refa, hawana uhakika kama mchezo utachezwa vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niulize swali lingine, siku moja kabla ya uchaguzi tulishuhudia makaratasi mengi yamepigwa kura na kusambazwa mtaani, *a day before*. Nataka njue majibu yakija, hizi karatasi zilizokuwa zimepigwa kura, zinasambazwa mtaani, mimi binafsi nilizikamata, zilitoka wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine Tume hawakufanya, labda ni Maafisa Wasaidizi waliopewa dhamana. Ndiyo maana tumekuwa tukisema tunahitaji Tume huru ili mshindi atakapokuja ndani hapa kila mmoja aguse kifua aseme, nimeshinda uchaguzi. Siyo tunasema umeshinda uchaguzi, kila mmoja ana wasiwasi kama ameshinda kweli. Hiyo ndiyo aina ya Tume huru tunayoitaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine, tunatamani marekebisho makubwa katika Tume ya Kusimamia Uchaguzi. Wasimamizi Wasaidizi wengi wameonekana sio waaminifu. Hata hivyo, katikati ya mchakato tumeona kubadilishwa kwa Wakurugenzi kinyume na Kanuni za Maadili tulizoisaini, kitu ambacho hakikuwa sahihi. Hiyo ilikuwa ni utangulizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi kwenye changamoto kubwa ambayo hata Mheshimiwa Rais ameisema. Kuna changamoto kubwa ya maji. Katika hotuba ya 2015 Mheshimiwa Rais aliahidi kumtua mwanamke ndoo. Mwaka 2020 nimesoma kwenye hotuba yake anasema: "Katika maeneo mengine Mheshimiwa Rais ameona watu wanalalamika kukosa maji. Bado kuna changamoto kubwa ya maji.

*(Hapa kengele ya pili illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Agness Marwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe na Mheshimiwa Innocent Bilakwate ajiandae.

**MHE. AGNESS M. MARWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa hii nafasi adhibu uliyonipa ya kuchangia hotuba wa Mheshimiwa Rais. Kwanza, namshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kunisababisha kurudi tena Bungeni kwa kipindi cha pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nimshukuru mume wangu mpenzi Anold Wanyambelwa kwa kunisaidia kukaa vizuri na kuishi vizuri na Wajumbe mpaka Wajumbe wakanielewa. Nashukuru sana na Mungu akubariki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wetu kipenzi kwa kazi nzuri aliyoifanya kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita. Kafanya kazi mbili kwa wakati mmoja. Mheshimiwa Rais Mungu ambariki sana kwa sababu kwanza amefanya kazi ya kujenga nchi na uchumi wa Watanzania na sasa tumetoka kwenye uchumi wa chini, tuko kwenye uchumi wa katii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kafanya kazi ya pili ya kukijenga Chama cha Mapinduzi kikaimarika kupitia kazi nyingi na nzuri alizozifanya zilizopelekea tukapata kura za kishindo. Mungu akubariki sana Mheshimiwa Dkt. Magufuli, Rais wetu kipenzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania hatuhitaji Katiba Mpya bila maendeleo. Watanzania tulikuwa tunahitaji

barabara tumeletewa barabara na Mheshimiwa Rais. Tena bahati mbaya jamani, pamoja na Ubunge wangu, yawezekana kidogo nimesababishwa kuwa mshamba na Mheshimiwa Rais nilipofika Dar es Salaam juzi nimepotea. Nimekutana na barabara nzuri sana ambazo zimetengenezwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Magufuli aliona ni vyema akafanya maendeleo kwa Watanzania; kajenga Vituo vya Afya. Badala ya kuchukua shilingi bilioni 400 na kuzipeleka kwa Wabunge wakae kwa ajili ya kujadili Katiba mpya, akaona ni vyema apeleke kwenye maendeleo ya wananchi. Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Mungu akubariki sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tunataka uzazi salama na siyo Katiba na sasa wanawake tunazaa salama. Ndiyo maana katika Bunge moja tu mimi nimezaa watoto wawili kwa kipindi cha miaka mitano na sasa niko salama. Mheshimiwa Dkt. Magufuli, Mungu akubariki sana. (*Makofi/ Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Magufuli ameona zile shilingi bilioni 400 badala ya kutuletea sisi kujilipa wakati wa kujadili Katiba mpya, amesababisha tumepata maji vijijini. Mheshimiwa Dkt. Magufuli sasa wanawake umewatua ndoo kichwani. Mungu akubariki sana kwa kuimarisha ndoa za wanawake, kwa sababu ndoa nyingi zilikuwa zinavunjika kwa kufuata maji mbali, kusubiri maji na kukaa muda mrefu kwenye vituo vya kutafuta maji. Mungu akubariki sana Mheshimiwa Dkt. Magufuli, tunakuombea uendelee na mwendo huo huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kipekee nimshukuru sana Rais wangu kwa kuwajali wajasiriamali wadogo wadogo, wakiwemo mama ntilie, bodaboda, baba lishe, mama lishe kwa kuboresha vitambulisho vyao hadi kupanda hadhi kuonekana kama vitambulisho vya Taifa ili na wao wawze kukopesheka katika mabenki pamoja na kampuni

na mashirika mengine ya kifedha. Niseme Mwenyezi Mungu ambariki sanaMheshimiwa Magufuli adumu miaka 200. Ingekuwa siku zinarudishwa nyuma tungemrudisha nyuma sasa ndiyo akawa unaanza mwaka wa kwanza ili mbele bado miaka kumi inayofuatia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe sana ndugu zangu Mawaziri walioteuliwa na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli. Mheshimiwa Magufuli kafanya kazi nyingi na kubwa sana kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita. Alifanya kazi kama Mbunge, kama Waziri, alifanya kazi kama Diwani na kiongozi wa chini kabisa na ndiyo maana tumesimama imara na ndiyo maana Chama Cha Mapinduzi leo tunajivuna kwa kazi nzuri Mheshimiwa Magufuli alizozifanya ambazo zimetusababishia kutembea kifua mbele na kupata ushindi wa kishindo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa basi kama alivyowaambia Mheshimiwa Rais sasa hivi wanatakiwa mfanye kazi. Hizo nafasi alizowapa ni deni sio kwamba eti amewachagua kwa sababu humu watu wengine hawatoshi, kuna wengine hapa tunawasubiria ili kusudi tu ushindwe kufanya kazi ili na sisi tupate nafasi hizo. Niwaombe sana, wamsaidieni Mheshimiwa Rais kufanya kazi kwa nguvu zote kwa juhudhi, sasa hivi sio muda wa kukaa ofisini. Pia nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuwajali akinamama. Mheshimiwa Rais kwa kweli Mungu ambariki sana, sana na ndiyo maana sasa hivi wanawake wengi tuko Bungeni, tumekuwa asilimia kubwa sana lakini kwa wale waliokwenda majimboni wameshinda, ushindi wa kishindo. Kwa hiyo, tunasema wanawake tunaweza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe sana ndugu zangu, tunapokuwa tuna mihemko ya kisiasa tuiache pemberi sasa tufanye kazi kwa manufaa ya Watanzania wote. Fimbo aliywachapa mwanzoni ndugu zetu wale rafiki zetu majirani msije mkaitamani tena maana kipindi kijacho wakiendelea kutoka nje maana yake hata wao wawili waliopo humu basi wataondoka jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Bilakwate na Mheshimiwa Dkt. Thea Mtara ajiandae.

**MHE. ALLY A. J. MLAGHILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pia naomba nami niungane na wenzangu kumshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia tumepata nafasi ya kuwatumikia Watanzania tukiwa wamoja katika Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru pia Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli. Huyu Rais amejidhihirisha hasa kuanzia kwenye uchaguzi wetu ambapo alihakikisha hata sisi wanyonge tunapata nafasi ya kufika hapa kupitia Chama Cha Mapinduzi ambacho anakiongoza kama Mwenyekiti wa Chama. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nidhahiri maneno mengi yanaweza yakasemwa juu ya huyu Rais, lakini nataka niwaambie Watanzania wote na Bunge hili Tukufu kuna wakati na mimi sitaki tufike huko tutakuja tujilaumu na kusema tunge, haya yasingetokea. Naomba tusifike huko tukafikia kwenye maneno ambayo Wanyakyusa wanasema *pride comes after a fall*. Naomba Watanzania na Bunge hili liflike wakati lilitathmini juu ya huyu Rais na ikiwezekana Wabunge tuungane, tufikie wakati tutoe tamko. Sio kwamba Rwanda ni wajinga walipofikia pale, sio kwamba Wachina ni wajinga walipofikia pale. Niwaombe Bunge hili, najua maneno haya wengi hawayapendi, lakini naomba tusifikie wakati wa kujilaumu tukasema tungelifanya hivi kwa huyu Rais basi Tanzania ingefika hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, llani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015 imemfanya Rais wetuna Chama Cha Mapinduzi kufikisha asilimia 84.4. llani bora ya sasahivi ya Chama Cha Mapinduzi, naomba sasa ifikishe Rais huyu kuzidi miaka mitano ijayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie hotuba hii na kuunga mkono kwenye maeneo machache. Naomba nifike kwenye eneo la kilimo ambapo zao la *cocoa* ambapo ukiitaja *cocoa* unaisema Kyela moja kwa moja, ni zao ambalo limetufikisha hatua ya kujiona na sisi tuna dhahabu. Hata hivyo, zao hili kwa sasahivi halimnufaishi mkulima kupitia kitu kinachoitwa stakabadhi ghalani. Wataalam wetu hawajatufikirisha vizuri, wamelichukua desa lao kama liliyvo wamelihamisha. Wamedesa mfumo unaotumika kwenye mazao ya msimu wameleta kwenye mazao ya muda wote. *Cocoa* sio zao la msimu ni zao ambalo lipo muda wote wa mwaka na zao hili sio zao ambalo linalimwa kwenye mashamba makubwa, ni vivuli kwenye nyumba za watu. Watu wanaokota kilo moja moja, kilo tano tano. Sasa huyu mtu ukidesa mfumo wa korosho au kahawa ukauleta kwenye mfumo wa zao kama hili, unafeli nahapo ndiyo unapofeli mfumo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye zao la *cocoa* sasahivi mtu anashindwa kusubiri siku nane za kuvundika *cocoa* ndipo akauze anaamua kuuza kwa Sh.2,500, wakati yule anayenunua mtu wa kati anapata zaidi ya Sh.5,000. Kwa kweli hili suala naomba kusema halijatusaidia wana Kyela na ni lazima tukae chini wataalam waishauri Serikali vizuri tuweze kutatua hili tatizo ili mnufaika awe ni yule aliyelengwa na ushirika ili suala la kumfanya apate faida yeye sio mtu wa kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kyela pia tunalima mpunga. Ni bahati mbaya sana, sasahivi kuna maneno yanaenea kwamba mchele wa Kyela umepungua ladha! Sio kweli. Ladha ya mchele wa Kyela ni ile ile ilakuna watu wanauza mchele wao kwa kutumia jina hilo. Naomba Wabunge na Watanzania wote waelewe mchele wa Kyela ni ule ule. Tunachoomba kwa Serikali sasa ni kwamba tuna mito minne mikubwa, sasa tunahitaji skimu za umwagiliaji ili tuwaoneshe mpunga wetu ulivyo bora ukiwa mwingi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maji ni tatizo kubwa sana, lakini naomba hebu tujikite pia kwenye sera zetu. Sera

ya Maji inasema mtu asitembee zaidi ya mita 400, lakini kwenye kituo kimojawachote watu 250. Maana yake ninini? Maana yake nikwamba kwenye saa 12 ina maana wanatakiwa kuchoka watu 20 kila saa moja na kila dakika tatu achote mtu mmoja na hapo ni kwamba maji yachuruzike muda wote. Sasa naomba hili suala liangaliwe na wataalam ili kuweza kuweka vizuri na takwimu zetu zikae vizuri tofauti na zilivyo kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara zetu sasahivi zinatia aibu. Mheshimiwa Rais anajitahidi kujenga barabara nzuri, lakini ndani ya muda mchache zinaharibika na tatizo lingine linaloharibu barabara ni kwamba viwango vyetu bado hatujaviweka vizuri, lakini bado tuna matatizo ya matuta barabarani. Hebu tujiulize, je mpaka sasa tunaingia kwenye uchumi wa katiba tunahitaji matuta kudhibiti spidi? Matuta haya yanaharibu barabara lakini kwa uchumi wetu sio mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Rais kwa kusema Wabunge tujitathmini, sisi ndiyo walinzi wa Rais wetu. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Innocent Bilakwate atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara na Mheshimiwa Anna Lupembe ajiandae. Mheshimiwa Bilakwate hayupo, Mheshimiwa Thea Ntara.

**MHE. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii ya kuingia kwenye Bunge hili kwa mara ya kwanza. Pia nichukue nafasi hii kuwashukuru wanawake wa Mkoa wa Ruvuma na wanawake wa Taifa hili wale wajumbe wa Baraza Kuu amba walinfanya mimi nikapita na nimeweza kuingia Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja katika kuchangiaspeech ya Rais. Najikita zaidi kwenye mikopo ya elimu ya juu. Bajeti ya mikopo bado ni ndogo

sanana wanafunzi wengi sana wanakosa mkopo. Sasa ili tuweze kusaidia kuondoa manung'uniko kwenye suala la mikopo ningeshauri Serikali itoe fedha kwa wanafunzi wote angalau wote wapate *flat rate* kama ni asilimia 80 mpaka 85 itasaidia, lakini kama wengine wanapata asilimia 100 halafu wengine hawapati kabisa basi hili suala la mikopo litaendelea kuwa na manung'uniko mengi sana. Kwa hiyo cha kufanyika sasa hivi ni kuhakikisha kwamba watoto wote wenyе vigezo vyа kuingia Chuo Kikuu wapewe mikopo kwa *rate* ambayo itafanana wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine sasa hivi tuna wanafunzi wengi sana katika vyuo vikuu. Unaingia darasa lile kufundisha lina wanafunzi 1,000, Walimu ni wachache, wafanyakazi ni wachache. Miaka miwili iliyopita kila wakati wanasema Walimu wataongezeka, Wahadhiri wataongezeka, watendaji ndani ya vyuo vikuu wataongezeka lakini bado hawaongezeki. Hilo linasababisha hata ufundishaji ndani ya vyuo vyetu unakuwa sio ufundishaji wa kufundisha kama tunavyotegemea. Kwa hiyo napendekeza kwamba lazima idadi ya Wahadhiri iongezeke, vyuo vikuu waruhusiwe au wapewe dhamana ya kuajiri Wahadhiri wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine katika kuboresha maarifa na ujuzi. Sasa hivi tunalalamika kwamba wanafunzi wetu wakitoka vyuo vikuu hawana *life skills, vocational skills* lakini hii yote kwa sababu bado ile *competence approach* hata Wahadhiri bado hawaijui. Ningeshauri Serikali kwamba wajitahidi sana kuongeza bajeti kwa *TAMi TA*waweze kutoa *seminar* au waweze kutoa hayo masomo kwa Wahadhiri pia na wao waweze kufundisha vizuri inavyotakiwa kama vile ambavyo wanatoa semina au ujuzi wa *Tutors*. Kwa hiyo pia hata Wahadhiri wanatakiwa wapewe hizo semina ili wafundishe katika ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali. Kulikuwa na jambo limetokea katika vyuo vikuu kuhusu rushwa ya ngono. Mimi niwapongeze sana TAKUKURU kwa lile jambo walilolifanya, lakini niwaombe kama walifanya utafiti na

kugundua kwamba kuna baadhi ya wahadhiri sio waaminifu wanatumia nafasi zao kupokea rushwa za ngono kutoka kwa wanafunzi wetu, basi tuwaombe hao wakuu wa vyuo pamoja na Wizara inayohusika wawachukulie hatua mara moja. Suala la ngono ni ngumu sana kupata ushahidi, lakini wengi wakikutaja wewe, watu 20 wanakutaja watu 50 wanakutaja, kwanini wasimtaje mtu mwingine? Viongozi wachukue hatua mara moja.Niwapongeze sana wale wakuu wa vyuo ambaao wamechukua hatua ya kuwasimamisha kazi baadhi ya Wahadhiri wanaowatumia watoto wetu kubageuza kuva vyombo nya kustarehe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, niwaombe TAKUKURU, baada ya kufanya tafiti zao, ile *feedback* waipeleke kwenye vyuo. Isibaki kwao. Ukiashafanya tafiti lazima wewe ile ripoti uwape vyuo vikuu waone, wasome, kwamba ninyi mnafanya mambo hayana haya machafu. Sio ngono tu, watoto wetu wa kiume pia wanaombwa pesa. Kwa hiyo Serikali iingilie hilo na wasaidiane na TAKUKURU kuona kwamba sasa tunapata elimu bora na sio elimu ambayo imepitia huko kwenye rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nikushukuru sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anna Lupembe, hayupo, Mheshimiwa Felista Njau, atafuatiwa na Mheshimiwa Zaitun Swai na Mheshimiwa Khatib Said Haji ajiandae.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye amenisaidia kufika mahali hapa hii leo. Naishukuru pia familia yangu ambayo kimsingi imekuwa nyuma yangu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda moja kwa moja kwenye hotuba ya Rais ambayo imeeleza kwenye ile *page* ya 21 namna gani wanawake na vijanawanakwenda kupata mikopo ya asilimia 10. Nimesema kuhusiana na hili linatakiwa

jicho la tatu kwa sababu wanawake wengi ndiyo wanaoonekana kwenda mbele kwenye hii mikopo na wanawake hawa wamepata changamoto lukuki. Changamoto hizi hazitatuliwi kwa muda mrefu, kwa sababu wanawake hawa wanaenda kupewa vigezo ambavyo haviko kwenye utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza wanadaiwa kadi za Chama Cha Mapinduzi, kama hauna kadi ya Chama Cha Mapinduzi hupati mikopo. Lakini wanawake hawa hawa baada ya kupata mikopo hawana mtu wa kuwafundisha ni namna gani watakwendwa kufanya biashara kwa kiwango kidogo wanachopewa ili kuleta tija kwenye jamii. Kikubwa zaidi hawa wanawake wanaopata mikopo au wengine wanaokosa wanakimbilia kwenye *microfinance*...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fellister Njau, kuna Kanuni inavunjwa. Mheshimiws Jenista Mhagama Kanuni inayovunjwa.

#### **KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye utaratibu. Kanuni ya 71 mambo yanayokatazwa Bungeni lakini 71(1) ambacho Mbunge haruhusiwi kusema taarifa ambazo hazina ukweli, lakini kiambatane na Kifungu cha 70(4) ambacho kinamtaka kuthibitisha ni kwa kiasi gani jambo linalosemwa kwamba si sahihi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niliambie Bunge Iako Tukufu, kwa mujibu wa miongozo tuliojiwekea inayosimamia utoaji wa mikopo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika halmashauri zetu, kigezo cha uanachama wa mwombaji wa mikopo hakipo na hakijawahi kutumika. Halmashauri zote zimekuwa zikitoa mikopo hiyo kwa uwiano ulio sahihi kabisa. Kinachozingatiwa ni taratibu zile za kimiongozo ambazo zinatakiwa kila mwombaji mkopo aweze kuzifuata. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Bunge hili lisitumike kuzungumza mambo ambayo hayana uasili na uhalisia. Mara nyingi tumekuwa tukimsikia Mheshimiwa Rais akisema maendeleo ya taifa hili hayatazingatia chama, dini, ukabila wala jambo lolote ni maendeleo huru kwa Watanzania wote kwa mambo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.  
*(Makof)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge alikuwa anachangia Mheshimiwa Felister Njau, ameелеza maelezo kuhusu mikopo inayotolewa na vigezo vinavyozingatiwa. Akasimama Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa mujibu wa Kanuni ya 71 na 70, ametoa maelezo ambayo sote tumeyasikia, sitayarejea lakini hoja ya msingi iliyotolewa hapo ni kwamba, Mheshimiwa Fellster Njau wakati anachangia amezungumza taarifa kuhusu mikopo ambazo hazina ukweli kwa mujibu wa Mheshimiwa Jenista. Kanuni yetu ya 70 inatuongoza namna ya kwenda na jambo ambalo limezungumzwa hapa, lakini Mbunge ataamua sasa kusimama kama alivyofanya Mheshimiwa Jenista kuonesha kwamba jambo hilo linalosemwa halina ukweli na ametoa ufanuzi kwa nini anasema halina ukweli.

Mheshimiwa Felista Njau, ili twende vizuri na kwa sababu sisi wengi hapa ndani ni wageni tutaelekezana tu vizuri hizi Kanuni taratibu, lakini Kanuni ya 70, Mheshimiwa Jenista ametumia fasili ya (4) na (7) inakupa fursa ya aidha kufuta kauli yako kama hilo jambo lililosemwa huna uthibitisho nalo, ama kama hutafuta hiyo kauli hapo nitatoa mimi maelekezo ya nini kifuate baada ya hapo.

Kwa hiyo, nakupa fursa kama huna uthibitisho ufute hiyo kauli, kama utakuwa hufuti kauli nitasimama tena kutoa maelekezo. Nakupa fursa ya kufuta kauli. *(Makof)*

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Nailbu Spika, ahsante. Sifuti kauli kwa sababu nina uthibitisho na kimsingi nilikuwa nashauri kwa sababu watu wengi wanaweza

wakatumia hiyo lakini ngazi za juu hawajui. Kwa hiyo, natoa ushauri mamlaka husika ifuatilie, hilo tu. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Sawa, sasa ukae Mheshimiwa Njau. Waheshimiwa Wabunge, naenda taratibu kwa sababu sisi wengi humu ndani ni wageni.

Mheshimiwa Felista Njau matakwa ya Kanuni ya 70, ukikataa kufuta kauli maana yake mimi naweza kukuelekeza uniletee ushahidi. Ushahidi utakaoniletea si wa maneno wa kuniambia kuna watu waliambiwa, hapana; utatakiwa ulete ushahidi wa kulithibitishia Bunge hili kwamba hicho ni kigezo cha mikopo mahali fulani na mahali fulani. Kwa hiyo, tuelewane vizuri Waheshimiwa Wabunge. (*Makof*)

Kwa hivyo, unavyopewa hii fursa ni fursa ya muhimu sana lakini kama unao uhakika Bunge hili kwa sasa hivi haliwezi kukulazimisha kufuta kauli kwa sababu, wewe umesema unao uthibitisho. Sasa kwa sababu ya ugeni nakupa tena fursa ya pili, kama unao uthibitisho nitatoa maelekezo. Karibu, sekunde 30, unao uthibitisho?

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kuondoa mlolongo nafuta lakini naomba... (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Haya, kaa niiweke vizuri, kaa niiweke vizuri, eeh.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni zetu namna zinavyotutaka kuenenda niwashauri sana sote tuzipitie, Wabunge wageni lakini sisi sote kwa sababu hili ni Bunge jipy. Kanuni hizi ni toleo jipy kwa hiyo, ziko Kanuni ambazo zimebadilika hapa na pale niwasihii sana tukazipitie.

Masharti yaliyoko humu huwa yanafuatiliwa nukta kwa koma, kwa hivyo, ukifuta kauli unafuta bila masharti. Hakuna neno lakini ama nafanya hivi, ahhh-aa, isipokuwa yale uliyokuwa unayasema maelezo yako ya pili, sasa hii natoa Mwongozo; ungeweza kusema naishauri Serikali wakati wa kutoa mikopo wajaribu kuangalia hiki na hiki, lakini

ukionesha kwamba kuna shida mahali ni lazima hiyo shida iletewe uthibitisho.

Waheshimiwa Wabunge, kwa muktadha huu na ili tuweze kwenda mbele, Mheshimiwa Felister Njau amefuta kauli yake. Kwa muktadha huo Mwongozo wa Kiti kuhusu huo utaratibu aliokuwa ameomba Mheshimiwa Jenista Mhagama ni kwamba taarifa hiyo haitakuwepo kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Njau endelea na mchango wako.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nakwenda kwenye kipengele kingine *page number* 72 ambapo kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Rais kumeeleza kulinda demokrasia, uhuru, haki za wananchi na vyombo vya Habari. Mpaka sasa navyoongea mimi nilikuwa meneja kampeni wa Jimbo la Kawe, Mheshimiwa Halima James mwana wa Mdee, haki, demokrasia, usawa havikulindwa na havikulindwa toka uchaguzi mdogo wa mwaka 2014 uliofutwa, 2019 uliofutwa, lakini 2020 kulikuwa kuna mambo ya ajabu. Mimi ni kati ya watu niliyekamata kura *fake* mabegi matano kwenye vyombo vingi, lakini nikasema kwa sababu tunakuja kwenye Bunge hili ni lazima tuseme ukweli, demokrasia tunayoiimba tuifuate kwa vitendo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mtu anajua kwenye Bunge hili amekuja vipi, ameshinda vipi, kwa njia zipi, lakini demokrasia ikaseme na miyo yetu. Haki ya vyombo vya habari, kuna kipindi sisi tulikuwa tukisimama kwenye majukwaa mwandishi akaonekana amepiga picha, humuoni hata siku tatu, nne, ukimpigia simu anakimbia anasema nina kigugumizi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme kama ni haki tunaitangaza, kama ni demokrasia tunaisema, tuiishi kwa vitendo kwa sababu hapa kila mtu ana imani yake. Kila mtu ana imani kwenye Bunge hili kwa hiyo, tuiishi kwa vitendo tusiimbe kwenye makaratasi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa minajili hiyo kuna watu lukuki, kuna wananchi waliokamatwa kipindi cha uchaguzi...

### **KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gwajima, Kanuni inayovunjwa?

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kwa Kanuni ya 71(1)(a). Inasema: "Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli." (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbunge aliyekuwa anazungumza, bahati nzuri mimi ndiye Mbunge halali wa Jimbo la Kawe niliyeshinda kwa kura 194,000 dhidi ya mpinzani wangu aliyepata 30,000 peke yake. Naomba alithibitishie Bunge lako kwamba alikamata kura maboksi 50 kama alivyosema. (*Makofi/kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, bahati nzuri hizi kanuni tutazifahamu tu, Bunge hili ni la miaka mitano, Mwenyezi Mungu atujalie uhai na uzima. Kanuni ya 71 inampa fursa Mbunge kusimama ukisoma fasili nydingine zinazofuata baada ya hapo na kusema kuhusu utaratibu, kwa maana ya fasili ya (2) inampa fursa Mbunge kusimama kusema Kuhusu Utaratibu ili kueleza mambo haya yasiyoruhusiwa Bungeni kwa lile ambalo linakuwa linazungumzwa.

Mheshimiwa Gwajima, Mbunge wa Kawe, amesimama kueleza kwamba taarifa zilizokuwa zinatolewa na Mheshimiwa Felista Njau za kuhusu vitu viliviyokamatwa huko Jimboni Kawe kipindi cha uchaguzi ama siku ya uchaguzi hazina ukweli. Sasa mimi siwezi kufahamu ukweli, anayeufahamu ni Mheshimiwa Felister Njau. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kabla hamjapiga makofi, hili jengo letu hili kuna muda kuna maneno fulani hivi yanaweza kusemwa pamoja na mambo mengine kwamba hili jumba ni jumba la kisasa, lakini hili ni jumba ambalo ndiyo maana wanasema Mheshimiwa Spika Bunge lako Tukufu. Haiyumkiniki kwamba mtu anayesimama kuchangia humu ndani atazungumza mambo ambayo yanazungumzwa bila ushahidi, bila uhakika kwa sababu kila mmoja wetu anaitwa Mheshimiwa kwa maana ya ni kiongozi anaweza kusimamia kile anachokisema, anaweza kuthibitisha kile anachokisema.

Mheshimiwa Felister Njau huu ni utaratibu wa pili kwamba Kanuni inavunjwa. Humu ndani huwa ni kawaida watu wanaweza kusimama hatu mara nyingi, lakini tazama michango yako isikupeleke mahali ambapo kuna Kanuni humu ndani zinakupeleka nje ya hili Bunge. Isitokee kwamba kila unachokisema tutafika mahali pa kwenda hapo, siyo kwa maana ya utoke nje, aah-aa, kwa maana ya uende huko Kamati ikajiridhishe, ulete huo ushahidi na mambo kama hayo. (*Makofi*)

Kwa hivyo, kwa muktadha wa Kanuni hizi kwa sababu, sasa husemi ukweli maana yake unarudi tena kwenye 70. Kama unao uthibitisho utasema hivyo, mimi nitaagiza utoe huo uthibitisho. Kama huna uthibitisho futa kauli yako kwa mujibu wa Kanuni ya 70 kama nilivyokusomea Fasili ya (7).

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Uthibitisho ninao na nikiambiwa nilete nitaleta uthibitisho. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Kanuni hii ya 70 inakataza Mbunge kusema uwongo...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Tusikilizane Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane. Kanuni ya 70 inakataza kusema uongo Bungeni na fasili ya (4) ya (5) na ya (6) ukizisoma zote kwa pamoja

utapata picha kwamba Kiti kitaagiza Mbunge ambaye amekataa kufuta kauli kuleta ushahidi kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge na siyo kumridhisha mtu mmoja.

Kwa muktadha huo fasili ya (6) inanitaka mimi nitoe muda wa kufanya hivyo. Mimi sitataka nimwambie alete ushahidi hapa kwa sababu naweza kumwambia alete sasa hivi ama alete baadae, kwa sababu alikamata maboksi na mabegi hataweza kuwa nayo humu ndani maana yatakuwa hayakupita pale nje kuingia humu ndani. Kwa muktadha huo, hayo mabegi, hayo masanduku yaliyokamatwa naiagiza Kamati yetu ya Maadili, itamsikiliza ye ye halafu mimi nitaletewa huo ushahidi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Njau utapeleka ushahidi wako kwenye hiyo Kamati yetu. Muda ninaoutoa kwa sababu leo ni siku ya Jumatano ndiyo kwanza tumeanza Bunge jana, kufikia Jumatano ijayo huo ushahidi uwe umeshauleta na Kamati yetu ya Maadili ikae wakati huo na kabla Bunge hili halijaisha tutatoa maamuzi kuhusu jambo hilo. (*Makofi*)

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba dakika zangu zilindwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo niombe mamlaka ambayo inaweza kushughulika, kuna vijana wengi katika kanda mbalimbali na mikoa wako ndani kwa kesi za kisiasa za uchaguzi na zinapigwa tarehe, ushahidi unakosekana. Katika kanda mbalimbali, Kanda ya Kusini 34, Kanda ya Nyasa 36, Viktoria 16, Serengeti 34, Pwani nane, wale vijana ni wa CCM na CHADEMA. Kwa hiyo, naomba mamlaka husika iwaondoe vijana hawa ndani kwa sababu shughuli au mtanange umekwisha. (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Njau, hao washauri wako wa hapo karibu wanatakiwa wakushauri mambo mengi sana ikiwa ni pamoa na mambo yaliyoko mahakamani. Mambo yaliyoko mahakamani hayatolewi maamuzi hapa ndani.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, *sorry*, wako mahabusu.

**NAIBU SPIKA:** Mambo yaliyoko mahakamani hayatolewi maamuzi hapa ndani. Mheshimiwa Esther Matiko na Ester Bulaya msimpoteze Mheshimiwa Felister Njau.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Njau malizia mchango wako.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** *No, please*, sasa mimi umeniingizaje hapo, *I did not say anything*.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Sijawasha *microphone* hapa, kichwa yake yeye mwenyewe iko vizuri.

**MHE. FELISTER D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko na Ester Bulaya, muachenii mchangiaji amalize mchango wake. Muachenii mchangiaji amalize mchango wake, Mheshimiwa Felista Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

## TAARIFA

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa, niko huku.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kunti.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Naomba tu nimpe Taarifa mchangiaji Mheshimiwa Njau kwamba watu anaowazungumzia ni

pamoja na wakazi wa Wilaya ya Mpwapwa ambao wako 18 walikamatwa, kesi haijaenda mahakamani...

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane vizuri. Bunge hili siyo kazi yake kuingilia michakato ya taasisi zilizoko huko nje, labda kama hapa mbele kuna hoja hiyo, tuelewane vizuri na ninyi mnazifahamu kanuni, tuelewane vizuri. Mheshimiwa Njau malizia mchango wako. (*Makofi*)

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nishukuru lakini niombe, wako Mawaziri wenye mamlaka hayo wasimame kidete kwa ajili ya kutetea haki za raia na tusiende kwa sababu ya itikadi au chochote. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khatib Said Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Zaitun Swai. Mheshimiwa Zainab katimba ajiandae.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kusimama hapa. Kwanza, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia uzima wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile leo ni mara ya mwanzo kusimama katika Bunge lako hili, napenda nitoe shukrani kidogo kwa wanaostahiki. Kwanza, nawashukuru kwa dhati kabisa wananchi wa Jimbo la Konde kwa kunipa kura za kunirudisha tena hapa Bungeni. Naamini kabisa maamuzi yao yalikuwa ni sahihi na nataka kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu anijalie niwawakilishe kwa usahihi kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nataka nitoe shukrani za dhati kwa chama changu cha ACT Wazalendo kwa kuniamini kunipa fursa na wanajimbo wakanichagua kuja hapa. Pia napenda kwa dhati kabisa kutoka ndani ya moyo wangu nimshukuru kiongozi wa chama chetu Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mwenyekiti wa Chama, Maalim Seif Shariff Hamad, niwaombee kwa Mungu awape afya njema wazidi

kusimamia mpaka pale haki itakaposimama ndani ya nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia, nataka niongee kwanza katika hotuba ya Mheshimiwa Rais aligusia habari ya viwanda, nataka hapa kidogo niongelee suala hili, dakika ni chache lakini tutagusa maeneo kidogo kidogo hivyo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuita wawekezaji tuanzishe viwanda ndani ya nchi ni maono yenye lengo la kuleta manufaa kwa nchi yetu na watu wetu, naunga mkono juhudzi zote zinazofanywa na Serikali katika kuhimiza wawekezaji kuingia ndani ya nchi yetu. Niseme kwamba tunapoomba wawekezaji waingie ndani ya nchi yetu tunawajibu wawekezaji kuwalinda ili wafanye kazi zao ili kuleta tija tunayodhamiria kuipata. Umezuka mtindo ambao naomba Mheshimiwa Waziri wa Viwanda awe makini sana, tunakuwa mahodari wa kutaka wawekezaji waingie, wanakuja na viwanda vinaanzishwa, lakini matokeo yake baada ya muda inatokea migogoro au sintofahamu inayofanya viwanda hivyo vishindwe kufanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa karibuni mtakumbuka palikuwa na mgogoro mzito wa Kiwanda cha Dangote, uwekezaji ule mkubwa lakini ulikuwa utendaji wake ni wa kusuasua. Kwasababu zozote zile nashukuru nimepata taarifa kwamba sasa kiwanda kile tayari kinafanyakazi, hilo ni jambo zuri na napongeza jitihada zote zilizofanyika kupelekea kiwanda kile kurudi katika uzalishaji. Hongera sana kwa wote waliohusika kufanikisha hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo pale Tanga tuna kiwanda kikubwa sana cha kuzalisha ngano, Pembe *Mills*, hiki kiwanda sasa kina takriban mwaka wa nne kimesimama na ni uwekezaji mkubwa, ni mionganoni mwa viwanda vichache vikubwa vyaa una ambavyo viro katika nchi yetu. Nataka Mheshimiwa Waziri afuatilie na jitihada zilizofanyika kufanya Dangote irudi kufanyakazi na watu wa Tanga wanahitaji Kiwanda cha Pembe *Mills* kirejee katika

uzalishaji ili wananchi wa Tanga wafaidike na ajira na mapato yao. Katika suala la viwanda naomba niishie hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi katika suala la katiba mpya, nilibahatika kuwa Mjumbe wa Bunge la Katiba na wewe ulikuwa shahidi, Mheshimiwa Spika alikuwa ni Mwenyekiti wangu wa Kamati. Maamuzi yale yaliyofanyika ninahakika yalipata Baraka ya Chama Cha Mapinduzi kwa 100% kwasababu Chama Cha Mapinduzi na ndio chama tawala na ndio chama chenye Serikali, kama jambo lile walikuwa hawakulikubali lisinegefikia kuingia kwenye Bunge la Katiba, ninahakika walikubali na walikuwa na dhati ya nafsi zao kulifanya jambo lile lifanikiwe. Kubwa zaidi tulikwenda kwa wananchi Tume ya Mabadiliko ya Katiba ilikwenda kwa wananchi ikazunguka nchi nzima kuchukua maoni ya Watanzania na Watanzania walijibu walichokitaka. Bahati nzuri Bunge la Katiba liliifanyakazi Watanzania waliyoitaka na bahati nzuri zaidi ni kwamba wako viongozi ambao wamepewa nishani kwa kufanikisha kazi ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunachokizungumza hapa si jambo geni wala jipya, ni jambo ambalo liko katika ahadi kwa wananchi wa Tanzania wakupatiwa katiba mpya. Kwahivyo tunapolizungumza hili katika hotuba ya Mheshimiwa Rais lipo, 2015 na kuna ahadi yake mwenyewe, kwahivyo tunapokumbushana ni kwa lengo jema la kujenga. Naomba Serikali iletu majibu Watanzania...

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khatib kuna taarifa

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Nashukuru naomba nimpe taarifa muongeaji kwamba suala la katiba mpya lipo katika hotuba ya Rais ukurasa wanane, akiahidi kwamba atahakikisha analitimiza.

**NAIBU SPIKA:** Ngoja ngoja tuelewane vizurikwasababu wewe tulikuwepo wote hapa, ye ye kashasema ipo kwenye

hotuba ya Rais, wewe unampa taarifa kwamba ipo kwenye hotuba ya Rais, ni taarifa gani unayompa maana kashasema...

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Nasaidia kumweleza.

**NAIBU SPIKA:** Hebu soma kanuni yako inazungumza nini kuhusutaarifa, ni taarifa gani unayoweza kutoa, siyo taarifa ambayo yeye anaijua hapana, taarifa ambayo yeye hajaisema, sasa yeye kashasema, ni taarifa gani unampa.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** kwenye *floor*kuna mtu alitaka kujua ipo wapi ina maana kuna mtu wa...

**NAIBU SPIKA:** Nani aliyekuuliza Mheshimiwa siyo wewe unayechangia? Yeye kashasema ipo, sasa wewe unasema taarifa, lazima umpe kitu ambacho yeye pengine amepitiwa ama hakifahamu. Mheshimiwa Khatib endelea na mchango wako.

**MBUNGE FULANI:** Hicho ni kiherehere.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme kwamba imani ya Watanzania ni kwamba itakapopatikana Katiba mpya pia katika katiba mpya moja ya tunda muhimu la katiba mpya itakuwa ni Tume huru ya Uchaguzi. Ndani ya nchi hii tunaamini, ni imani yetu sisi na imani yetu hailazimishi imani yangu mimi kuikubali mtu mwingine, tunaimani na tunaamini hivyo kama katika nchi yetu ya Tanzania hatuna Tume huru ya Uchaguzi, *whatever* wengine tumerudi, lakini kurudi kwetu kama mnavyotuona hili benchi loote lilikuwa letu enzi zile za CUFna hili loote lilikuwa la CHADEMA, Tume ya Uchaguzi imetufanya tumekuwa maskini, tumekuwa mayatima, tumerudi kajipande hiki tu, Wabunge wa Majimbo tuko watano wanaume tuliobakia wote tuna wanawake humu jamani haki hii? (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khatibu kuna taarifanyingine kutoka kwa Mheshimiwa David Ernest Silinde.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Khatib wakati wa mchakato wa Katiba mpya na mimi wakati huo nilikuwa upande wa pili. Kwahiyio mimi nilikuwa sehemu ya ule mchakato na bahati nzuri sana tangu wakati tume inaundwa ilikuwa bado ni Serikali ya Chama Cha Mapinduzi ndiyo ilitengeneza ile tume na tume ikakusanya maoni. Serikali ya Chama Cha Mapinduzi wakati huo niko upinzani, ilipounda tume ikaleta mchakato ule wa maoni yote ukaletwa ndani ya Bunge na mimi niko ndani ya Bunge, mchakato ukaanza tukaushiriki, sasa baada ya kuona kwamba ile ngoma ngumu, wakati huo na mimi niko upande wa pili, sisi tukaingia mitini umenielewa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwahiyio wakati ule wa mchakato siyo CCM waliokwamisha, wakati ule ni sisi tulikimbia ndani ya Bunge na uzuri ni nini? Jambo hili Tanzania nzima inajua siyo kwamba ilikuwa la kificho, Bunge ilikuwa liko wazi, ilikuwa linarushwa, sisi ndiyo tukagoma, tukakaa kule ndani kwa mashinikizo na shinikizo kubwa ilikuwa kwamba tunataka Serikali tatu, ndiyo sababu iliyotuondoa ndani ya Bunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwahiyio nilikuwa nataka nimpe tu taarifa kwamba malengo ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi yataendelea kubaki kuwa sahihi, isipokuwa mwisho wa siku sisi na ilitakiwa wakati Mheshimiwa Khatib anachangia hapa ilitakiwa aseme kwa kweli sisi tulikimbia, kwahiyio tunaomba kwa kukimbia kwetu kule Mheshimiwa Rais atusamehe. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khatib unapokea taarifa hiyo?

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme hivi nimesikiliza taarifa yake, lakini nataka

nimfahamishe ndugu yangu Silinde kwamba tuliokimbia ni sisi Wabunge wa CHADEMA na CUF...

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika,taarifa

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Hawakukimbia Watanzania maana yake nini?

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kunti uwe na utulivu kidogo kwasababu taarifa anayojibia ni hii aliyopewa sasa unataka kuweka taarifa juu ya taarifa utulie kidogo eee mama.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Kama kutoka kwetu sisihakuondoa *majority*ya Bunge la Katiba kufikia maamuzi na ndiyo maana ninyi mliendelea kubakia, kama kutoka kwetu sisi kulikuwa na maana kwamba katiba isipatikane? Ninyi mlakaa mkasubiri kufanya nini?Na kwanini mlimalizia? Na ninyi ilikuwa mtoke kuonekana kwamba sisi tulichokataa hakina maana kwaWatanzania, lakini kutoka kwetu sisi na mllichokiamua tumeona bado kama kuna kosa tulifanya lakini kulikuwa na maana kwa Watanzania. Kwa hiyo ina maana kwa Watanzania madai yao, hayakufa kwasababu ya kutoka sisi. Mheshimiwa Silinde usijisahau leo kwa kuwa uko kwenye kiti kikubwa zaidi, kwasababu una V8, ndugu yangu ni mapito tu hata sisi V8 tutapanda. (*Kicheko*).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee nataka nizungumzie habari ya mikopo ya elimu ya juu. Kimekuwa ni kilio cha wanufaika wa mikopo hii na hili ndugu zangu wana CCM wanabunge la kijani, naomba sana tuangalie athari ya makato yaliyoongezwa ya wanufaika wa mikopo, yanawaumiza. Inaanza kujengeka dhana sasa kuona kwamba utajiri ni muhimu kuliko elimu tuondokane na hilo, yaani inaanza kujengeka dhana matajiri wengi siyo wasomi...

**NAIBU SPIKA:** Endelea Mheshimiwa Khatib.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Kwamba matajiri wengi siyo wasomi umuhimu wa elimu utabaki kuwa muhimu kuliko chochote katika maisha ya mwanadamu, lazima tukubaliane hilo. Kwahiyo tuangalie namna ambavyo wamepandishiwa marejesho yale ya 15% na Serikali badala ya 8% ikiwezekana naunga mkono Mbunge mmoja wa CCM aliota hoja jana kwamba ikiwezekana ishushwe mpaka 5% kwa wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu naomba sana hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *mwisho nataka nzungumzie habari ya utawala bora*. Kuna watu wenye mamlaka vyombo vyetu Jeshi la Polisi limekuwa likifanya mambo ambayo siyo utawala bora, juzi iko taarifa inasambaa kwenye vyombo vya habari askari polisi kule Mbeya wamemshusha raia driver kwenye gari na wakamuua, matendo yaliyokuwa yalifanyika Afrika Kusini enzi za Makaburu, ndiyo matukio ambayo vyombo vyetu vya ulinzi baada ya kusimamia usalama wa raia, sasa vinajenga uhasama wa raia. Naomba Serikali itoe tamko kali na zito kuhusiana na kadhia ya raia Yule, driver Yule, aliyetolewa kwenye gari, akapigwa akauliwa na askari wa Jeshi la Polisi. **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa naona Mheshimiwa Waziri amesimama, Mheshimiwa Waziri nadhani nikupe muda ili hili jambo Mheshimiwa Khatib namna alivyolisema ni kana kwamba ana uhakika Polisi wameua raia. Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria. (*Makofii*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwasababu tayari umeshaniruhusu. Nilitaka niombe mwongozo nikiunganisha na kanuni ile inayozuia Mbunge kusema uongo ndani Bunge. Kwanza raia wa kawaida hata uwe kiongozi hatuna ule ujuzi wa kuweza kujua kiini cha binadamu kupoteza maisha. Mamlaka hayo yako kwenye vyombo ambavyo vinaweza vikajua chanzo cha binadamu kupoteza maisha na hata mwanadamu

awapo kwenye mikono ya vyombo haiwezi ikawa chanzo kwamba mikono ile ndiyo imesababisha akapoteza maisha, kwasababu kuna watu wengine anaweza akapoteza maisha akiwa tu kitandani na akawa hajapata tatizo lingine lolote,bali mwisho wa maisha yake ukawa umefikia hapo.

Kwahiylo kwa hili analolisema Mheshimiwa Mbunge huku akijua kuna taarifa ambazo zimetolewa na kukiwa bado kuna kazi zingine zinafanyika kupata undani wake, nadhani si muda muafaka na si mahali pale kwa yeze kulisema hilo na kwasababu hairuhusiwi Mbunge kutoa taarifa ya uongo ningeomba Kiti chako kilitolee maelekezo jambo hili. Pia naomba kitoe onyo watu wasiwe wanatoa toa lugha ambazo zinaweza zikatugawa kama Watanzania kwa misingi tu ya wao kuyachukulia masuala kihisia. Maana yake yameongelewa mambo mengi hapa, mengine wanajihukumu wao wenyewe kuongelea masuala kama hayo aliyoyasema Mheshimiwa Khatib na mengine haya ambayo ameyasema yanayohusisha masuala ya haki. Kusingekuwepo na haki hata wenyewe wasingekuwepo hapa, hii kuwepo hapa tu peke yake inaonesha jinsi ambavyo nchi yetu inajali haki ya kila mtu na hata wao imewalinda wawepo hapa japo haki yao ilitaka kupotezwa na wale ambaao hawapendi haki.(Makof)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge niwasihhi sana kanuni zetu zinaweka mwongozo wa namna ya kupata fursa ya kuzungumza humu ndani, lakini mambo gani unaweza kuzungumzia humu ndani. Taarifa yoyote ambayo huna uhakika nayo namna yako ya kuileta humu ndani usiilete kama uhalsia wala ukweli. Mchango wa Mheshimiwa Khatib kuhusu dereva wa lori ambaye amefariki unaashiria kana kwamba yule mtu aliuawa, siyo tu kuuawa, ameuawa na Polisi. Uchunguzi umefanywa kwa kiasi na uchunguzi bado unaendelea, lakini mtu atasema amewaona Polisi wakiua kwasababu ameona *clip*, yule mtu akishushwa kwenye gari, ile haimaanishi kiongozi wa hadhi ya Mbunge akimbilie kusema wamempiga wakati ile *clip* hakuna mahali inapoonyesha wanampiga.

Kwahiylo ndugu zangu niwaombe sana, yaani haya mambo mengine ndiyo maana mliambiwa mnaweza kuandika hata ujumbe kwa Waziri Mkuu au kwa Waziri kumuuliza kuhusu jambo hilo, kwasababu sisi wote humu ndani tumeapa kuilinda Katiba yetu, sheria zetu tunazotunga wenyewe, tusifike mahali sisi ndiyo tukawa wazua tataruki, wakati sisi ndiyo tunaotakiwa kuwatuliza wananchi kama viongozi. Niwasihi sanaWaheshimiwa Wabunge michango yetu izingatie misingi yetu tuliojiwekea kikanuni, kisheria na kikatiba.

Mchango wa Mheshimiwa Khatib kuhusu hili jambo la askari kuuawa kwa namna alivyouleta, nauondoa kwenye taarifa rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Zaitun Swai atafuatiwa naMheshimiwa Zainab Katimba.

**MHE.SALOME W. MAKAMBA:** Mwongozo

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo umeombwa wapi, MheshimiwaSalome Makamba

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:**Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba Mwongozo wa kiti chako juu ya matumizi ya kanuni hizi hasa kanuni ya 70 kwasababu na ikifuatia maamuzi ambayo yametolewa na Kiti chako kwa sababu kanuni ya 70(1)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salome Makamba, kaa kwanza, kaa chini. Waheshimiwa Wabunge huwa nazungumza mara nyingi niwakumbushe tena maamuzi yanayotolewa na Kiti hayahojiwi hapa ndani.(*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salome Makamba, kaa kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, huwa nazungumza mara nyingi, niwakumbushe tena maamuzi yanayotolewa na Kiti hayahojiwi hapa ndani. Niwakumbushe tena, Kanuni hizi

ndiyo maana nimewashauri mkazisome, Kiti kikifanya maamuzi hayahojiwi humu ndani, hayajohojiwi kama nimekaa mimi nillyefanya maamuzi wala akija kukaa mtu mwingine hayahojiwi. Kanuni zinatoa mwongozo ufanye nini kama hujaridhika na maamuzi ya Kiti. Utaratibu ni mzuri kabisa kila jambo liko humu tukasome kanuni. (*Makofi*)

Jambo hilo lipelekwe linakotakiwa kupelekwa kwa mujibu wa Kanuni zetu. Nadhani tumeelewana vizuri kwenye hilo. Kwa hiyo, maamuzi yakitoka yameshatoka na wewe fuata utaratibu wa kutokuyakubali, usisimame hapa kuzungumzia maamuzi ya kwangu mwenyewe kwa sababu sasa maana yake unaona kama vile, sasa lazima aamue mtu mwingine siyo wewe. Kwa hiyo, ukisimama hapa inakuwa kukikosea heshima kitu na mimi Kiti lazima kiheshimiwe, lazima kiheshimiwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Zaytun.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo wako, ungenisikiliza tu wala siongelei hayo maamuzi yako.

**NAIBU SPIKA:** Siwezi kukusikiliza kwa sababu umesema unaomba mwongozo kwa mwongozo niliota mimi.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Hapana! Sijasema hivyo Mheshimiwa.

**NAIBU SPIKA:** Naomba ukae Mheshimiwa Salome.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka ufanuzi wa Kanuni na wala siongelei mwongozo ulioutoa.

**NAIBU SPIKA:** Mimi hapa naweza nikakuruhusu au nisikuruhusu, kitu ambacho nalazimika kukuruhusu ni kuhusu utaratibu umeomba mwongozo kaa chini. Mheshimiwa Zaytun.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu na vilevile naomba niwashukuru wananchi wangu wa Mkao wa Arusha hususan kinamama wa Mkao wa Arusha kwa kuniamini kuwa mwakilishi wao katika Bunge hili. Nawaahidi wananchi wangu hususan kinamama wa Arusha sitawaangusha. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa, naomba nishukuru familia yangu wakiongozwa na mama yangu mpendwa mama Sifa Swai, mume wangu na mtoto mpenzi Alina. Wote hawa kwa nyakati tofauti wamekuwa wakinishauri vyema jinsi gani ya kuwaongoza wananchi wetu na vilevile wananiongezea busara. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie hotuba ya Rais, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na suala la elimu. Serikali imefanya mambo makubwa sana kwenye awamu zilizopita kwenye suala la elimu na yote haya imeyafanya kwa sababu inatambua umuhimu wa elimu na mchango wake mkubwa katika uchumi wa Taifa letu. Kutokana na umuhimu huu, Rais ameeleza mambo mbalimbali yanayohusiana na elimu katika hotuba yake na majawapo ikiwa ni kuanzisha shule za sayansi za watoto wa kike katika kila mkoa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi ni mnufaika wa elimu iliyotolewa bure na Serikali katika masomo haya ya sayansi na hisabati. Kwa hiyo, natambua vizuri changamoto wanazozipata watoto wa kike katika masomo haya na naipongeza Serikali kwa kuamua kuanzisha shule hizi ili kutatua changamoto zile. (*Makof!*)

Mheshimia Naibu Spika, naomba niishauri Serikali, suala la shule za sayansi ni muhimu sana na linatakiwa lichukuliwe kwa umuhimu wake. Shule hizi zinahitaji umakini mkubwa kwenye kuziendesha. Kwa kuanza zinahitaji kuwa na ubora wa hali ya juu, maabara zenyenye viwango vya juu na

walimu wenye uwezo mkubwa wa kuwafundisha wanafunzi hawa. Vilevile shule hizi zinahitaji nyezo mbalimbali kama vitabu na kadhalika. Kwa hiyo, naiomba Serikali isikurupuke kwenye suala hili, iliangalie kwa umakini na tuhakikishe shule hizi zinajengwa kwa umakini wa hali ya juu tukizingatia hayo mambo niliyotaja ili basi lengo la Serikali liweze kutimia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi sote ni mashuhuda, tumeshuhudia jinsi halmashauri zetu zinavyopata shida sasa hivi kujenga madarasa na kutafuta madawati katika shule mbalimbali na wananchi wetu pia wanalamika kwa sababu michango ni mikubwa kusaidia maendeleo haya. Kwa hiyo, naiomba Serikali suala hili la ujenzi wa shule za sayansi kwa watoto wa kike isilichukulie juu bali ilichukulie kwa umakini na tulianze suala hili mapema tuisubiri mpaka mwisho wa miaka mitano ili tuweze kuzijenga shule hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vilevile niongelee suala la mikopo ya asilimia 10 inayotolewa kutokana na mapato ya halmashauri. Tumeona jitihada kubwa sana za Serikali inazofanya kuwawezesha wananchi wake kiuchumi kupitia mikopo isiyokuwa na riba na mikopo mingine yenyе riba nafuu na vilevile kupitia mifuko na *program* mbalimbali zilizoanzishwa na Serikali. Mikopo hii ya asilimia 10 inatolewa kulingana na mapato ya halmashauri husika na sisi sote tunajua kwamba halmashauri zote hazilingani kimapato. Kwa hiyo, *formula* hii haizingatii halmashauri zenye changamoto ya vyanzo vya mapato. Mikopo hii isiwe ni adhabu kwa wanufaika walioko vijijini na sehemu zenye changamoto za mapato. Naiomba Serikali iweze kuangalia *formula* hii kwa undani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatolea mfano mdogo tu, hauwezi kulinganisha mapato ya Ilala, Kinondoni na halmashauri za Ngorongoro, Longido au Monduli na sehemu zingine za vijijini. Kwa hiyo, tunaomba Serikali yetu iangalie fomula hii na iweze kugawa mikopo hii kwa usawa. Suala hili pia litapunguza *gap* lilipo la umaskini wa vijijini na mijini ambapo nadhani ndiyo lengo kubwa la Serikali yetu,

tupunguze *gap* la umaskini lililopo kwa sasa vijjini na mijini.  
*(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba nichangie kwenye sekta ya maji. Nashukuru Mheshimiwa Rais bado anatambua kuna changamoto nyingi za maji, hususan vijjini. Serikali yetu imefanya mambo mengi sana hasa kutekeleza miradi mikubwa ya maji ikiwemo mradhi wa shilingi bilioni 520 ulioko Mkoani Arusha. Naomba niishauri Serikali isiwekeze tu kwenye miradi mikubwa kama hii vilevile iangalie vyanzo vingine vya maji ikiwemo uchimbaji wa visima virefu. Nitatolea mfano tu, mradhi huu wa shilingi bilioni 520 unapita Wilaya ya Arumeru lakini kuna kata katika Wilaya ya Arumeru kama Kata ya Nduruma haina maji. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie pia vyanzo vingine vya maji ukiachia mbali miradi hii mikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. *(Makof)*

**NAIBU SPIKA:** Shukrani sana. Mheshimiwa Zainab Katimba, kama muda wetu utaruhusu tutamalizia na Mheshimiwa Constantine Kanyasu.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa ajili ya baraka zake nyingi sana. Pia nikishukuru Chama changu cha Mapinduzi kwa kuendelea kuniamini. Kipekee kabisa niwashukuru wanawake wa Mkoa wa Kigoma, wapiga kura wangu ambao wameniamini mimi kjana wao niweze kuwa mwakilishi katika Bunge hili Tukufu. Nachowaahidi sitowaangusha. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi sote ni mashahidi ya namna gani Serikali ya Awamu ya Tano imefanya jitahada kubwa sana ya kuwawezesha wanawake lakini pia kusimamia masuala ya kijinsia. Hata ukisoma kwenye hotuba hii ya Mheshimiwa Rais, ukurasa namba 4, utaona Mheshimiwa Rais ametoa ahadi na amesema naomba kunukuu: Kwa msingi huo, napenda nitumie fursa hii kuwaahidi kuwa Serikali ninayoiongoza itaendelea kuwaamini

wanawake katika kushika nafasi mbalimbali za uongozi. Wanawake na kinamama hoyee". (*Makof*)

**WABUNGE FULANI:** Hoyeee.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni katika Serikali ya Awamu ya Tano katika historia ya nchi hii Tanzania tumepeata Makamu wa Rais wa Kwanza mwanamke, Mheshimiwa mama yetu Samia Suluhu Hassan ambaye pia amefanya kazi vuziri sana na sisi sote ni mashahidi ni namna gani ye ye amedhihirisha uongozi wa mwanamke jasiri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sio hivyo tu, kuna mifano mingi ya wanawake wengi ambaao wamepewa fursa katika Serikali hii ya Awamu ya Tano ikiwemo wewe mwenyewe Naibu Spika, Mbunge wa Jiji la Mbeya. Tuna Mheshimiwa Jenista Mhagama, aliyekuwa Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, tuna viongozi wengi pia kwenye Serikali, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu, Wakurugenzi, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Mabalozi na wote wanafanya kazi nzuri sana. Kwa hiyo, naomba nichukue nafasi hii kusisitiza na kuwaambia wanawake wenzangu tunavyopewa nafasi sisi wanawake tufanye kazi kwa weledi ili tuhakikishe tunajenga taswira nzuri ya uongozi wa mwanamke katika jamii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma kwenye ukurasa wa 17 - 19 wa hotuba ya Mheshimiwa Rais, utaona ameelezea mafanikio makubwa ya kiuchumi yaliyofanyika katika kipindi cha miaka mitano. Ameelezea ni namna gani sisi kama nchi tumeingia katika uchumi wa kat, tena tumeingia katika uchumi wa kat miaka mitano kabla ya ule muda tuliotarajia, haya ni mafanikio makubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye ukurasa wa 20 amesisitiza kwamba mipango hii ya kuendeleza na kukuza uchumi wetu itaendelea. Amezungumzia mipango ya kuwawezesha wanawake kiuchumi, masuala ya kuhakikisha kwamba anatoa kipaumbele kikubwa sana katika sekta

binafsi lakini pia kutengeneza ajira milioni 8. Kusema kweli mipango mingi ya Serikali ni mizuri, naomba kusisitiza katika maeneo mawili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha kwanza, naomba sana Serikali ihakikishe na isimamie katika hiki kipindi kunakuwa na sera, sheria, miongozo na taratibu ambayo inagusa masuala ya uwekezaji, biashara na uchumi isiwe inabadilika sana ili kutoa fursa ya wawekezaji na wafanyabiashara kuzitambua lakini kufanya biashara kwa utulivu. Pia Serikali isimamie utekelezaji wa *blue print*, kazi kubwa imefanyika lakini sasa tusimamie utekelezaji wa haraka ili kuhakikisha mazingira ya uwekezaji na kufanya biashara yameboreshwa na yamekaa vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuishauri Serikali katika sekta ya elimu. Katika sekta ya elimu sisil tunajenga uchumi wa viwanda, kwa hiyo lazima tuhakikishe tunaandaa rasilimali watu ambao wataenda kuhudumia uchumi wa viwanda. Kwa hiyo, lazima tuwekeze katika kada ya katika kwa sababu ndiyo inayohitajika kwa ajili ya kuhudumia uchumi wa viwanda. Kwa hiyo, nguvu yetu kubwa tuangalie katika zile kada za katika kwa maana yaani tuangalie wale wanafunzi wanaosoma cheti, mafunzo ya ufundi na stashahada, hawa ndiyo wengi watakaohitajika katika uchumi wa viwanda. Hata Bodi ya Mikopo iwawezeshe hawa wanafunzi wa hii kada ya katika ili kuzalisha rasilimali kubwa ambayo itahijika kwa ajili ya uchumi wa viwanda. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba sana tuangalie katika mtaala ya elimu. Katika mitaala yetu ya elimu tuhakikishe katika masomo yote angalau kuwe na mafunzo ya msingi ya namna gani ya kuanzisha na kuendeleza biashara ili mhitimu anapomaliza chuo hata kama amesoma shahada tuseme ya *sociology* au *political science* na anashindwa kuajiriwa katika ajira rasmi basi aweze yeye mwenyewe kuwa mawazo ya namna gani yeye mwenyewe anaweza akaanzisha biashara na kuiendeleza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na nawaomba sana Watanzania wote kila mmoja wetu ana jukumu la kuhakikisha anatimiza wajibu wake ili ile dhamira ya dharti ya Mheshimiwa Rais ya kulijenga Taifa hili iweze kutimia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Constantine John Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimshukuru sana Mungu kwa kunipa kibali cha kurudi tena kwenye Bunge lako Tukufu. Nakishukuru sana chama change, Chama cha Mapinduzi kwa kunitfea na baadaye kushinda uchangazi Jimbo la Geita Mjini. Naomba kuwaahidi wananchi wa Jimbo la Geita Mjini kwamba nitaendelea kuwa mwakilishi mwaminifu sana kwao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Rais ya kufungua Bunge ukurasa wa 41 alizungumzia madini na alisema sekta ya madini imekua kutoka mchango wake katika malipo ya pato la Taifa wa shilingi billioni 168 mpaka 527 lakini katika pato la Taifa kutoka asilimia 3.4 mpaka 5.2. Naungana na Mheshimiwa Rais kuwapongeza sana Wizara ya Madini wanafanya kazi vizuri. Mimi ambaye natoka jimbo ambalo uchumi wake kwa asilimia zaidi ya 80 unategemea sana pato la madini, naona faida ya mabadiliko ya Sheria ya Madini ya mwaka 2017 ambayo imeleta heshima katika matumizi ya fedha za CSR katika Halmashauri yangu ya Mji wa Geita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo moja tu hapa wachimbaji wadogo *investment capital* yao ni kubwa kuliko faida wanayoipata. Teknolojia wanayotumia na duni na bado mitaji ni midogo. Unakuta wachimbaji wadogo wanaendelea kubahatisha. Inaweza kutokea *rushwataanza* kuchimba mpaka wanafika mita 60 mpaka 100 hajaanza

kufanya uzalishaji lakini tunazo teknolojia. Niombe Wizara kama makampuni yanafanya *CSR*na yenyewe ifanye hivyo, ileta mitambo ya kutosha ili sehemu *rush* zinapotokea wawaambie wachimbaji kwamba eneo hili mnalochimba dhahabu zipo au madini yapo na yapo umbali gani na mlalo wa miamba. Namna tunavyokwenda sasa hivi utakuta ni kweli tunaongeza uzalishaji wa dhahabu lakini kimsingi gharama za uzalishaji wa dhahabu hizo ni kubwa kuliko faida ambayo wachimbaji wadogo wanapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili katika eneo hilo, juzi Mheshimiwa Rais akiwa kule Mbogwe alisema kwamba siyo sahihi wachimbaji wakubwa wanapopata */license* kuamini kwamba sasa wamenunua haki ya wananchi ya ardhi na kukiuka sheria ambazo zipo. Wananchi wangu katika maeneo ya Nyakabale, Magema, *Compound* na Katoma wameendelea kuishi kwenye mgogoro wa takriban miaka 20. Ni kweli wako ndani ya leseni ya mgodi lakini mashamba yao ya asili sehemu ambayo mgodi haujataka kuanza kuchimba, hawaruhusiwi hata kwenda kukata kuni. Sasa hivi kuna ulinzi katika maeneo ya Magema hawaruhusiwi hata kupita nyumba moja kwenda nyumba nyingine kwa sababu ni ndani ya mgodi wa leseni. Nataka kushauri, Mheshimiwa Waziri alitolea maelekezo lakini Serikali ya Mkoa imeendelea kuweka askari pale, wananchi wameendelea kunyanyaswa tutoe mwongozo sahihi kama mgodi unataka eneo lile walipe fidia kama wananchi bado wanatakiwa kukaa pale wawaache wafanye kazi zao kwa uhuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende eneo la pili kwenye ukurasa wa 27 sehemu ya kilimo. Ni kweli kwamba nchi hii inategemea ajira kwenye kilimo ambacho ni zaidi ya asilimia 80 na kimesaidia sana kudhibiti mfumuko wa bei na mimi nakubaliana na hilo. Nataka kutoa *challenge* kidogo hapa kwamba bado Watanzania wanalima *very local* na shida ya Watanzania siyo ukubwa wa mashamba. Mheshimiwa Rais anaweza kuendelea kuongeza mashamba, kubadilisha hifadhi, kubadilisha mapori ya akiba lakini shida hapa ni *productivity* kwenye maeneo walijonayo wakulima. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bado wakulima mtu analima heka kumi anapata gunia kumi za mahindi. Nataka kuwaambia Wizara ya Kilimo twenda sambamba na hotuba ya Mheshimiwa Rais, tulime kisasa na hili linaweza likaonekana kabisa kwa macho lakini tupate mbegu za kisasa na tupate huduma za ugani za kisasa. Utasikia tu kwenye magazeti na vitabu huduma zipo lakini kimsingi wakulima wetu bado wanalima kwa kizamani sana, *productivity* ya heka moja ni sawasawa na mtu aliyelima nyuma ya nyumba. Niiombe Wizara hii katika kipindi cha miaka mitano iweze kufanya jambo hili kwa umakini zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka kuona kwamba kilimo cha kawaida hakitiliwi maanani sana wakati wa mavuno ya mazao ya biashara, maeneo yetu sisi tunalima pamba, *store* zote za pamba zimeoza, zimeanguka na zimegeuka kuwa nyumba za watu binafsi. Kwa hiyo, niombi Wizara iweze kujipanga vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo tunalolipata kwenye kilimo liko pia kwenye mifugo. Utuna kuna uboreshaji wa matumizi ya mashamba ya *NARCO*, lakini bado hata walio katika *NARCO* kinachowafanya waonekane wanafuga kisasa ni fensi, ukiingia kwenye shamba la *NARCO* utakuta hakuna mashamba ya nyasi, hakuna teknolojia unaotumika lakini bado ufugaji wa mle ni *local*, usambazaji wa mbegu za kisasa ni wa kizamani. Kwa hiyo, utakuta wafugaji hawa hata tunazungumza tuna ng'ombe milioni 33 hazijawasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe sana hasa katika kipindi hiki tunachokwenda nacho mabadiliko haya yawewe kutafsiriwa kwenye level ambayo wakulima na wafugaji wa kawaida wataondokana na kufuga ng'ombe 500 zenyе kilo 250 waende wafuge ng'ombe 100 zenyе tani moja ambazo zinaweza kuzalisha maziwa mengi lakini teknolojia iweze kusambazwa kwa njia ya urahisi. Tumeangalia maeneo mengi sana unakuta migogoro mingi ya wakulima na wafugaji, kwa nini? Ni kwa sababu mkulima akipata eneo la kwenda kulima akinunua mifugo anahamia hapo na akihamia hapo

anajenga, kesho yake anasogea mbele anapata eneo la kulima anahamia na anajenga kwa sababu anafuga ng'ombe nyingi ambazo anashindwa kuzimudu kulingana na eneo alilonalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niiombe Wizara katika kipindi iweze kutumia muda wa kutosha kufanya mabadiliko ya kisayansi. Unayaona haya mabadiliko kwenye vitabu lakini wafugaji na wakulima tunaokaa nao sisi bado wanafuga kizamani na wanalima kizamani na hakuna mabadiliko yoyote ambayo yameendelea kuwepo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda la mwisho, nimeona juhudhi kubwa za Wizara ya Nishati katika Mikoa ya Pwani, ikisambaza gesi kwa ajili ya matumizi ya majumbani. Nililitamani kujua mkakati wa Serikali wa gesi hii kuifikisha kwenye mikoa ambayo iko nje ya Pwani, kwa mfano gesi hii itafika lini Mwanza au Geita ili tuweze kuachana na matumizi ya kuni na mkaa? Ziko taasisi zinatumia zaidi ya *cubic* mita 40 za kuni kwa mwezi, tunafanya nini kuzibadilisha taasisi hizi ziweze kutumia nishati ya gesi asilia tuliyonayo na kuweza kuzuia misitu yetu ambayo inaharibika kila siku. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa muda wetu uliobaki hatutaweza kuwa na mchangiaji mwingine. Nitaje majina machache ambao tutaanza nao kipindi chetu cha mchana, Mheshimiwa Jumanne Sagini, Mheshimiwa Assa Makanika, Mheshimiwa Deo Sanga, Mheshimiwa Kenneth Nollo, Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, Mheshimiwa Innocent Bilakatwe, Mheshimiwa Anna Lupembe, hao tutaanza nao mchana.

Kabla sijaahirisha shughuli zetu hapa nilikuwa nimeombwa mwongozo na Mheshimiwa Leah Komanya kuhusu majibu ya maswali yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu

Waziri wa Maji. Mheshimiwa Leah Komanya ameniandikia hapa kwamba mwongozo wake ameomba uondoke. Nilikuwa nimeahidi kutoa huo mwongozo baadaye ili nipitie Taarifa Rasmi za Bunge lakini Mheshimiwa Leah Komanya ameuondoa mwongozo wake. Kwa hiyo, Taarifa Rasmi za Bunge zitaonesha hivyo aliomba mwongozo na ameuondoa mwenyewe. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni leo.

*(Saa 07.02 Mchana Bunge lilitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lillrudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

Hotuba ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliyoitoa Wakati wa Ufunguzi wa Bunge la Kumi na Mbili, Tarehe 13 Novemba, 2020

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge majadiliano yanaendelea. Yapo majina ambayo tuliyataja kabla ya kwenda mapumziko mafupi. Mheshimiwa Anna Lupembe atafuatiwa na Mheshimiwa Jumanne Sagini na Mheshimiwa Assa Makanika ajiandae.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ninaomba nimshukuru Mungu ambaye ametuumba, ametupa uhai, hatimaye tu wazima kabisa. Vilevile naomba niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Nsimbo kwa kuniamini niwe Mbunge wao wa jimbo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa muda huu niweze kuchangia hotuba ya Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwanza kabisa ninaomba nimshukuru sana Rais na kumpongeza kwa kazi kubwa sana ambayo ameifanya kuanzia mwaka 2015 mpaka 2020. Tumeona jitihada zake kubwa ambazo zimewafanya Watanzania wawe na imani kubwa sana na Rais wetu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona katika hotuba yake alivyoendelea kusema ataendelea kuwatumikia Watanzania kwa kila hali na nguvu zote. Ninaomba niipongeze sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi kubwa, miradi mikubwa imefanyika, tumeiona kwa macho miradi ambayo ilikuwa inaenda sambamba, miradi ya maji, miradi ya barabara, miradi ya *standard gauge*, bandari, kila kitu kimekwenda sambamba. Tunaomba tuipongeze sana Serikali kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wameifanya kwa muda mfupi na malengo ni mazuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wengi wameongea na nijikite kwenye ajira. Rais amesema ataendelea kuboresha ajira na tumeona ajira nyingi sana, yupo ndani ya kampeni lakini akamuagiza Waziri Jafo aongeze *staff* kuditia walimu ajira 13,000 ndani ya kampeni. Ni jitihada kubwa sana. Tullaona jinsi gani anaongeza madaktari ili kuendelea kutibu wagonjwa, madaktari bingwa. Tumeona jitihada ambazo zinaendelea kuditia ajira, lakini bado tunahitaji ajira kwa sababu kila sehemu tukienda mapungufu ni mengi sana kuditia ajira.

Tunahitaji sana tuongeze ajira kwa sababu tunaendelea kujenga zahanati, tunaendelea kujenga vituo vya afya na Rais wetu ametujengea hospitali katika mikoa mingi, hospitali za mikoa zingine za kanda, hiyo ni jitihada kubwa nzuri lakini bado watenda kazi ni wachache. Tunaomba Serikali iendelee kupambanua kuhusu ajira kwani inahitajika sana kwa kipindi hiki kwa sababu tumeongeza vitu vingi, shule zetu za *secondary* tunaongeza siku hadi siku, shule

zetu za kata tunajenga, tunafungua shule, tunahitaji watenda kazi kwa ajili ya kutufundishia watoto wetu

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais amejitahidi sana kwenye upande wa kilimo, tulikuwa tunapata shida pembejeo viatilifu matrektta, mbegu lakini sasa hivi mkulima anakuta mbolea madukani, anakuta pembejeo madukani, mbegu madukani, kusema kweli hali ya kilimo imeendelea kuwa nzuri siku hadi siku kutokana na uwezo ambao imeonesha Serikali ya Awamu ya Tano tunaomba tuwapongeze sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kidogo kwa sababu kilimo ni uti wa mgongo na tunategemea sana, kilimo kije kutusaidia kupitia viwanda, Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli anatamani sana nchi yetu ya Tanzania tuwe na viwanda ili vijana wetu waweze kupata ajira na vile vile malighafi yetu iweze kufanya kazi ndani ya nchi yetu. Kilimo ndio kinaweza kufanya hivyo ili tuweze kupata viwanda vingi, lakini bado kuna maeneo ambayo hatujaweza kuwafikia wakulima vizuri, tukawapa semina mbalimbali na tukawawezesha wapate matrektta ili waweze kulima kilimo bora ambacho kitaweza kuleta tija. Naomba sana Serikali kwenye kilimo tuendelee kupaweka vizuri kwa ajili ya vifaa ambavyo vitawafanya wakulima waweze kulima vizuri ili tuweze kupata viwanda ambavyo tutapata ajira na vitu vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nakwenda kwenye ufugaji; kwenye mambo ya ufugaji leo hii tumeshuhudia kuna viwanda vyta kuchakata nyama viko viwanda vyta samaki, tumetoa ajira na vile vile sasa hivi tunaweza tukasafirisha wanyama wetu nje ya nchi. Naomba nipongeze kufikia hatua nzuri ambayo tumeona ndege ya Ethiopia ilishakuja hapa kubeba *cargo* zetu za mizigo mbalimbali ambazo zinasafirishwa nje ya nchi ili kuendelea kukuza uchumi wa Watanzania, ndio maana unakuta sasa hivi watu wengi wametamani kufuga ili kuweza kupata uchumi mzuri. Naomba niipongeze sana Serikali ya Awamu ya Tano, kazi ni nzuri inaonekana wazi wazi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa barabara, Serikali imejipambanua sana kuhusu barabara za lami, tumeunganisha mikoa, sasa hivi hata sisi watu wa Mkoa wa Katavi tukitoka Dodoma mpaka tufike Katavi ni masaa saba, nane, tunaomba tuipongeze sana Serikali, tunakwenda kwa lami sehemu zote. Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuliamefanya kazi kubwa sana, lakini bado sisi Wabunge wa Majimbo tunaomba Serikali sasa ijkite kuongeza bajeti ya *TARURA* ili sasa zile malighafi ambazo zinatoka ndani ya vijiji vyetu, vijiji vyetu barabara hazipitiki kabisa, wakulima wanalima, lakini sasa kutoa mazao ndani ya vijiji vyetu ili tuweze kufisha sokoni na kipindi hiki cha mvua, inakuwa ngumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya mwaka jana ya *TARURA* sidhani kama ilitumika kabisa, kulikuwa kuna mitaro barabara zimekatika lakini hazikuweza kurekebishwa kabisa mpaka imekutana na mvua nydingine. Tunauliza shida ninini? Wanasema shida ni bajeti, kwa sababu barabara za vijiji zikitengenezwa vizuri, zikawa zinapitika ina maana malighafi zote zinazopatikana ndani ya vijiji vyetu zitatoka kwa urahisi.

Sasa hivi sisi tunasafiri vizuri, tukitaka kwenda sehemu tunakwenda, ndege zipo tunamshukuru sana Rais wetu amenunua ndege, usafiri ni mrahisi na mwepesi. Tatizo linakuja sasa ndani ya *TARURA*, hatujajipangia bajeti nzuri, naomba sana Serikali kwenye upande wa *TARURA* waongeze bajeti ili tuweze kutengeneza barabara na madaraja ndani ya maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda umeisha?

**NAIBU SPIKA:**Ndiyo.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naomba niunge mkono hoja.(*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jumanne Sagini atafuatiwa na Mheshimiwa Assa Makanika na Mheshimiwa Deo Sanga ajiandae.

**MHE. JUMANNE A. SAGINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nianze kwakumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana hapa na kwangu mimi ni mara ya kwanza kuzungumza katika Bunge lako Tukufu. Niwashukuru pia wana CCM na hasa Wajumbe wa Butiama kwa kuniwezesha kupita kwenye kura za maoni na baadaye vikao vyta chama vikaleta jina na baadaye nikapita bila kupingwa. Watu wa Butiama nawaahidi mtumishi bora uliotukuka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishukuru familia yangu kwa kunipa moyo wakati wote wa harakati na wanaponipa moyo ninapohudumia wananchi wa Butiama kupitia Bunge lako Tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hotuba za Mheshimiwa Rais zote mbili, napenda nianze kusema naunga mkono hoja hiyo, lakini nianze kwa kusema moja kwa moja zinapaswa kuwa rejea kwetu sote hususani wasaidizi wa karibu sana wa Mheshimiwa Rais kwa maana ya Mawaziri wetu na watendaji wote wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia hotuba hizi hakuna jambo aliloliacha kwenye sekta ya kilimo, kwa mfano imezungumzwa kwa kirefu kuanzia ukurasa wa 13 mpaka wa 15 lakini imekwenda kutaja mifugo mpaka ukurasa wa 17 ambapo Mheshimiwa Rais amesisitiza umuhimu wa kuongeza tija katika mazao ya ukulima, ufugaji na uvuvi. Sasa ushauri wangu kwenye hili baada ya Rais kulizungumza kitaifa, ni jambo jema sasa wasaidizi wake warudi kwenye ngazi za utekelezaji ili kweli kilimo hiki kiweze kuleta tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Wabunge wamezungumza hapa kiwango cha chini cha uzalishaji kwa heka, nimehudumu pale Simiyu, wastani kwa hekari moja ya pamba wananchi wa kawaida wanapata kilo mia sabini, lakini pale pale Simiyu Wilaya ya Maswa wapo wakulima bora wanaweza kupata kilo 1,200 kwa hekari moja. Sasa kumbe upo uwekezano wa kuongeza *productivity* kwa heka badala ya kufikiria kuongeza ukubwa wa mashamba ni muhimu wataalamu wetu wajikite kuwaelekeza wananchi

hasa wakulima namna ya kuongeza uzalishaji kwa hekari moja, mbili kuliko kuongeza ukubwa wa mashamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye mifugo, nilikuwa naongea na wananchi wajimbo langu nilifanya ziara baada ya vikao vilivyopita, unakuta ukubwa wa ng'ombe kwa maana ya uzito ng'ombe anaweza akawa na kilo 90, tukawa tunatania baadhi ya wananchi wanakilo 150, 120 kwa uzito, ina maana mtu anamzidi ng'ombe uzito, jambo ambalo halikubaliki. Sasa Wizara ya Mifugo na Wizara ya Kilimo tunaona wameanza vizuri na kasi nzuri, nampongeza Waziri na Wasaidizi wake, lakini zaidi na Katibu Mkuu kwa kazi ambayo wameanza kwa kasi kwenye sekta ya kilimo, ambapo wameshakutana na wataamu lakini wamesogeza huduma za ugani karibu na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Simiyu kwenye viwanja vya 88 Nyakabindi utaalam wote wa sekta ya mazaoupo pale, kwa hiyo wananchi wetu wa mikoa ya jirani wamekuwa wakienda pale kupata elimu ya namna ya kuongeza tija kwenye mazao yao. Vile vile nimeona kwenye sekta ya mifugo Waziri na wataalam wanajitahidi kuhamilisha mifugo (*artificial insemination*)ili tuweze kupata koo bora na hivyo tuweze kupata uzalishaji wa mifugo iliyokuwa bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais amezungumzia miundombinu na mimi kwenye hili namuunga mkono sana na naomba Watanzania wengine tuendelee kumuunga mkono kwenye hili. Nakumbuka kabla ya Rais wetu hajaingia kwenye sekta ya ujenzi watu wa Kanda ya Ziwa wakitaka kwenda Dar es Salaam ilikuwa inalazimika wapite Bukoba, waende Kampala, waende Nairobi ndiyo wafike Dar es Salaam, unaenda kwenye nchi yako unapita kwenye nchi nyingine mbili, lakini leo mtu anatoka Bukoba anaingia sehemu yoyote ya Tanzania kwa lami, hivi ni vitu vya kumpongeza Mheshimiwa Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Jiji la Dar es Salaam tafiti za *World Bank*, nakumbuka niliwahi kutoa taarifa iliyokuwa inaonesha kwambakwa ile foleni tuliyokuwa nayo,

tulikuwa tunapata hasara, tunapoteza karibu shilingi bilioni 40 kwa siku kwa ile foleni tu, leo Rais amesaidia kufungua hizo barabara, kuweka hizo *flyover*, kupanua ukubwa wa barabara, *efficient* ya usafiri umeanza kuiona, *frustration* ambazo wananchi walikuwa nazo, wawe wanafunzi kuchelewa shule, wawe wagonjwa wanaopelekwa hospitali, wawe wasafiri wanaoenda *airport* walikuwa wanakumbwa na msongo wa mawazo kwenye foleni za barabarani, lakini leo tunaona Dar es Salaam inavyopitika, tunataka mikoa yote iwe hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba Rais wetu aendelee, nina imani hata nchi jirani wanatuonea gere kwa namna tulivypambana kuboresha miundombinu yetu. Ushauri wangu kwenye sekta hii ya usafiri na usafirishaji ni kushuka kule chini, Waheshimiwa Wabunge wamesema karibu wote kwamba kiwango cha fedha wanazopewa *TARURA* hakitoshelezi sekta ya *TARURA* kuboresha barabara za halmashauri na za vijijini. Nafahamu sababu, wakati wanaweka hivi viwango vya asilimia 30 kwa 70 kiwango cha barabara za halmashauri kilikuwa ni kilometra 58, leo tunazungumza zaidi ya kilometra 120,000 za barabara za vijijini, sasa kuendelea kuwapa kiwango cha asilimia 30 kwa kweli ni kuwatweza wataalam wetu wa *TARURA* na kufanya walaumiwe pasipo na sababu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunazungumzia hizi barabara kuu, naomba pia barabara za wilaya zetu zizingatiwe. Nafahamu tunayo barabara kutoka Ziroziro kwenda Bukabwa, Bwiregi, Nyamimange, Silolisimba hadi Serengeti, ushauri wetu hizo barabara zisaidiwe. Naona sekta ya ujenzi wanajenga kilomita mbili mbili kila mwaka, kwa kasi hii itachukuwa miaka makumi kabla hatujafika mwisho. Piai ipo barabara ya kutoka Mazami kuititia Butiama kwenda Nata, hii nayo ikamilike, maana ni ya muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye sekta ya nishati...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:**Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. JUMANNE A. SAGINI:**Mheshimiwa Naibu Spika, basi nashukuruna naunga mkono hoja.(*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Assa Makanika atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Sanga na Mheshimiwa Innocent Bilakwate ajiandae.

**MHE.ASSA N. MAKANIKA:**Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema ambaye kwa kweli amemwezesha kila mmoja wetu kufika mahali hapa. Jambo la pili, nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais pamoja naChama changu Cha Mapinduzi ambacho kwa kweli kimeweka imani kubwa kwa sisi vijana, kimetuamini katika umri huu, ni jambo kwa kweli kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais na Chama chetu Cha Mapinduzi. Kwa kweli ni jambo ambalo mimi katika umri huu nisiposhukuru tena mara ya pili nitakuwa sijamfanya haki Mheshimiwa Rais kwa kusema ahsante sana Mheshimiwa Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hotuba zake mbili ambazo alizitoa Mheshimiwa Rais nitajikita kuchangia sanasana katika hotuba yake aliyeitoa Novemba 13 mwaka 2020. Kumekuwa na jambo ambalo ningependa nizungumzie katika hotuba ya Rais na jambo lenyewe ni juu ya kilimo. Jambo la mafuta ya kula limekuwa *nicross cutting issue* na imekuwa ni *current matter* ambayo kwa kweli inaendelea kujitokeza mwaka hadi mwaka na mimi leo nitakuwa na mchango kidogo juu ya suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa mafuta ya kula hapa nchini naomba iwe ni ishara ya Serikali yangu ya Chama Cha Mapinduzi na chini ya Jemedari Dkt. John Pombe Magufuli kuwa ni ishara ya katuonyesha kwamba tunahitajika kufunga kamba ndani ya viuno vyetu ili tuweze kufikia azma ya viwanda kikamilifu. Kwa takwimu tu haraka haraka nchi yetu inaonyesha kabisa kwamba inazalisha tani

laki mbili za mafuta ya kula, lakini mahitaji yetu ni tani laki tano kwa mwaka, hivyo tunakuwa na upungufu wa tani laki tatu ambazo nchi yetu inaagiza tena hasa katika nchi za bara la Asia san asana Malaysia na nchi ya Indonesia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa tafsiri hiyo inaonyesha kabisa kwamba tunachukua pesa nyingi za kigeni kwa ajili ya kuagiza bidhaa hii ya mafuta ambayo nikisoma hotuba ya Mheshimiwa Rais ukurasa wa 15, naona hii ni aibu kubwa kwa nchi kama Tanzania ambayo ina ardhi yenyе rutuba kuagiza mafuta nje. Kwa hali halisi ilivyo nakulingana na matamko mengi ambayo Serikali imekuwa ikitoa, naomba nijielekeze kuionesha Serikali kwamba kuna wajibu mkubwa wa kuelekeza katika zao hili la mbegu ambapo mafuta yanatokana na mbegu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, mwezi Mei, 2017 aliyekuwa Waziri wa viwanda wakati huo Mheshimiwa Mzee wangu Mwijage alinukuliwa akisema: "Takribani asilimia 70 ya mafuta ya kula yanayohitajika kutumiwa hapa nchini huagizwa kutoka nje ya nchi, maana mafuta yanayozalishwa na viwanda vyetu hayatoshelezi kabisa."

Mheshimiwa Naibu Spika, si hivyo, tarehe 4 Septemba 2018 bado kauli hii imeonyesha kabisa kwamba bado hatujajitosheleza katika kuzalisha mafuta ambayo yanatosha kutumiwa na watu wetu. Hivyo Mheshimiwa Waziri Mkuu alinukuliwa naye pia akisema kauli ambayo inafanana nahiyo nami nitamnukuu kwa kifupi sana, anasema: "*Hivi sasa nchi yetu inatumia takribani dola za kimarekani milioni mia mbili tisini na nne kila mwaka kuagiza mafuta nje ya nchi.*"

Mheshimiwa Naibu Spika, tafsiri ya hali hii inaonyesha kwamba pamoja na kuwa na janga la *corona* ambalo limeikumba dunia na limelikumba dunia na limezikumba baadhi ya nchi bado inaonyesha changamoto hii imekuwa ikijirudia mwaka hadi mwaka, nini kifanyike na ushauri ambao naona nishauri Serikali yangu. Naona kwamba ni vema zaidi ikajielekeza kwenye kilimo cha mazao ya mbegu, kama karanga, zao la chikichi ambalo kwa kweli nimshukuru sana

Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuwa akionesha jitihada kubwa, amefika Kigoma katika kulishughulikia zao hili la chikichi. Itoshe tu kusema kwamba zao hili la chikichi linaonesha katika takwimu za kidunia kwamba ndilo ambalo limeziwezesha nchi zingine kamaNchi za Malaysia kuweza ku-supplykwetu mafuta haya ya kula na hata kusambaza duniani kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna faida kadhaa tukijielekeza katika kilimo cha mazao yanayotokana na mbegu. Faida ya kwanza ni jambo la uhakika ambalo soko letu la ndani tutaweza kulihudumia kwa kujitosheleza na hatimaye tutaepuka kuagiza mafuta haya ya mchikichi. La zaidi sana, itakuwa ni ishara tosha ya kwenda kutekeleza ndoto madhubuti ambayo ya kutibu aliyonayo Mheshimiwa Rais ya kuweza kuzalisha ajira milioni nane alizozisema katika llani ya Uchaguzi kwenye ukurasa wa tano.

Vile vile tukifanya hivyo kuwekeza katika mazao haya, itakuwa ni ishara tosha kabisa kwamba tutaifanya nchi yetu kuweza *ku-export* zaidi mafuta na hatimaye kutoka kwenye kundi lakuwa *importation country* na hiyo hiyo itatuwezesha hata kuimarisha shilingi yetu na hali ya shilingi yetu itakuwa imara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie kauli ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa katika hotuba yake ya Novemba 13, amesema kabisa: "Kwa haya machache ninaona ni vyema zaidi Wizara husika ikachukua hatua madhubuti na kujielekeza katika mazao haya ya mbegu ili tuweze kuepukana na changamoto hii ya mafuta ambayo inajitokeza mwaka hadi mwaka". Kwa nchi nilizositaja kama Malaysia na Indonesia lakini nchi kama Malaysia walichukua mbegu kwetu Kigoma katika Kata ya Simbo na wakapeleka kwao kwa ajili ya kuzalisha mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona kengele imelia, nilikuwa na mengi ya kuchangia ila mchango wangu nitauleta kwa maandishi ili Serikali waweze kuona mawazo yangu juu ya hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mheshimiwa Keneth Nollo na Mheshimiwa Ng'wasi Kamani ajiandae.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kabla sijachangia nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa nguvu na uhai kuwepo katika Bunge hili. Kipekee, niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa ambao wameniamini tena kwa mara nyingine na kunipa kura nyingi za kishindo ambazo zimenirudisha katika jengo hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikichangia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais, kwa kweli niseme ukisikia na ukisoma vizuri kwenye hotuba hii, hotuba hii imejaa matumaini na neema kubwa sana kwa Watanzania. Mimi nachosema wasaidizi wake ambao Mheshimiwa Rais amewaamini, niombe wachukue hatua ambazo zitaibeba hotuba hii na kuifanya kazi. Kwa nini nasema hivyo? Mara nyingi wakati mwingine viongozi wetu wanaongea mambo mazuri na makubwa lakini yanaishia kwenye vitabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwanza niongelee upande wa kilimo, tunaongelea Tanzania ya viwanda. Wazalishaji wakubwa wako vijijini, lazima tuwekeze nguvu kubwa kwa wakulima wa hali ya chini na ili tuweze kufanikiwa lazima tuandae miundombinu mizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wamekuwa wakichangia kuhusu *TARURA*, ni ukweli usiopingika kuwa mtandao wa barabara nyingi sana uko kule kwa wananchi wa hali ya chini na ndiyo wazalishaji wakubwa. Mimi nashindwa kuelewa, kwa nini hili jambo tumeshauri muda mrefu toka Bunge liliopita lakini bado halijatatuliwa naomba

Serikali ilione hili jambo ni la muhimu. Tunaongelea Tanzania ya viwanda, hatuwezi tukafanikiwa kwenye viwanda vyetu kama hatutaboresha miundombinu mizuri kwa wananchi wetu wa hali ya chini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwa mfano kule vijijini, mimi niongelee kwa mfano Kyerwa, barabara hali ni mbaya lakini haohao ndiyo wazalishaji wakubwa. Ukienda kwa Mkoa wa Kagera, ndizi zinazotoka Kagera ndizo zinalisha nusu ya Tanzania. Tusipoboresha mazingira haya yawe mazuri huyu mkulima akawenza kusafirisha mazao yake vizuri, hatutaweza kufanikiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini siyo hilo tu; malighafi nydingi tunategemea zitoke kwa hawa wananchi wa hali ya chini. Tusipoboresha haya mazingira mazuri, tukaweka miundombinu mizuri, tutashlia kuchukua malighafi kule nje kuwanufaisha watu wa nje badala ya kutumia malighafi ambazo zinazalishwa hapa kwetu

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe sana Mawaziri ambao wanahuksika suala la *TARURA* walitilie mkazo.niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, suala hili ni kwa faida yetu sote. Tuombe sana Wizara inayohusika na *TARURA* itengewe pesa, kama haitatengewa pesa sisi ndiyo tunaopitisha bajeti, haiwezekani tukae tunazungumza mambo hayafanyiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, nimekuwa nikishangaa, ukienda kwenye vyuo vyetu, kwa mfano kile Chuo cha *NIT*, tuna wataalam ambao wanaweza wakatengenezwa pale kusimamia miradi yetu mikubwa. Leo hii tunao Mradi wa *SGR*, mradi huu unajengwa na watu kutoka nje lakini Serikali imejipanga vipi kuandaa wataalam ili hawa waliojenga huu mradi wakishaondoka tupate wataalam wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiwasikiliza wale watu wa *NIT* wanakwambia mtaalam mmoja kwenda kusoma nje anatumia zaidi ya milioni 200, lakini wao kumuandaa

mtaalam huyohuyo wanatumia milioni 25, lakini unakuta chuo hichohicho Serikali bado hajjawekeza nguvu. Sasa hili na lenyewe lazima tuliangalie, vinginevyo hii miradi mwisho wa siku itakosa wataalam wetu wa kusimamia. Jambo ambalo unalismamia wewe mwenyewe hata kama mradi ni wako unakuwa na ule uzalendo. Haya masuala ya miradi kusimamiwa na watu wengine, tunakwenda kutafuta wataalam nje, hili jambo halijakaa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais kwenye hotuba yake amezungumzia miradi mingi ya maji. Kwa kweli tuseme ule ukweli, miradi mingi ya maji bado hajjafanikiwa. Unakuta hapa wamedonoa kidogo, hapa wamegusa kidogo. Niombe sana Serikali tusianze kufanya usanifu miradi mipyä, tukamilishe ile miradi ya zamani ndiyo tuanze na mingine. Hili suala la kushika hapa kidogo tuonekana tuna miradi mingi ambayo haina manufaa hatutaweza kufika mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano Kyerwa tuna mradi wa maji wa vijji hamsini na zaidi, mradi huu ukikamilika naamini utanufaisha wananchi zaidi ya laki mbili. Kwa hiyo, niombe sana Serikali, tunapoanzisha miradi hasa hii ya maji basi ikamilike kuliko tunagusa kidogo, Serikali inaonekana tuna miradi mingi sana lakini mwisho wa siku hatuikamilishi. Kwa hiyo, niombe hili na lenyewe tuliangalie. Tutakapokuwa tumehakikisha hawa wananchi wetu wamepata maji, nina uhakika hata uzalishaji utakuwa mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho napenda kukiongelea ni barabara zetu kuu, kwa kweli ni jambo ambalo linasikitisha. Ukienda kwa mfano mpakani kwetu na Uganda ni aibu. Kule kwetu unaweza ukafikiri ni uchochoro kule kwao ni Ulaya. Hizi barabara ambazo zinaunganisha nchi na nchi niombe sana tuweze kuzikamilisha ili na sisi tuonekane ni sehemu ya Watanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kenneth Nollo, atafuatiwa na Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, Mheshimiwa Deo Sanga ajiandae.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwani hii ni mara yangu ya kwanza kuchangia katika Bunge hili Tukufu. Vilevile niwashukuru zaidi Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM Wilaya ya Bahi na niwashukuru wananchi wa Bahi kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais inaonesha dira ya namna gani taifa letu linapotaka kwenda. Tumeshuhudia nchi yetu imefanya uwekezaji katika sekta mbalimbali. Serikali imewekeza kwenye afya, elimu na sasa inawekeza kwenye miundombinu ya reli na umeme, ni mabilioni ya shillingi yanatumika katika uwekezaji. Katika nchi yetu takribani asilimia 75 ya wananchi wetu wako kwenye kilimo, kwa maana hiyo unavyowezesha afya, elimu, ni ili uwe na *productive force* ambayo itaweba sasa ku-*engage* kwenye uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunafahamu kilimo kwa maana ya uhai wa taifa lakini kilimo tangu historia ndiyo habari ya *national security*. Serikali nyingi duniani zimeangushwa kwa sababu ya kulegalega na kukosa chakula. Sote tunafahamu historia ya mkate ulivyoangusha utawala pale Ufaransa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuchangia hivi na hili nasisitiza siyo kwamba tulete wawekezaji kwenye kilimo, tunataka Serikali iwekeze kwenye kilimo. Maana yangu ni kwamba tumekuwa na Benki ya Kilimo lakini bado haijawasaidia wakulima. Mchango mwingu wa wenzangu waliopita wamechangia kwamba tunaagiza kwa kiasi kikubwa ngano, mafuta lakini hata sukari yenyewe bado hatujakaa sawasawa kuhimili utoshelevu katika taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilo moja ya korosho mkulima anaiuza kwa dola moja, lakini kilo moja hiyo hiyo

ikishakuwa *processed* inakwenda kuuzwa kwa dola 20. Ireland walianza na *model* inaitwa *vertical forward integration* kwamba mkulima wa alizeti atapeleka alizeti kwenye kiwanda cha kukamulia mafuta kwa huduma ya kukamuliwa mafuta, siyo kwenda kuuza alizeti yake. Ikishatoka pale sasa ile alizeti inakwenda katika mlolongo wa kwenda kuuzwa na hela ile mkulima ndiyo anaipata. Pamoja na hilo, kwenye kiwanda kile mkulima anapata hata mashudu. Kwa hiyo, ni vyema Serikali ikawekeza hasahaha kwenye ushirika, kwamba kama tunaitumia Benki ya Kilimo tuweze kuwa-*empower*watu wetu kwa kuanzisha vyama vya ushirika ambavyo vitakuwa na mashine za kufanya *processing*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, suala la ngano; tunatumia takribani shilingi milioni 300 kwa mwaka, hivyo hivyo kwenye mafuta. Kwa hiyo, bado soko la ndani ni kubwa kwa hiyo ni vyema sasa Serikali iwekeze yenye si kuleta wawekezaji kwenye kilimo. Bado tuna nafasi ya sisi wenyewe kuwekeza kama Serikali ili tupate utoshelevu wa bidhaa hizi ambazo tunaagiza kwa kiasi kikubwa kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, *total importation* ya chakula katika Bara la Afrika ilikuwa ni dola bilioni na zaidi kwa mwaka kwa takwimu za mwaka 2018. Maana yake nini? Maana yake ni kwamba hata soko la Afrika bado ni kubwa kwa sisi Watanzania tukaweza ku-*export*. Tumeshuhudia tani na tani za mchele zinapita hapa kwenda Kongo, mchele kutoka Asia unapita kwenye nchi yetu kwenda Kongo. Kongo wame-*import* mchele kwa thamani ya dola milioni 65 lakini fedha hizi za Wakongoman zilitoka hapa na kwenda katika Bara la Asia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize kwenye *export*. Nchi ya Vietnam ni ndogo kwelikweli katika Bara la Asia, ni nchi ya tatu duniani lakini kwa ujumla wake ina-*export* mchele kuliko Bara la Afrika, yaani chukua nchi zote za Bara la Afrika, ziunganishe, hazifikii kiwango cha Vietnam inacho-*export*. Vietnam ina-*export* kiasi cha *1.4 billion dollars* kwa mwaka; hizo ni takwimu za mwaka 2019 lakini kwa *combination* ya Afrika hawaifiki Vietnam, Vietnam ni nchi ndogo sana.

Niliwahi kwenda Hanoi, ukitoka kidogo kama hapa ukienda *Area C* tayari kuna majeruba ya mpunga. Kwa hiyo, wenyewe mpunga *is everywhere* lakini kama navyosema, ni aibu kwa Bara zima la Afrika kwamba tunashindwa na nchi kama Vietnam.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kilimo cha mpunga kwenye Jimbo langu la Bahi. Bahi tuliwahi kujengewa skimu na FAO na IFAD. FAO walitujengea skimu mwaka 1997; hakujawahi kufanyika tena ukarabati tangu kipindi hicho. IFAD walitujengea skimu mwaka 2004, mvua ya kwanza ilikuja ikavunja tuta, hakujawahi kufanyika tena *repair* na kilimo hakiendelei katika skimu ile ya Mtita.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu Bodi ya Mikopo. Nataka tubadilishe *model* ya kuwafadhili vijana wetu. Vijana wetu tukiwapa hela, hela ile hawawezi kuitunza, ndani ya wiki mbili, tatu wameshazimaliza na hela zinavyotoka wengi wanajaa mjini huku kwa ajili ya kugonga bia. Sasa kwa nini tusiwe na mfumo, kwa mfano nchi ya Japan, anakuwa na kadi ya kwenda ku-*swipe* kwenye chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itarahisisha *ku-manage economy*, hasa vijana wetu wasiweze kushinda njaa kwenye vyuo vikuu. Badala ya kuwapa hela washike sasa tufanye utaratibu wa ku-*swipe* katika huduma mbalimbali, iwe kwenye chakula, *hostel*, hii itarahisisha vijana wetu wasome, hata *book allowance* siku hizi kuna vitabu *electronic*, wataweza ku-*swipe* na kununua vitabu. Suala hili litatusaidia kwanza Watanzania wengi wapata mkopo lakini vilevile itasaidia zaidi vijana wetu waweze kusoma kwa uhakika.

Mheshimiwa Niabu Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

Waheshimiwa Wabunge, mchango wa muhimu sana huo, pengine tutafikia mahali na sisi Wabunge tuwe tuna-*swipe* maana kuna Wabunge nao wanamaliza zote halafu humu ndani zinaanza naomba elfu tano kidogo *canteen* na mambo kama hayo.

Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Sanga, Mheshimiwa Stella Fiyao ajiandae.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Kwanza kabisa, nianze kwa kumrudishia shukrani Mwenyezi Mungu, Muumba wa Mbingu na Nchi kwa kutupa kibali wote kuwa hapa jioni hii ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa nafasi ya kipekee kabisa niwashukuru vijana wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuititia katika Baraza la Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi kwa imani kubwa walijonipa ya kuwawakilisha katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa aliyokwishafanya katika nchi yetu kwa miaka mitano iliyopita. Hotuba aliyoitoa katika Bunge hili Novemba, 2020 inatia matumaini makubwa sana kwetu sisi Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ajira limekuwa changamoto kubwa sana kwetu sisi vijana. Mimi kama mwakilishi wa vijana naomba kuungana na Wabunge wenzangu kulichangia suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ajira ni mtambuka na linahitaji juhudzi za pamoja za Serikali, sekta binafsi, wadau wa maendeleo na sisi vijana wenywewe. Pamoja na hayo, jukumu la msingi bado linabaki kwa Serikali kuhakikisha inawezesha sekta binafsi ili kuzalisha ajira nydingi zaidi nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonesha kwamba kuna sababu kuu nne zinazochangia pakubwa sana katika tatizo la ajira katika nchi hii. Naomba nizitaje na zitakuwa pointi zangu za msingi jioni ya leo. Kwanza, ni mifumo ya elimu ambayo ujuzi wake hauendani na mahitaji ya ajira; la pili ni vijana kutokuwa na taarifa na takwimu za fursa za

biashara na ujasiriamali zinazowazunguka; ya tatu ni sera za vijana na uwezo mdogo wa kiteknolojia; ya nne ni Serikali kutowekeza vya kutosha kwenye sekta binafsi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala zima la mifumo ya elimu ambayo ujuzi wake hauendani na mahitaji ya ajira, kwanza kabisa, nianze kwa kuipongeza Wizara ya Elimu kwa kuendelea kuboresha vyuo vya ufundi katika sehemu mbalimbali. Pia nizidi kuwapongeza kwa kutupa ule mfumo *wa competence-based system of education* ambapo lengo lake kubwa ni kuwawezesha watoto na vijana wanaosoma kupata ujuzi wa msingi wa maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini changamoto kubwa ya mfumo huu ni kwamba walimu ambao wanatakiwa kufundisha vijana wetu bado hata wao hawajaelewa mfumo huu. Utafiti uliofanywa na wanazuoni wa Chuo cha Sokoine unaonesha kwamba asilimia 86 ya walimu bado hawajaelewa dhima kuu ya mfumo huu na asilimia kama 78 ya *lesson plans* wanazotumia kufundisha haziendani na mfumo huu wa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuendelea na utaratibu huu kutatufanya tuwe na vijana ambao hawana stadi za kutosha na hawa wakiingia katika soko la ajira, itaongeza changamoto. Ushauri wangu kwa Wizara ya Elimu tuandae utaratibu ambao Walimu na Wakufunzi wataelekezwa upya ili waelewe namna mfumo huu unavyofanya kazi, kwa sababu mfumo huu una faida kubwa ili wao waweze kufundisha vijana wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niungane na Wabunge wengine walioweka msisitizo katika suala zima la elimu ya stadi ya ujuzi ambayo itaendana na mfumo wa sayansi na teknolojia. Katika hili niishauri Wizara ya Elimu ione utaratibu ambao elimu ya usimamizi wa fedha inaweza ikaanza kufundishwa katika shule zetu kuanzia ngazi ya chini kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni changamoto sana kama vijana hawa ambao wanatoka mashulenii wanakuja,

tunawakabidhi fedha na mikopo mbalimbali kutoka kwenye Halmashauri zetu na Serikali lakini hawana elimu ya usimamizi wa fedha. Kwa hiyo, kama tulivyolifanya somo la historia ili kukuza uzalendo, vivyo hivyo somo la usimamizi wa fedha lianze kufundishwa katika shule zetu kuanzia ngazi ya chini kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala zima la vijana kutokuwa na taarifa na takwimu ya fursa za biashara na ujasiriamali zinazowazunguka, ningependa katika suala hili niongelee mikopo ya Halmashauri, almaarufu 4,4,2 na mifuko mbalimbali ya uwezeshaji wa vijana katika Wizara zetu. Tunaishukuru sana Serikali kwa kuanzisha utaratibu huu na kweli unasaidia vijana, lakini bado kuna changamoto katika utoaji na ufanisi wa mikopo hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, kuna baadhi ya halmashauri ambazo zinakuwa na mapato makubwa kuliko nyingine. Hivyo vijana ambaao wako katika halmashauri zisizo na mapato, wanakuwa na shida kidogo. Tungeangalia utaratibu wa kuweza ku-centralize mfumo huu au Mfuko huu ili vijana wote tuweze kunufaika sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba tuangalie utaratibu wa kuweza kupunguza idadi ya watu katika kundi la watu ambaao wanaweza kuwa *eligible* kwa ajili ya kupata mikopo hii. Kundi la watu 10 ni changamoto kidogo. Tuangalie kupunguza *list*, wawe watano mpaka watatu ili tuweze kupata ufanisi zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala zima la Mifuko ya Uwezeshaji katika Wizara mbalimbali; kwanza nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais, katika hotuba yake ya ufunguzi wa Bunge hili alisisitiza kwamba Mifuko hii iongezewe ufanisi. Mifuko hii ina changamoto kuu tatu; kwanza, mara nyingi haina fedha; na ile yenye fedha huwa mara nyingi ina urasimu mkubwa katika upatikanaji wa fedha zake; na tatu, vijana wengi hawana taarifa ya namna gani fedha hizi wanazipata. Hivyo, nadhani ni jukumu la moja kwa moja la Serikali kuhakikisha kwamba vijana wanapata taarifa zilizo sahihi za

fedha hizi na namna gani wanaweza kuzipata fedha hizi.  
*(Makofii)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanza, nimeamua kuanzisha Kongamano la Vijana na Maendeleo kwa vijana wote nchi nzima, litakalofanyika mwaka huu mwezi wa Saba na litakuwa endelevu kwa kila mwaka, ambapo nitaalika Wizara zote na Taasisi zote za uwezeshejji wa vijana ndani na nje ya nchi, ili tukutane na vijana hao na kuwapa elimu juu ya Mifuko hii na fursa zilizopo. *(Makofii)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nawaomba Waheshimiwa Wabunge, pale nitakapokuja kuwaomba ku-*support* mfumo huu, naomba muwe wepesi ku-*support* kwa sababu vijana hawa amba ni asilimia 61.9 wa nchi hii ndio waliokuwa wapiga kura wenu na tuna jukumu la moja kwa moja kuhakikisha tunawasaidia kuwanyanya kiuchumi. *(Makofii)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la Sera ya Vijana na uwezo mdogo wa kiteknolojia; namshukuru sana Mheshimiwa Rais na sera yake ya Serikali ya Viwanda. Hii imetusaidia sana katika kuzalisha ajira nyingi. Katika Hotuba yake Mheshimiwa Rais ameweka wazi, viwanda vidogo vidogo kama 8,477 vimeanzishwa kati ya mwaka 2015 mpaka 2020; na jumla ya ajira kama 480,000 zimezalishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi hii bado ni ndogo. Naomba kushukuru sana Wizara ya Kazi na Vijana chini ya Mheshimiwa Jenista, imeanzisha Mfumo wa *Green House* ambapo itaweka *green house* hizi katika Halmashauri mbalimbali...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na mengi ya kusema, lakini naamini mengine nitayawasilisha kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho wa yote, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Naona makofi hayo yanakutia moyo kabisa.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Deo Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Stella Fiyao na Mheshimiwa Priscus Tarimo ajiandae.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi nami niwe mionganoni mwa wachangiaji. Katika kuchangia kwanza nianze kwa kuunga mkono hotuba zote mbili; wakati wa kufunga Bunge na wakati wa Ufunguzi wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Bunge linaahirishwa au likihitimishwa, ndiyo kazi kubwa iliyofanywa na Serikali ya CCM chini ya Mheshimiwa Dkt. Magufuli, jemadari na ndiyo iliyofanya Wabunge wengi turudi hapa ndani, kazi hii! (*Makof*)

Katika ufunguzi, mwelekeo huu wa miaka mitano, naomba nichangie na nianze na elimu. Tunapozungumzia elimu bila malipo na ndiyo imefanya watoto wetu wengi wapatikane katika maeneo yetu, ambapo wazazi wao walikuwa hawawezi kuwapeleka shule. Elimu bila malipo kwenye sekondari tunasema, msingi na sekondari, ombi langu kwa bajeti inayokuja na Rais wetu mpendwa, isiwe elimu bila malipo kidato cha kwanza mpaka cha Nne. Inatupa taabu hata sisi Wabunge kule Majimboni wakati fulani kusema. Tunaomba iwe mpaka kidato cha sita yaani kuanzia kiadto cha kwanza mpaka cha sita. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunadhani hili linaweza kuwa ni zuri. Tunamwomba Waziri mwenye dhamana katika bajeti ambayo inakuja, hebu tujipange vizuri, tuishauri Serikali kupitia Rais wetu kwamba elimu bila malipo iendelee mpaka mpaka kidato cha Sita, yaani cha Kwanza mpaka cha Sita. Tutakuwa tumekwenda vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wamechangia hapa juu ya mikopo, nilikuwa nafuatilia jana. Kwenye mikopo hii kuna baadhi ya watu ambao watoto wetu hawa wanafadhiliwa na taasisi mbalimbali na baadhi ya watu. Inapofika mahali yule mtu aidha ameshindwa kuendelea kumfadhlili na kadhalika; unakuta mtoto amefaulu vizuri Kidato cha Sita na kuendelea anashindwa mkopo na baadaye anakuwa hana mahali pa kwenda kwa sababu wafadhili wake wameshindwa na kadhalika. Nami nina mifano hai mingi, watu mbalimbali na wananchi wanavyokuja kwangu, najua hii iko pia kwa Wabunge wenzangu. Ombi langu, jamani wapewe bila masharti, bila kujua amesoma wapi na kadhalika. Maadamu ana vigezo vya kupata mkopo, apewe bila masharti ya aina yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye suala la umeme, ndugu zangu Waziri mhusika yuko hapa, Mheshimiwa Kalemani. Unajua penye kazi nzuri ambayo mtu amefanya lazima tumpongeze. Amefanya kazi nzuri sana. Ombi langu sasa kwenye jimbo langu, najua na kwa wenzangu, asubuhi tumetoka kuongea, Kijiji cha Mutanga kule, walianza kupeleka nguzo, lakini wamesimama. Ombi kwa Mheshimiwa Waziri, wananchi hawa wapewe umeme wa kule Mtanga na Ingangidung, utakuwa umetusaidia na baadhi ya maeneo, nitawasiliana na Waheshimiwa Madiwani, baadhi ya vitongoji ambavyo leo amezungumzia kwamba ni lazima na vyenyewe sasa tulete ili waweze kupata umeme. Kwa hiyo, nitawasiliana na Madiwani, mwishoni mwa wiki hii nitamkukabidhi maeneo ambayo bado hayajapata umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye afya, kazi iliyofanyika ni nzuri sana ya kujenga vituo, zahanati na kadhalika. Ombi langu, kwenye Jimbo langu la Makambako wananchi wanaonipenda sana, nami nawapenda sana kwa dhati kabisa kabisa; na Rais wao wanampenda sana; ombi langu tumekuwa tukizungumzia habari ya *X-Ray* na *Ultrasound*. Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana yuko hapa, hivi kweli Mji wa Makambako ambako ndiyo *corridor* ya kwenda Songea, Mbeya na wapi, ndiyo Jiji kubwa, hivi

hatuna *X-Ray*. Chumba cha *X-Ray* tulishakijenga, kipo tayari. Tunaomba katika bajeti tunayokwenda nayo tupate *X-Ray*, Mheshimiwa Waziri atakuwa ametutendea haki katika Mji wetu wa Makambako.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji; Mheshimiwa Aweso yuko hapa, ambaye ni Waziri wa Maji. Naomba ndugu yangu Waziri; Mawaziri wote wanafanya kazi nzuri, wanaendana na kasi ya mwenyewe, wote! Sasa Mji wa Makambako ndiyo mji mkubwa katika mijii yote kwa ukanda. Ndiyo *corridor* pale jamani; kwenda wapi na wapi kama nilivyosema. Ule mradi mkubwa ambao tunapata mkopo nafuu kutoka Serikali ya India, ni vizuri sasa katika Miji 26 ile na Mji wa Makambako upo, Mheshimiwa Waziri atakapokuwa amesimama hapa atuambie ni lini mradi huo wa maji Makambako utaanza ili nikawaambie wananchi wangu wa Makambako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba leo asubuhi Mheshimiwa Waziri amenijibu kuhusu maji, sasa aseme hapa kwamba maji hayo ni ya mwakani au ni ya mwaka huu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara, naishukuru Serikali kwa Mji wangu wa Makambako, tumepata fedha za lami kilometra 3.5 Mjini pale, tunaishukuru sana Serikali. Hata hivyo, wenzangu wameongelea chombo cha *TARURA*. Naomba kwenye bajeti hii tutakayoanza, naomba tuongezewe fedha ili barabara zetu ziweze kupitika msimu wote. Kwa hiyo, naomba sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu hapa kuna maboma mbalimbali ambayo yamejengwa; madarasa, zahanati na kadhalika. Ombi langu, Wizara hasa TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo, ahakikishe maboma haya ambayo wananchi wamejenga pamoja na Waheshimiwa Madiwani pamoja na Wabunge tulimo humu ndani, yanaisha kwa kipindi hiki.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, siyo kwa umuhimu...

**NAIBU SPIKA:** Muda umekwisha Mheshimiwa. Kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, dakika moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wameongelea hapa juu ya Rais wetu kumwongezea aidha muda. Kuna watu wengine ni kama dhambi hivi kumwongezea. Ndugu zangu, mtu huyu amefanya kazi kubwa kwa miaka mitano iliyoisha na mipango ya miaka hii mitano, ombi langu hapa ndani, atake asitake tumwongezee muda ili aweze kufanya kazi na kukamilisha mipango yake vizuri katika nchi hii. Kabisa! Ili aweze kufanya kazi yake vizuri ili mipango aliyolpanga iweze kukamilika. Atake asitake, tumlazimishe! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu, nilisema hapa kama mnakumbuka kipindi fulani kwamba China wamefanya hivyo na mahali pengine wamefanya hivyo, siyo dhambi kwa mtu anayefanya vizuri. Hata ninyi Wabunge mlorudi maana yake mlifanya vizuri, ndiyo maana watu walisema tena mrudi, kwa hiyo, siyo dhambi tena kumwongezea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani msimamo wa Mheshimiwa Rais wote tunaufahamu, lakini Mbunge hazuiliwi kuzungumza kile anachoona kwamba naye anatoa mchango. (*Makofi*)

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Stella Fiyao, atachangia kwa dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Priscus Tarimo na Mheshimiwa Joseph Kakunda ajiandae.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Jambo la kwanza,

nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniba neema na kibali cha kuwepo katika Bunge hili la Kumi na Mbili. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, naishukuru familia yangu ambayo imekuwa bega kwa bega na mimi mpaka hatua ya mwisho hata kuipata hii nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende moja kwa moja kwenye kuchangia suala la hotuba ya Mheshimiwa Rais kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kilimo kwenye Taifa hili limekuwa ni muhimu sana na linahitaji kuchukuliwa kwa uzito wa hali ya juu sana. Endapo suala hili litachukuliwa kwa uzito huo itapelekea kutokutoa shilingi trillioni 1.3 kila mwaka kwa ajilli ya kwenda kuagiza chakula nje ya nchi na fedha hili tuielekeze moja kwa moja kwenye pembejeo za kilimo ili wakulima waweze kupata pembejeo kwa bei ndogo na waweze kulima na kupata mazao ya kutosha ikiwa ni sambamba na kuwatafutia soko la mazao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kwamba suala la kilimo limebeba ajira nydingi sana za vijana ndani ya Taifa letu na endapo totalichukulia kipaumbele, tutapunguza changamoto kubwa ya vijana wetu kukosa ajira ndani ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni la wafanyabiashara ndani ya Taifa letu la Tanzania. Suala hili limekuwa changamoto kubwa kwa wafanyabiashara. *Issue* ya kodi imekuwa ni changamoto kubwa sana ambayo inapelekea wafanyabiashara wengi ndani ya Taifa kukimbia na kwenda kuwekeza katika mataifa mengine kwa sababu ya kukwepa kodi kubwa ambazo wameendelea kuzipata ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba kuna umuhimuwa kupitia upya Sheria za Kodi kwa wafanyabiashara, kwa sababu kodi hizi zimekuwa ni

kandamizi. Huu utaratibu wa *TRA* kuwakadiria kodi wafanyabiashara, unapaswa kupitiwa kwa upya. Wafanyabiashara wamekuwa wakikadiria kodi kubwa na wakati mwingine zinazozidi mitaji yao na hivyo kupelekeakukimbia kuwekeza ndani ya Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Mheshimiwa Rais amesema wazi kabisa kwamba anahitaji kodi ziwe rafiki kwa wafanyabiashara, kuna umuhimu mkubwa wa kulichukulia jambo hili kwa uzito ili wafanyabiashara wengi na wa kutoka mataifa mengi waweze kuwekeza ndani ya Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho kabisa, pamoja na kwamba Mheshimiwa Rais ameipongeza Tume ya Uchaguzi kwa kusimamia uchaguzi, lakini ni suala lisilopingika kabisa na ni suala la wazi kabisa kwamba uchaguzi ulikuwa na dosari nyingi. Kutoka hatua ya kwanza kabisa ya zoezi la uchukuaji wa fomu, zoezi la urudishwaji lligubigwa na mambo mengi ya ovyo kabisa. Katika hatua ya kwanza ya uchukuaji wa fomu, wagombea wengi kutoka Vyama vya Upinzani walikamatwa na kupewa kesi mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, siku zilivyokaribia za urudishaji wa fomu, hata wale waliokuwa wamebahatika kuchukua fomu, walikamatwa na kupewa kesi, hawakupata kabisa ile nafasi ya kurudisha fomu. Pamoja na hilo, hata wale ambao walipata nafasi ya kurudisha fomu, siku chache baadaye walikamatwa na kupewa kesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kabisa, hatuwezi kusema uchaguzi ulikuwa wa huru na haki. Pamoja na hilo, hata tu mara baada ya uchaguzi wananchi walijitokeza kwenda kupiga kura. Watu walipiga kura kwa kujitoa na wengine walikuwa ni wazee, wengine walikuwa ni wanawake wajawazito, lakini watu walivamiwa kwenye vituo vya kupigia kura. Wengine walipigwa, wengine

waliumizwa na wengine wameachiwa majeraha mpaka sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, hata mara tu baada ya wananchi kupiga kura, wagombea walitangazwa kabla ya majumuisho. Ni kitu ambacho kinaumiza sana.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, wakati natafuta amekaa wapi huyo mtoa taarifa, kengele imeshagonga.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa muda wako umekwisha. Ahsante.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Priscus Tarimo, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kakunda na Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo ajiandae.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Priscus Tarimo, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kakunda, Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo ajiandae.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Nisikitike tu kwamba nilikuwa nimejijandaa kuongea dakika 10 na sasa tumeambiwa ni tano tano, nitajaribu kwenda kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa nafasi hii adhimu ya kuwatumikia Watanzania katika chombo hiki kitukufu cha Bunge.

Nikishukuru chama changu cha Mapinduzi lakini zaidi niwashukuru wazazi wangu baba na mama Tarimo pamoja na familia yangu, mke wangu Eveline na watoto wangu watatu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaenda mbali niseme tu kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia 100. Nasema hivyo nikiwa nimechukua *reference* ya kwanza kwenye hotuba ile ya Bunge la Kumi na Moja ambayo aliitoa Mheshimiwa Rais hapa na baadaye yale aliyoyafanya kwa miaka mitano ambayo yalisababisha sasa Watanzania kutuelewa na tukapata ushindi wa kishindo kwa mwaka huu wa 2021 kwa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Rais yako mambo mengi ambayo nataka nilyaongelee. Nianze na maslahi ya watumishi wa umma kama yalivyo kwenye ukurasa wa 8 na wa 9 wa hotuba ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba watumishi wa umma wamekuwa na malalamiko ya muda mrefu haswa walimu. Wanalamakia madeni yao ya muda mrefu, kupandishwa kwa madaraja pamoja na mfumo mpya huu ambao umeshakuja lakini hata wastaa fu wamekuwa na malalamiko ya kucheleweshewa mafao yao. Naomba Serikali iliangalie suala hili vizuri na kwa sababu liko kwenye hotuba hii basi liweze kushughulikiwa kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee mikopo ya halmashauri hasa ile asilimia 10 kwa ajili ya akina mama, vijana na walemvu. Niishukuru na kuipongeza Serikali kwa kuamua kuibadilisha sheria ile na kuzifanya fedha zile sasa ni *revolving* kwa maana ya kwamba fedha zinazokopeshwa sasa zinaweza zikawekwa kwenye mfuko amba ni *revolving fund* na kukopeshwa kwa vijana na akina mama wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo mawili ya kuishauri Serikali kuhusiana na mikopo hii. Wangalie uwezekano wa kukopeshwa fedha hizi kwa mtu mmoja mmoja na kwa sababu sasa tuna mfumo mzuri kwa kupitia

vitambulisho vya *NIDA*, hata kama ikibidi kuwakopesha vifaa kama bodaboda ili basi ilete tija zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni katika ile sheria iliyobadilishwa na kusema kuwe na mradi wa pamoja. Nakubaliana kabisa na mawazo ya Serikali lakini nishauri pia kukopeshwa kikundi ili wakopeshane kama zamani iendelee kuruhusiwa kwa sababu iliwajenga akina mama wengi katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la viwanda limeelezewa vizuri na nimshukuru Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali yake kwa kutuwekea kiwanda kiwanda kikubwa sana pale Moshi mjini lakini bado nina ombi kwa Serikali. Viko viwanda vilivyobinafsishwa ili viendelezwе vitoe ajira na kodi mfano ni kiwnada cha viberiti cha *Kibo Match* na kiwanda cha magunia. Katika hotuba ya Mheshimiwa Rais ya Bunge la Kumi na Moja, ukurasa wa 21, alielezea dhamira yake ya kuwanyang'anya viwanda wale walioshindwa kukidhi vigezo vile. Moshi tuko tayari, tunaomba aje awanyang'anye wale waliofanya viwanda vile ni mago-down.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye ukurasa wa 95 kuna marekebisho ya viwanja vya ndege 11. Naomba niikumbushe Serikali kiwanja cha ndege cha Moshi nacho kimetajwa lakini kinahitaji matengenezo ya haraka. Kiwanja hiki kina umuhimu mkubwa sana, kitabibu, kibashara na kiutalii. Naomba kipewe kipaumbele katika viwanja vya ndege vinavyorekebishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 32 umeongelea masuala ya afya na niipongeze Serikali kwa hatua kubwa ya kujenga zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya pamoja na za mikoa na za rufaa zile za kanda. Nawaomba katika hizi 98 zinazotarajiwa kujengwa katika awamu hii tafadhali sana wawakumbuke wananchi wa Moshi Mjini na Vijijini, pote pale hakuna hospitali ya wilaya ya Serikali, tunaomba sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la elimu nililizungumzia jana kwenye swali langu na limezungumziwa sana. Hoja

yangu kubwa itajikita kwenye mikopo kama nilivyosema na niendelee kusisitiza, wapo watu wanaokidhi vigezo vyote lakini hawapati mikopo ile pengine kwa sababu walismeshwa kwa ufadhilli kwenye shule za binafsi au kwa sababu nyingine zozote. Kama Mawaziri watahitaji kuniona nitawapa mifano halisi ambayo ipo na naifahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba msisitizo upelekwe kwenye kidato cha tano na cha sita hasa kwenye shule za kata kwenye Taifa hili. Kuna shule ambazo zina nafasi tuweke mkazo zaidi kwenye elimu inayoendelea kwa kujenga madarasa mapema badala ya kujenga mwisho baada ya watoto kumaliza shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 36 wa hotuba ile umeongelea wafanyabiashara wadogo. Niipongeze sana Serikali namna ambavyo imewaweka vizuri na niombe uangalizi uwekwe katika kuwapanga vizuri. Yapo maeneo wamezuia kabisa kutumia miundombinu ambayo imewekwa kama barabara. Halmashauri zinayo nafasi kubwa na sisi tunaendelea kuzishauri lakini tuweke namna bora ya kuwapanga wafanyabiashara hawa wadogo ili basi waweze kushirikiana na watumiaji wengine wa miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 37 Mheshimiwa Rais ameongelea umuhimu wa kuboresha michezo. Mimi naona eneo bora zaidi la kuanzia ni kuboresha viwanja vya michezo ambavyo vinasimamiwa na halmashauri kwenye majimbo mbalimbali. Moshi Mjini tunacho kiwanja cha majengo, naomba Serikali iangalie namna ya kutusaidia na kukiboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumalizia na eneo la watalii ambalo kaka yangu na baba yangu Mheshimiwa Dkt. Kimei ameliongelea lakini pia madereva...

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Kakunda atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo, Mheshimiwa Aloyce Kamamba ajiandae.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Awali ya yote nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba zake mbili nzuri ambazo zilinigusa mimi sana kama Mbunge wa Sikonge. Hotuba hizo mbili zimefanya mapitio ya nchi yetu, tulikotoka, tulipo na tunakoelekeea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili sisi Watanzania tuweze kujuu tumetoka wapi na tunakoelekeea ni wapi, jambo la kwanza kabisa ni kuangalia kwamba nchi yetu hii illitawaliwa na wakoloni kwa muda wa miaka 74 na sisi tangu tujitawale kwa Tanzania Bara huu ni mwaka wa 60 na kwa Zanzibar ni mwaka wa 58. Utaona kwamba kipindi ambacho walikaa wakoloni katika nchi hii ni kirefu kuliko kipindi ambacho sisi tumekuwa huru. Katika kipindi ambacho tumekuwa huru, mambo ya maendeleo yaliyofanyika ni makubwa zaidi kuliko kipindi cha wakoloni. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu tupate uhuru pia tumekuwa na vipindi vikuu vitano vya kiuchumi. Kipindi cha kwanza ni kipindi cha soko huria (1961 – 1967), kipindi cha pili cha uchumi hodhi miaka 18 kuanzia mwaka 1967 – 1985, kipindi cha tatu ni kipindi cha mpito cha marekebisho ya kufufua uchumi cha mwaka 1985 – 1995, kipindi cha nne ni cha mwaka 1995 – 2015 ambacho hicho ndiyo kiliweka *prudent economic reforms* ikiwemo ubinafsishaji, kurejesha

baadhi ya njia ya kiuchumi kwenye sekta binafsi ikiwemo masuala ya ubi ana *programs* mbalimbali za maendeleo ikiwemo uandaaji wa dira na kuanza utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukirejea dira ina maeneo gani, maeneo makuu manne ya dira ambayo iliandaliwa na kuanza kutekelezwa mwaka 2000, eneo la kwanza ni huduma za jamii; eneo la pili ni amani, usalama na umaja wa Taifa; eneo la tatu utawala bora; na eneo la nne kukuza uchumi. Katika maeneo yote hayo manne hadi sasa tunavyozunguzma tumefanya vizuri zaidi na hasa kipindi hiki cha tano cha 2015 – 2025 tunakoelekea kumekuwa na uwekezaji kwenye maeneo karibu yote muhimu ya miundombinu na huduma za jamii, elimu, afya, maji, barabara, madaraja, viwanja vya ndege, bandari, reli na umeme mambo makubwa sana yanafanyika katika nchi hii hata watu wengine wanatuonea wivu. Juzi alikuja Mkongo mmoja akasema hebu tuazimeni Magufuli Congo angalau kwa muda mfupi aje kutawala huku. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais na kwa hotuba zake mbili muhimu sana. (*Makofii*)

Naomba sasa kuititia Bunge lako Tukufu niwasilishe changamoto kuu ambazo bado zinatukabili. Ya kwanza ni masoko ya mazao, bado wakulima katika maeneo mengi wana manung'uniko dhidi ya bei. Kwa Sikonge, tumbaku bado tuna manung'uniko makubwa lakini tunashukuru Mheshimiwa Naibu Waziri Bashe alivyokuwa Tabora juzi alitoa hotuba nzuri ambayo imetuletea matumaini, tunachoomba *vision* yake iweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya pili ni barabara vijijini. Ufinyu wa bajeti ya *TARURA* inatakiwa Serikali itafute chanzo chochote kile ili kuiongezea *TARURA* uwezo wake iweze kusaidia barabara vijijini. Hatuwezi kupata maendeleo ya kilimo kama *TARURA* hawezeshwi kutengeneza barabara za vijijini. Wanatengeneza barabara nyingi kwa udongo, ikija mvua kidogo tu inaosha na tunarudi kwenye matatizo yale yale. Changamoto kubwa ya tatu vijijini ni huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina maombi maalum kutokana na hotuba ya Mheshimiwa Rais. Katika ukurasa wa 33 amesema: "Tunakusudia kujenga shule moja ya sekondari kila mkoa itakayofundisha masomo ya sayansi kwa wasichana". Sikunge tunacho kituo cha vijana cha TULU ambacho kiliwekwa jiwe la msingi na Mheshimiwa Waziri Mkuu Pinda mwaka 2012 na kikazinduliwa na Mheshimiwa Rais Kikwete mwaka 2014. Hadi sasa waliofaidika pale hawazidi 100. Sasa kwa kuwa zilitumika shilingi bilioni 2.5 na zaidi za Serikali na kuna majengo pale Serikali iwekeze fedha kidogo tu ili tupate shule hii katika mkoa wa Tabora ambayo itakuwa Sikunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa naomba Serikali ijenge barabara ya Ipole – Rungwe ili kuunganisha Tabora na Mbeya. Vilevile ijenge na ikamilishe barabara ya kutoka Chunya - Itigi - Mkiwa illi kuunganisha Mkoa wa Mbeya na Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana kwa nafasi hii. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Aloyce Kamamba, Mheshimiwa Innocent Karogeris ajiandae.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichukue nafasi hii kumshukuru Rais wetu Dkt. John Joseph Magufuli. Pili, niunge mkono hotuba mbili zote alizozitoa Mheshimiwa Rais. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda ukurasa wa 12 wa hotuba ya kufungua hili Bunge, Rais alisema: "Nataka Watanzania wote washiriki kikamilifu katika kujenga uchumi wa nchi yao." Tunapoongelea uchumi jumuishi hii ndiyo falsafa yenyewe ambayo Rais anatuelekeza katika hotuba yake. Hata hivyo, hatuwezi kuwajumuisha Watanzania wote katika kujenga uchumi wa nchi yao kama hatujawawekea miundombinu ya kutosha. Ili kuhakikisha kwamba Watanzania wote wanashiriki katika uchumi wa nchi yao,

lazima tuangalie sekta za kimkakati ambazo ni pamoja na kilimo na uvuvi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiongelea kilimo, nchi yetu bado inategemea kilimo katika kuzalisha mazao ambayo tunauza nje. Tunayo mikoa ya kimkakati ambayo ni wazalishaji wakubwa wa mazao ya kilimo na biashara. Hatuwezi kuwa na kilimo chenyetija kama tunaendelea na kilimo cha jembe la mkono na cha kutegemea mvua, jua na kiangazi, lazima twende kwenye kilimo cha umwagiliaji maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu la Muleba Kusini tunayo miradi miwili ya umwagiliaji maji. Tunao mradi wa Kyamyorwa ambao Serikali yetu Tukufu imeugharamia kushirikiana na wadau wengine, tekeo tayari, mfereji umejengwa, tumbakiza banio. Niombe Wizara ya Kilimo ikamilishe mradi huu ili wananchi wa Kyamyorwa na Muleba na Mkao wa Kagera kwa ujumla wake waweze kufaidi na kuendeleza kilimo cha umwagiliaji maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao mradi mwingine wa Buhangaza ambao umejengwa lakini haujakamilika. Hii miradi imetumia fedha za walipa kodi, niisihi, kuiomba na kuishauri Wizara ya Kilimo, miradi hii ikamilishwe ili iweze kuzalisha kulingana na pesa tulizoziwekeza pale ili wananchi wanufaikie na miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkao wa Kagera unapakana na nchi nyingi jirani kama Rwanda, Uganda na Burundi. Tukitumia fursa tulizonazo katika Mkao wa Kagera ambaapo tunalo bonde la Mto Ngonon ambalo linafaa kwa ajili ya kilimo na uzalishaji mkubwa wa chakula, tukiweza kuwekeza katika bonde hilo Mkao wa Kagera unaweza ukawa soko la chakula kwa ajili ya nchi zote zinazozunguka mkao wa Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye sekta ya uvuvi. Sekta hii inaanjiri vijana wengi na nitajikita katika Ziwa Victoria ambako mimi natoka. Ukiangalia kazi zinazoendelea katika Ziwa Victoria sisi kama Tanzania tunamiliki asilimia 51

ya ziwa lile, wenzetu wanamiliki asilimia 49, Uganda wana asilimia 43, Kenya wana asilimia 6 lakini ukiangalia mauzo nje ya nchi inaonekana sisi tunauza kidogo kuliko wenzetu ambaao wanamiliki eneo dogo la Ziwa Victoria. Kwa nini inakuwa hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, jana kuna Mbunge hapa alichangia kuhusu sekta ya mifugo, ukiangalia kwa nini hatufanyi vizuri katika mauzo ya nje kama Rais anavyotuambia biashara ni vita, mfumo wa tuzo zinazotozwa kwenye mazao yanayotokana na uvuvi na ukilinganisha na nchi za jirani, sisi tozo zetu ziko juu sana. Niishauri Wizara ya Uvuvi kuhakikisha kwamba tunapitia tozo zote ambazo zinazotozwa kwenye mazao ya samaki. Tuhakikishe kwamba zile tozo aidha zinalingana na nchi jirani au kwa kuwa tuna eneo kubwa la ziwa tunaweza tukafanya ujanja tuka *under cut* tuwe na tozo za chini ili tuweze kuvuna na kuuza nje mazao mengi ya uvuvi. Vinginevyo tutabaki nyuma, tutabaki kulalamika lakini jambo la msingi tupitie tozo kama nilivyoshauri ili tuweze kupata pesa za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kwenye sekta ya uvuvi, Wilaya yangu ya Muleba ina visiwa 39 na visiwa 25 vinakaliwa na wavuvi. Ilipokuja hii ya sera ya kukamata wavuvi haramu, siwaungi mkono lakini nawaomba na nishauri Wizara ya Uvuvi, busara itumike tunapokwenda kwenye zoezi la kuwakamata wavuvi haramu. Kinachoendelea sasa imekuwa kama kukomoana na kuna kesi nyingi ambazo zinaendelea watu wanakamatwa, wanafunguliwa kesi na wakati mwingine kesi zenyewe ukiziangalia hazina hata ushahidi wa kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bukoba tumejengewa Chuo cha *VETA*. Nimshukuru Rais wetu na Serikali yetu Tukufu. Nategemea Waziri wa Elimu, kati ya mitaala itakayoendeshwa kwenye Chuo kile cha *VETA* tuwe na mtaala ambaao unawafundisha vijana wetu kutengeneza nyavu na vifaa ambavyo tunavitumia katika sekta nzima ya uvuvi kwa sababu Mkoa wa Kagera na Mikoa ya Kanda

ya Ziwa inategemea sana uvuvi katika uchumi wake.  
*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana na naunga hoja mkono hotuba zote mbili na hotuba zote zilizotangulia kabla ya hizo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Aloyce Kamamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Kalogeresi, Mheshimiwa Antipas Mungus ajiandae.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru kwa nafasi, lakini kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuchangia katika Bunge lako Tukufu, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia baraka zake zote na hatimaye kuweza kuchaguliwa, lakini nikishukuru Chama Cha Mapinduzi kwa kuniamini, lakini wananchi wa Wilaya ya Kakonko na Jimbo la Buyungu kwa ujumla kwa kunichagua kwa kura nydingi ikiwa ni pamoja na Rais na Madiwani wote wa Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, moja nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya ya kukiongoza chama chetu, lakini pia katika miradi mbalimbali anasimamia na nchi kwa ujumla. Vilevile niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri ambao wameaminiwa. Wameanza vizuri sisi Wabunge tutaendelea kuwatia shime, ili muweze kufanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mbalimbali imeanzhishwa katika nchi yetu ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Kakonko. Katika wilaya yetu ipo miradi mbalimbali ya umeme, ipo miradi ya maji, lakini iko hospitali ya wilaya inajengwa, lakini katika uchaguzi uliopita mwaka 2015 Mheshimiwa Rais alitupatia kilometra tatu za Mji wa Kakonko, ujenzi unaendelea. Shida yangu ni ukamilishaji wa miradi inayoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichukua mfano stendi ya Mji wa Kakonko ambayo iliahidiwa mwaka 2015; ujenzi

umeanza kwa kilometra 0.63, lakini ninavyozungumza ule mji wamekwenda wameujaza kifusi, ujenzi haujakamilika na hakuna kinachopendelea, lakini vilevile kuna stendi ambayo nimeitaja bado fedha zake hatujaweza kuzipata. Wazo la jumla ambalo naliomba ni uletaji wa fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa miradi hiyo ikiwa ni pamoja na ufuatiliaji na ubora wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu; nishukuru sana kwamba, Mheshimiwa Rais ameweza kuanzisha program ya mpango wa elimu bila malipo. Hii inawalenga watoto wa Watanzania, lakini ambao wanatoka katika familia maskini. Tumefanikiwa vizuri sana watoto wameandikishwa, lakini imeleta changamoto nyingine ya vyumba vyta madarasa na uhitaji wa walimu. Tuna shida kubwa sana ya walimu katika shule zetu za msingi na sekondari. Hasa kwa sekondari walimu wa masomo ya sayansi, lakini kwa shule za msingi walimu katika masomo yote. Niombe tunapotekeleza program hii ya mpango wa elimu bila malipo, chonde chonde, walimu waajiriwe ili waweze kujaza kwenye upungufu ambao tunao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi wanaomaliza darasa la saba wapo wanaofanikiwa kwenda kidato cha kwanza, lakini wapo wanaobaki. Tunao wanafunzi wamemaliza kidato cha nne, hawafanikiwi kwenda kidato cha tano au kwenda kwenye kozi yoyote ile, hawa tunawasaidiaje? Ndio hoja inakuja ya kuwa na vyuo vya VETA. Jana katika swalii la msingi liliulizwa, lakini ikatajwa kwamba, vinajengwa vyuo vya VETA. Niombe vyuo hivi vijengwe vingi na kwa haraka kwa lengo la kuwasaidia watoto hawa waweze kupokelewa katika vyuo hivyo wapate mafunzo na kozi mbalimbali ambazo zinawasaidia watoto wetu katika masomo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna upangaji wa Walimu. Kuna utaratibu ambao umewekwa, inachukuliwa idadi ya wanafunzi wanagawa kwa idadi ya Walimu, wanafunzi ambao ni 40; utaratibu huo haujibu shida ya Walimu tulionao. Uandalifiwe utaratibu maalum tofauti na utaratibu uliopo

wa kuangalia jinsi ambavyo walimu wanaweza wakapangwa katika shule zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa kilimo; kilimo ndio uti wa mgongo na wananchi wetu wengi wanategemea kilimo, lakini pembejeo hazifiki kwa wakati. Hiyo inakwenda sambamba na mbolea, lakini Maafisa Ugani. Maafisa Ugani nao hawapo wa kutosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe Serikali ichukue hatua za makusudi ili nao waweze kuajiriwa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba, mbolea inapatikana, lakini inapatikana kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna upande wa madini; madini yapo maeneo ambayo yameashabainishwa na uchimbaji unaendelea, lakini kuna maeneo ambayo wachimbaji wadogo wanagundua madini katika maeneo tofauti tofauti katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe nayo Serikali ichukue hatua za makusudi pale ambapo imebainika kwamba, kuna madini yamebainishwa, basi utafiti ufanyike na hatua za ziada zichukuliwe ili uchimbaji uweze kufanyika iwe sambamba na maeneo mengine ambayo uchimbaji unafanyika katika nchi hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa afya; vituo vya afya havitoshelezi. Nikitoa mfano katika wilaya yangu nina vituo vitatu tu Kituo cha Nyamtukuza, lakini Gwanumpu na Kakonko, havitoshelezi na katika kata kumi vituo hivyo havipo. Naomba sana Serikali iweze kuchukua hatua vituo hivyo viweze kujengwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Antipas Mungus, atafuatiwa na Mheshimiwa Ramadhani Suleiman na Mheshimiwa Edwin Enos Swalle ajiandae.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwanza naunga mkono hoja, lakini pili napenda nijikite kwenye hii hotuba ukurasa wa 46 ambaa unazungumzia masuala ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Serikali, hasa Wizara ya Maliasili, Waziri na wasaidizi wake kwa kuongeza idadi ya wageni kutoka 2015 mpaka sasa hivi 2021 idadi ambayo imetajwa pale sambamba na mapato yameongezeka kama ambavyo imetajwa kwenye hotuba kwa wale waliopitia, lakini pamoja na hayo niseme tu kwamba, hii dira ya Rais, maono yake ya kutaka kuongeza idadi ya wageni kutoka milioni moja na kitu mpaka milioni tano mwaka 2025 itafikiwa tu kama Wizara na wataalam wake wakitoa ushirikiano wa kutosha, lakini hasa kubadilisha *mind set* kwa maana ya kwamba, lazima tukubaliane utalii ni biashara. Kwa uzoefu tu wa kawaida kumekuwa na hali ya kwamba, uhifadhi umekuwa unashindana na utalii ndani ya Wizara na taasisi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yangu ni kwamba, kunapokuwa na changamoto ya bajeti kwenye Wizara pamoja mashirika, lakini bajeti ya kwanza kuonewa ni ya utalii, lakini hasa ya masoko, kwa maana ya *tourism promotion*. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake na wengine kwenye mashirika waanze kubadilika kwa maana ya kuona utalii ni biashara, lakini pia utalii ndio unamlea uhifadhi. Shughuli zote za doria za magari, za mafuta, *uniform* za wapiganaji, posho na vitu vingine vinanunuliwa au vinalipwa kutoptera na makusanyo yanayotokana na utalii. Kwa hiyo, niwaombe sana ndugu zangu waweze kutoa kipaumbele kwenye bajeti za utalii kuliko vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hata Bodi yetu ya Utalii ambayo sasa ndio inayofanya masoko imekutana na changamoto ya bajeti kwa miaka mingi. Tumekuwa tunajitahidi inawekwa fedha nyingi, lakini fedha ambayo inatoka kwa utekelezaji inakuwa ni ndogo sana, hali ambayo inafanya tusiweze kushindana kama ambavyo inapaswa.

Ukiangalia wenzetu nchi jirani ya Kenya, wengine wa Afrika Kusini na Wamoroko wanafanya vizuri zaidi kitakwimu, wanaingiza wageni wengi, lakini hawana vivutio vingi kama ambavyo sisi tunavyo Watanzania. Kwa hiyo, utalii ni biashara, lazima tukubali kwamba, utalii ndio unalea uhifadhi, ili uhifadhi ufanyike kwa kiwango tunachokipenda, basi tupate fedha kwanza kutoka kwenye utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, niwashukuru wafanyabiashara kwa maana ya wakala wa utalii. Wao ndio wamekuwa wakileta wageni kwa zaidi ya asilimia 80 hapa nchini. Kwa hiyo, niombe tu Wizara iendelee kushirikiananao kwa ukaribu kujifunza kuona wenzetu wanachokifanya, ili wageni waweze kuja kwa wingi kufikia hili lengo la Rais la kufikisha wageni milioni tano mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, kumekuwa na changamoto ya migogoro ya mipaka ya ardhi. Sisi kwetu Bonde la Kilombero tuna changamoto nzuri kidogo niseme kwa sababu, kuna hili suala la mradi wetu wa umeme wa Nyerere, *Stiegler's George*. Ni mradi mkubwa wa kitaifa ambao sote tunaupenda na tunautakia heri, hatuko tayari kumuona mtu ye yeyote ambaye anaharibu, lakini sisi watu wa Bonde la Kilombero imeonekana tunatoa sehemu kubwa ya maji ya mradi ule, kwa hiyo, kwa maana yake ni kwamba, baadhi ya maeneo ambao tulikuwa tunalima muda mrefu na kufuga kwa sasa yanakwenda kuathirika. Suala la uhifadhi limekuwa *serious* na Serikali kwa hiyo, baadhi ya vitongoji vyetu vya Jimbo la Malinyi, Ulanga na Mlimba vitaenda kupotea kwa maana ya vinafutika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji kimoja cha Ngombo ambacho kipo Malinyi nacho kwa msimamo wa Serikali lazima kifutwe kwa sababu, inasemekana ndio chanzo cha maji mengi ambayo yanakwenda *Stiegler's*. Pengine sisi hatuna pingamizi sana, nniombe Serikali, Waziri Mkuu yupo hapa na ndugu yangu Dkt. Ndumbaro, Waziri, yuko hapa tutatoa ushirikiano kadiri inavyotakiwa, lakini naomba tu tusaidike kwa maana ya Kijiji cha Ngombo kibaki, lakini kwa masharti ili tusiharibu uhifadhi.

Kwa hiyo, tuko radhi kupunguza idadi ya mifugo. Serikali tutashirikiana nayo kupunguza hata matrekta na masuala mengine ambayo tunaona yanachangia kuharibu uhifadhi, ili mradi wetu huu mkubwa usikwame, lakini naomba Serikali itufikirie wananchi waweze kubaki kwa masharti ambayo watayatoa au ambayo tutaafikiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, maeneo ya ziada ya kulima kwa Jimbo zima la Malinyi imekuwa ikitusumbua. Kuna mpaka wa mwaka 2012 uliwekwa, badaye kuna mpaka mwingine mpya 2017, yote hayo inasemekana hayapo kwenye *GN*, lakini niombe Serikali, hatubishani nao, lakini naomba tufikiriwe angalau mita 700 tu kutoka kwenye mpaka ule wa 2017 tuweze kupatiwa ili tuweze kuendeleza shughuli zetu za uchumi. Sasa hivi Malinyi imesimama, watu hawalimi, tunasubiri hatma ya mwisho ya Serikali kutuambia mustakabali wetu ukoje.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliambiwa kuna Mawaziri wanane wale watakuja kutoa hatima, lakini muda unazidi kwenda watu hawana cha kufanya, majibu yanatakiwa na mimi kama Mbunge majibu sina. Kwa hiyo, niwaombe Serikali basi itoe *official statement* tuweze kujua nini ni nini na nini kinachofuata, maana sasa hatujui hatima yetu. Kwa hiyo, nashukuru sana, naamini Wizara na Waziri Mkuu watashirikiana kuweza kutufikiria sisi watu wa Malinyi, Ulanga na Kilombero.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ni suala la changamoto ya miundombinu ya barabara. Kwetu Malinyi kuna barabara kubwa ambayo tunaisubiria, maarufu kama Barabara ya Songea, lakini Kiserikali inaitwa Lupilo – Malinyi – Londo – Namtumbo, kilometra 296 ambayo itaunganisha Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Ruvuma kupitia Wilaya ya Malinyi na Namtumbo.

Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Miundombinu na Serikali kiujuimla kutufikiria hili jambo liweze kuanza kwa uharaka ili tuweze kutokea Songea na mikoa mingine. Jambo hili likifanyika itakuwa imetusaidia

kukuza uchumi wa Malinyi na Ulanga Kilombero kama mbadala wa kilimo ambacho sasa inaelekea tunaenda kuacha kutokana na changamoto ya mpaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, nitoe shukrani kwa Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya, hasa kunisaidia wakati nimeumwa Novemba, Disemba. Nilipata huduma nzuri Ofisi ya Bunge ilinisaidia, lakini Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Hospitali ya Sokoine Morogoro, walinisaidia nilipata huduma nzuri kwa hiyo, nimesema nichukue wasaa huu kuwashukuru. Mwisho wazazi wangu Mzee Zeno Mgungusi na mke wake Theopista Nghwale na mke wangu Mariam Ali Mangara *aka* mama Moringe nawashukuru wote kwa kunipa ushirkiano.. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge muwe mnanukuu watu waliotaja wenzi wao humu ndani, baadaye watu sio wanaanza kubisha wanaleta orodha mpya hapo. (*Makofii*)

Tuendelee na michango ya Waheshimiwa Wabunge. Tutaendelea na Mheshimiwa Ramadhan Suleiman, atafuatiwa na Mheshimiwa Edwin Eno Sware na Mheshimiwa Salim Musa Omar ajiandae.

**MHE. RAMADHANI SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia kwenye Hotuba ya Rais ya kufungua Bunge aliyoitao katika Bunge hili tukufu Novemba pamoja na ile ya kufunga.

Kwa kuwa na mimi ndio mara yangu ya kwanza kuchangia ndani ya Bunge lako hili tukufu, naomba kwa heshima kabisa nitoe shukrani zangu kwa chama changu Chama Cha Mapinduzi kwa imani yake iliyonipa, hasa kwa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wetu Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa utumishi uliotukuka. Pia,

nichukue fursa hii kutoa shukrani zangu kwa wananchi wa Chakechake kutokana na *support* waliyonipa na imani waliyonipa ili niye niwawakilishe katika Bunge hili Tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu ambao nataka niongezee kwenye hii *guide book* ambayo ni hotuba ya Mheshimiwa Rais ni kwenye suala la utalii. Mheshimiwa Rais *vision* yake aliyoiweka kwenye *guide book* hii ya hotuba ni kwamba, anasema ndani ya miaka mitano kutoka 2020 mpaka 2025 anatamani aone watalii wameongezeka Tanzania mpaka kufika milioni tano ambao watachangia kwenye pato la Taifa kwa Dola za Kimarekani bilioni sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ushauri wangu kwa wasaidizi wa Rais ambao wamepewa kazi ya kumsaidia Rais kufikia hayo malengo ya *ku-promote* utalii Tanzania ni kwamba, ninavyoona mimi ili hili lengo lifikiwe, la watalii milioni tano ambao watachangia zaidi ya Dola za Kimarekani bilioni sita, moja katika eneo ambalo tunalikosea ni mawasiliano mazuri baina ya taasisi zinazokuza utalii za Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi unahisi inakuwa ni *very normal*/mgeni kutua Zanzibar akatumia zaidi ya siku nane akiwa Zanzibar, katoka ulaya, halafu akaondoka kurudi Ulaya bila kupita Tanzania Bara, hili jambo sio sahihi. Inavyoonekana ni kwamba, hizi taasisi zetu za kukuza utalii au idara za utalii baina ya bara na Zanzibar hazina mawasiliano mazuri. Hakuna juhudzi za makusudi zinazochukuliwa baina ya pande mbili hizi kuwasiliana ili kuwashawishi wagensi wapate kutumia siku zao wanazokuwa Tanzania kwenye pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtalii ameshakuja Zanzibar au yuko Serengeti anatumia siku nane, unaachaje kutumia fursa hiyo kumshawishi mgeni atumie siku mbili za siku nane zake akiwa Serengeti wakati ameshakuja Tanzania? Kwa hivyo ilivyo sasa haiku vizuri sana. Ushauri wangu kwa kaka

yangu Waziri wa Utalii, Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, ni kwamba anaweza akatafuta namna ya kuzi-link hizi idara za utalii zilizoko Tanzania Bara na zilizoko Zanzibar ili tuwashawishi wageni wanaokuja Tanzania waweze kutembelea pande zote mbili za Muungano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano ni kwamba, mwishoni mwa mwezi Desemba, Wizara ya Utalii ya Tanzania Bara ilipata ugeni wa Bwana Drew Binsky alitoka Marekani. Huyu jamaa ni mtu maarufu sana ambaye ametengeneza makala nyingi za utalii duniani. Ni mtu ambaye kwenye *face book page* yake ana zaidi ya *follower* milioni 30, *video* yake moja aliyo*-post* akiwa Moshi imetazamwa na *viewers* zaidi ya milioni 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kusikitisha hizo fursa watu wameshindwa kuwasillana baina ya Zanzibar na Tanzania Bara maana yake hata siku moja huyu Drew alishindwa kuwa Zanzibar akapiga picha akiwa *Stone Town*, ambayo pengine ingeonekana leo na watu zaidi ya milioni 20 duniani watu wangeshawishika kufika Zanzibar nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ushauri wangu, ili tumsaidie Mheshimiwa Rais afike hilo lengo la hao watalii milioni tano tuna haja ya kufanya jitihada za makusudi. Watalii wanakuja kutembelea Zanzibar kwenye fukwe pia tuweze kuwashawishi wawe wanakuja kutembelea kwenye mbuga zetu za Serengeti na nyingine zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndiyo mchango na ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri anapokwenda kumsaidia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufikisha *vision* yake ya kukuza pato la Taifa hasa kupitia utalii kwa kukusanya zaidi ya dola za Kimarekani bilioni 6. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. RAMADHANI SULEIMAN RAMADHAN:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Edwin Enos Swale atafuatiwa na Mheshimiwa Salim Mussa Omar, Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda ajiandae.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba za Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu leo ni mara yangu ya kwanza kuzungumza ndani ya Bunge lako Tukufu, naona basi ni vema nikatumia nafasi hii pia kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt John Joseph Pombe Magufuli na Mwenyekiti wa Chama chetu cha Mapinduzi na Halmashauri Kuu ya Chama chetu cha CCM kwa kuwa na imani kubwa na kuitisha jina langu kuwa Mbunge wa Bunge hili la Kumi na Mbili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wetu amekuwa akiacha alama kila mahali. Ameacha alama kwenye nchi lakini pia ameendelea kuacha alama kubwa kwa sisi vijana wa nchi hii kwa kutuamini na kutupa nafasi. Mheshimiwa Rais ahsante sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ufupi sana napenda nitumie kama dakika moja pia kuwashukuru sana familia yangu ya Mzee Enos na kipekee mke wangu mpenzi Tumaini anayelea wanangu wawili kwa ufasaha mkubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijikite kwenye mchango wa hotuba za Mheshimiwa Rais. Nimesoma hotuba mbili za Mheshimiwa Rais, hotuba hizi zina sura mbili sehemu ya kwanza zinaleza mafanikio makubwa ya miaka mitano iliyopita, lakini sehemu ya pili inaeleza mipango ya Serikali kwa miaka mitano ijayo. Tunavyompongeza Mheshimiwa Rais kwangu mimi nadhani pia ni muhimu sana kuwapongeza Makamu wa Rais, Waziri Mkuu wetu na Mawaziri wote waliopita kwa kazi nzuri waliyofanya kwa ajili ya nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sote ni mashahidi, tulishuhudia Waziri Mkuu wetu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Kassim, akizunguka hii nchi nzima kusimamia llani ya Chama cha Mapinduzi. Mimi ni kati ya Wabunge ambao niliomba sana Mungu Mheshimiwa Majaliwa aweze kuendelea kuwa Waziri Mkuu na tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Mwenyezi Mungu alimuonyesha akampa nafasi Mheshimiwa Waziri Mkuu ya kuendelea na utumishi wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini maombi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuendelea kuwa na nafasi ya Waziri Mkuu nilikuwa na sababu maalum. Pamoja na kazi nzuri sana ambayo Serikali imefanya kwa miaka mitano iliyopita na hasa kwenye kipengele cha kilimo, Waziri Mkuu ameshughulika sana kutatua kero za mazao mengi ya kimkakati. Tumemuona Waziri Mkuu akihangai na zao la korosho katika nchi hii, pamba, mkonge na mazao mengine katika nchi hii. Hata hivyo liko zao moja ambalo katika miaka mitano iliyopita na hiki pengine ni kiporo ambacho naiomba Serikali katika mpango wake wa kuendelea kukuza ajira kwa wananchi wa Tanzania Serikali kupitia Waziri Mkuu awamu hii ya pili ya miaka mitano ya utumishi watazame katika zao la chai ambalo ni zao la kimkakati la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu la Lupembe wananchi walisikiliza hotuba ya Mheshimiwa Rais. Ukiangalia kwenye ukurasa 12 wa hotuba ya Mheshimiwa Rais ya mwezi Novemba 2020, Mheshimiwa Rais aliwaahidi Watanzania pamoja na wananchi wa Jimbo langu la Lupembe kwamba anayo ndoto na angetamani sana wananchi wetu waweze kuwa mabilionea. Wananchi wa Jimbo la Lupembe wako tayari kuwa mabilionea na wamejiandaa kuwa mabilionea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mchango wangu wa hotuba hii wamenituma kumuomba Mheshimiwa Rais mambo mawili ya msingi sana. Jambo la kwanza wananchi wa Lupembe wanasema pamoja na uchapa kazi, wanamuomba Mheshimiwa Rais awasadie ahadi ya barabara ya lami kuanzia Kibena - Lupembe - Madeke -

Morogoro. Barabara hii ikifunguka hata wewe Naibu ukitoka pale Mbeya utapita Jimbo la Lupembe kuelekea Dar es Salaam, lakini hata Waziri Mkuu mwenyewe anaweza kupitia barabara hii badala ya kupita barabara ya Iringa ambayo ni ndefu na ina milima mikali sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jambo hili la zao la chai kuna changamoto kubwa sana katika Jimbo la Lupembe. Wananchi wengi wa Jimbo la Lupembe hawalipwi fedha zao na viongozi wengi wa Serikali wamekuja Lupembe wakipewa ahadi na wawekezaji kwamba wangelipa fedha hizi kwa wakati lakini mpaka leo tunavyozungumza Makamu wa Rais amekuja kapewa ahadi hii, Waziri Mkuu amekuja kapewa ahadi hii, Waziri wa Kilimo amekuja kapewa ahadi hii nilikuwa lakini utekelezaji hakuna.

Kwa mujibu wa Sheria yetu ya Makosa ya Jihai, kifungu cha 122 ni kosa kwa mtu kumweleza taarifa za uongo kiongozi wa umma na kwa kuwa wawekezaji hao wamekuwa wakitoa taarifa siyo za kweli kwa viongozi wetu wa Serikali, naiomba Serikali sasa ingewaita wawekezaji hawa waeleze ni kwa nini wasichukuliwe hatua kwa kuiambia Serikali au viongozi wetu taarifa ambazo hawawezi kutekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili naomba niseme kidogo sana kwenye ajira. Naomba sana watu wa TRA waweke mazingira rafiki kwa vijana wetu, wanapofungua biashara wapewe *grace period* ya kuanza kulipa kodi angalau mwaka mmoja au miaka miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huo, naunga mkono hoja, ahsante sana kwa nafasi hii. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Salim Mussa Omar atafuatiwa na Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, Mheshimiwa Nasrat Hanje ajiandae

**MHE. SALIM MISSA OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu *Azzawajal* kwa kutujalia siku ya leo sote tukiwa wazima na

akili timamu. Pili, nikishukuru chama changu cha Mapinduzi kwa kunichagua mionganini mwa vijana ambao wameaminika kupeperusha bendera katika nafasi hii ya Ubunge katika Jimbo ambalo kwa mara ya kwanza linaongozwa na Chama cha Mapinduzi toka 1995. Nawaahidi wananchi wa Jimbo langu la Gando Pemba Kaskazini kwamba sitowaangusha. Naamini huko wanakonisikia sasa hivi au watakaponisikia wataamini kwa yale ambayo yameshaanza kutendwa na Mbunge huyu ndani ya miezi hii miwili mitatu ambayo tumeanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nijikite katika mchango wangu kidogo kwa kutumia dakika chache kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. John Joseph Magufuli kwa yafuatayo. Kwanza, namshukuru sana katika hotuba yake aliposema kwamba ataleta meli nane Tanzania, nne zitaelekezwa upande wa Zanzibar na nne zitabaki upande wa Tanzania Bara. Hii imeonesha wazi kwamba Mheshimiwa Rais wetu kumbe anafahamu kwamba sisi Wazanzibar hatuna madini, madini yetu yako katika bahari. Ndiyo maana licha ya utofauti wa ukubwa uliopo baina ya Tanzania Bara na Zanzibar aliweka uwiano sawa wa mgawanyo wa meli zile, ahsante sana Mheshimiwa Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, papo hapo niiombe Serikali yangu ya Mapinduzi ya Zanzibar kuititia Bunge hili Tukufu kwa kuititia Waziri wetu wa Muungano mama yetu Mheshimiwa Ummy Mwalimu afanye juhudini za kuweza kushauri na kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuanza sasa mchakato mzima wa kutoa mafunzo katika suala zima la bahari kuu. Kwa sababu licha ya kwamba meli hizo zitakuja, tunahitaji utaalami kutoka kwenye kidau au viboti vidogo tulivyovizoea mpaka kwenda kuyazoea mameli haya yanayokuja kunahitaji taaluma kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali iweze kujikita katika suala la utoaji wa elimu kwenye hilo. Naamini ushirikiano ambao Mheshimiwa Rais aliaahidi katika hotuba yake yataenda kuifanya Zanzibar kuwa kama Brunei *In shaa Allah.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais katika hotuba yake hakusita kuzungumzia suala la ushirikiano wa dhati kabisa na Rais wa Zanzibar kwenye suala la amani na utulivu sambamba na kuulinda Muungano na Mapinduzi Matukufu. Nimwombe kaka yangu Mheshimiwa Mkuchika na Waziri wa Mambo ya Ndani wasitoe fursa na mwanya hata kidogo kwa wale watu wachache wa Zanzibar ambao wanatumia *platform* za kidini lakini pia na za kisiasa kutaka kuchokonoa amani ya nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, nimwombe Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu aliahidi kwamba atatoa ushirikiano kwa Rais wa Zanzibar basi afanye hivyo. Nakumbuka alipomtuma Mheshimiwa Waziri Mkuu kuja Pemba katika kampeni yake kumwakilisha alipopiga simu pale alisema atakuja Pemba. Tunamuomba basi Mheshimiwa Rais aje Pemba tupitie katika yale maeneo ambayo ni kero ili aweze kutoa msukumo wa hali ya juu na kumshawishi Mheshimiwa Rais wa Zanzibar. Kwa nguvu yake mimi naamini mambo yataenda kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, namwomba Mheshimiwa Rais pia katika suala la *business dispute* ambalo allilzungumzia kwenye hotuba yake lipewe kipaumbele kwa sababu yapo makampuni yana shida nydingi sana. Sisi vijana ambaao tulimaliza vyuo tukaamua kujiajiri mwanzo tumekumbana na mambo mengi ambayo mwisho wa siku hujui uende ukalalamike wapi. Unakuta muda mwingine unafanya kazi na taasisi ya Serikali wana-freeze pesa, wanashindwa kuzirejesha Serikalini, wanazibakisha ndani ya akaunti ya kampuni yako, kushtakiwa hushtakiwi, pesa ukiangalia ipo lakini kukopesheka hukopesheki na mwisho wa siku unaua mpaka ile taaluma ndani ya kampuni yako. Kwa hiyo, naiomba hii *business dispute* hii ifanyiwe kazi haraka iwezekanavyo ili sisi tulioelekea kujiajiri na wenzetu ambaao wanamaliza shule sasa hivi wanaofikiria kujiajiri waweze kujua wapi wanaelekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nusrat Hanje atafuatiwa na Mheshimiwa Zuena Bushiri na Mheshimiwa Josephine Genzabuke ajilande.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa muda nizungumze.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kabla sijazungumza kwa sababu na mimi ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika Bunge hili la Kumi na Mbili, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa uzima na kunijaalia kila kitu mpaka hapa nilipofika. Pia niwashukuru wazazi wangu na familia yangu na watu wangu wote ambao wako karibu na wananihamu wanajua nini kinafanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijachangia hotuba ya Mheshimiwa Rais ya kuzindua Bunge la Kumi na Mbili iliyotolewa Novemba 2020, niseme kabisa nimesikilizia hotuba hiyo nikitokea gereza la Isanga ambako nilikuwa mahabusu pale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia katika maeneo mawili, eneo la kwanza nitachangia katika ukurasa 13 wa hotuba ya Mheshimiwa Rais ya mwaka 2020 ambako amezungumza na nitaanza na hilo kwa sababu amezungumza kwenye hotuba yake kwamba ndiyo jambo la kwanza na la umuhimu ambalo anafikiri katika Serikali yake kwa muda wa miaka mitano atashughulika nalo ambalo ni kulinda na kudumisha amani ya nchi umoja, uhuru na mshikamano pamoja na kuyalinda Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Kwa uzito wa hoja hiyo na mimi naomba nichangie kwenye hoja hiyo kwa yafuatayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nia ya dhati ya kulinda amani ya nchi, kwa sababu wote tunafahamu kwamba amani ni tunda la haki, kwa hiyo, kimsingi unapozungumza kwamba Serikali imejipanga kulinda amani ya nchi lakini pia kulinda mshikamano wa nchi huwezi ku-*ignore* vitu vidogo vidogo ambavyo vinaonekana kama tunazungumza vitu vingine na tunatenda vitu vingine. Ninasema hivi kwa

sababu naona hapa kama vile hawa wanazungumza hawa wanajibu lakini kimsingi kuna mambo ya msingi ambayo wote tunakumbuka, mimi nitasema *deep down* kila mtu anajua kwamba *there was something very wrong* kwenye uchaguzi wa 2020.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Kuhusu Utaratibu.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kila mtu anajua moyoni kwake kulikuwa kuna mambo ambayo si ya kawaida mpaka watu ambao si wanasiasa walikuwa wanajua, watu wanaofutilia demokrasia ya nchi yetu, watu wanaofutilia taratibu za uchaguzi kwenye nchi yetu walikuwa wanajua kuna shida kubwa imetokea kwenye uchaguzi wa 2020. *That is the fact* kwa sababu *fact* hazibishaniwi. Kwa hiyo, sitaenda *into details* nini killitokea kwa sababu kila mtu anafahamu nini killitokea Zanzibar, watu waliwekwa ndani, kesi zaidi ya 20 na kimsingi mpaka sasa kuna kesi mbili tu na sitaenda kwenye *details* kwa sababu najua kuna kanuni zinanizua kuzungumza masuala ya kimahakama.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nusrat, naomba ukae. Mheshimiwa Ali King, kanuni inayovunjwa.

## KUHUSU UTARATIBU

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 70 (1) mpaka 9 inaeleza kuhusu kusema ukweli au kuhusu kusema uongo. Mheshimiwa aliyekaa kitako, Mheshimiwa Nusrat Hanje anazungumza kwamba vyombo vyote ambavyo vilikuwa vinashughulikia uchaguzi huu vimethibitisha kwamba uchaguzi haukuwa mzuri au haukuwa huru na haki kwa mujibu wa maneno ambayo ameyatumia.

Mimi namthibitishia kwamba vyombo hivyo vyote vilivyoruhusiwa na kujihusisha na uchaguzi ikiwemo Tume ya Uchaguzi na *observers* wote walithibitisha kwamba uchaguzi ulikuwa uko sawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Uchaguzi ndiyo iliyotoa matokeo ya uchaguzi kwa sababu uchaguzi ulikuwa huru. Ma-*observers* wa Umoja wa Afrika, *EISA* ya *South Africa*, Umoja wa Ulaya na *East Africa* wote hawa walisema uchaguzi ulikuwa sawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa afute kauli yake au athibitishe chombo gani ambacho kilikuwa kina *authority* ambacho kimethibitisha uchaguzi haukuwa sawa. Nashukuru. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, alikuwa anachangia Mheshimiwa Nusrat Hanje, kwa mchango wake akasimama Mheshimiwa Ali King kuonesha kwamba anachokizungumza au anachochangia Mheshimiwa Nusrat kinavunja Kanuni ya 70 ambayo inakataza Waheshimiwa Wabunge wanapotoa michango yao kusema uongo Bungeni.

Mheshimiwa Ali King ameeleza yeye kwa kuvitaja ama kwa kuzitaja taasisi alizoona kwamba zilionesha kwamba uchaguzi huo ni huru. Wakati wote tukimsikiliza Mheshimiwa Nusrat nilikuwa najaribu kusikiliza hoja yake ni ipi kwa sababu ameeleza mambo ambayo yako jumla hajasema mahsus, kwa hiyo nilikuwa nasikiliza hoja yake njue inaelekea wapi.

Kwa hiyo, pengine atakuwa pia na mifano kama ambavyo ziko taasisi, ama viko vyombo ambavyo vimesema uchaguzi ulikuwa huru na wa haki. Kwa hiyo, pengine viko vyombo vya habari, ama taarifa, ama taasisi zilizosema haukuwa! Kwa hiyo, mnipe fursa nisikilize mchango wake halafu njue hoja yake inaishia wapi kwa sababu kwa sasa inanipa vigumu kidogo kutoa mwongozo mahsus. (*Makofi*)

Mheshimiwa Nusrat, ushauri wa jumla umesikiliza Waheshimiwa Wabunge wakichangia pande zote, hata wa huku umewasiliza wakichangia hoja ambazo hauna uthibitisho mahsus zinatakiwa kusemwa kwa namna

ambayo hutaambiwa ulete ushahidi, kwa hiyo, huo ni ushauri wa jumla, malizia ushauri wako.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi nilizungumza nikasema *deep down* ndani ya moyo wako kila mtu anajua kulikuwa kuna shida mahali kwenye uchaguzi wa 2020, kila mtu atajitafakari yeye na Mungu wake anajua hicho ndio nilichokizungumza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia labda nishauri jambo moja ambalo ndio hoja ilikuwa hiyo, kama ni kweli umeshinda kihalali na umeshinda, kimsingi sitaki kwenda kwenye uchaguzi kwa sababu Taifa linasonga mbele na kimsingi Watanzania wana matumaini makubwa na pengine namba ndogo ambayo imepatikana na watu ambao wataleta chachu fulani kwenye Bunge hili. Kwa hiyo, wacha tu mwiba utokee ulipoingilia.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, wacha tu mwiba utokee ulipoingilia. Kwa hiyo, kimsingi, nashauri kama kuna kesi ambazo zilitokana na uchaguzi...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri, Mheshimiwa Rais kwa sababu ya hotuba yake...

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mniruhusu hapa mbele nina majina mengi kwa hiyo hapana! Mheshimiwa Halima tafadhalii! Kuhusu taarifa sitaziruhusu ili majina yawewe kuisha hapa, isipokuwa kama mtu anavunja kanuni hilo halivumiliki na Bunge kwa sababu muda tulionao ni mfupi na majina ni mengi. Mheshimiwa Nusrat. (*Makofii*)

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa ushauri kwa Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri ambao wanahuksika na masuala ya kisheria na kimahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi uchaguzi umeisha tujenge Taifa si ndio hivyo tunazungumza hivyo, sasa twende ili tusonge mbele. Kuna watu mpaka leo bado wanasumbuliwa mahakamani na kesi za uchaguzi. (*Makofij*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba kama kuna watu wanahusika na hayo mambo waachieni watu wakafanye maisha yao, kwa nini bado wanaenda mahakamani mpaka Mheshimiwa Salome Makamba bado ana kesi ya uchaguzi, tuna kesi zipatazo 20 *Mainland* na Visiwani. Sasa watu wa *ACTkule* kuna vitu walifanya huko na nini kesi zimepunguzwa mpaka zimebaki mbili ya Nassoro Mazrui na mwenzake yule Ally Omar Shekha. Kwa hiyo, kimsingi nashauri hivyo hatuna haja waache basi watu waendelee na mambo yao unawashikilia watu kwenye kesi za uchaguzi ambao unajua uchaguzi wenyewe yaani mtu unamchukulia mkewe halafu unataka kumuua, *come on!* (*Makofij/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye jambo la pili ambalo nataka kumalizia ni kuhusiana na masuala ya mahakama. Kwenye hotuba ya mwaka 2015 ya kufungua Bunge kwa maana ya Bunge la Kumi na Moja na Bunge la Kumi na Mbili, Mheshimiwa Rais alizungumzia suala zima la mahakama na ni mionganoni mwa watu ambao nimeishi kwa vitendo na ninashuhudia vitu ambavyo vinafanyika kwenye mahakama zetu na kwenye magereza zetu. Kimsingi kuna tatizo kubwa sana na ye ye alizungumza na akashauri kwamba wajaribu kurekebisha mifumo ya uendeshaji kesi ili kusiwe na mrundikano wa watu wengi sana kwenye magereza zetu. Kimsingi huwezi kutenganisha magereza, wafungwa, mahabusu na mahakama. Kwa hiyo, tukizungumza mahakama maana yake haya mambo yote yanahusika. (*Makofij*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka tunapozungumza tishio la *COVID* na mrundikano wa watu ambao wana kesi za upelelezi za miaka zaidi ya kumi kwenye magereza ni jambo la hatari kiafya. Mheshimiwa Waziri wa Afya yupo anasikia, kule kuna changamoto kubwa na niseme, Bunge

likiwa hapa watu wale wadada zetu wale wengine wanafanya shughuli zao nyngine wanakuja, wakija hapa kila siku wanakamatwa wanapelekwa hapo, mimi nimekaa hapo Isanga, wanakuja pale tunaitaga kontena jipya mpaka wanatenga *cell* maalum ya watu wanaoletwa ambao wanaondoka na kuja ambayo unajua huyu wiki ijayo atakuja tena kwa sababu atakamatwa tena uzururaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, labda nishauri kuna vitu vya kurekebisha, Mheshimiwa Rais sijui kama wale wanaomshauri au pia Waziri kuna jambo moja la *digital platform* ya kuendesha kesi, siyo lazima watu wahudhurie mahakamani, lakini pia itasaidia kupunguza molongo wa kesi, kwa sababu kulikuwa kuna malalamiko kwenye kipindi cha *corona* watu walikuwa hawaendi kabisa mahakamani kwa sababu kila mtu alikuwa anajua mikusanyiko ilikuwa haitakiwi. Walijaribu kidogo kuendesha kesi kwa kupitia *digital platform zoom*, Jaji huko aliko kesi zinaamuliwa, nafikiri waongezewe uwezo wafanye kazi ili tupunguze milolongo na mrundikano wa kesi kwenye magereza zetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nimalizie...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele imeshagonga Mheshimiwa, huwezi kuanza na jambo jipya.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nusrat ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Zuena Bushiri, Mheshimiwa Josephine Genzabuke atafuatia na Mheshimiwa Tumaini Magessa ajiandae.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa Bungeni, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali hiki

kwa siku hii ya leo na niwashukuru wapiga kura wangu wanawake wa Mkoa wa Kilimanjaro kwa kunichagua kuingia katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niko katika ukurasa wa 34 wa hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa tarehe 13 Novemba, 2020. Kwanza niipongeze Serikali kwa kutekeleza miradi mikubwa ya maji, 1,423. Hii ni katika sera ya kumtua mwanamke ndoo ya maji. Katika Mkoa wa Kilimanjaro, tunazo wilaya ambazo zina matatizo ya maji na wilaya hizo ni Wilaya ya Mwanga, Same pamoja na Wilaya ya Rombo. Wilaya hizi mbili zimetolewa majibu na Waziri wa Maji asubuhi na bahati Mbunge wa Jimbo la Same aliongozana pamoja na Waziri wa Maji kwenda kuongea zaidi kuhusu mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kuhusu Mradi wa Maji wa Ziwa Chala ambao ni mradi mkubwa ambao uko katika mipango ya kutekeleza katika Wilaya ya Rombo. Wilaya ya Rombo ina changamoto kubwa sana ya maji, mwanamke anaweza akatoka asubuhi nyumbani kwake, akatumia masaa sita kwenda kutafuta ndoo moja ya maji. Katika kutatua suala hili la maji, kuna mradi mkubwa ambao unatekelezwa katika Wilaya ya Rombo, Mradi wa Ziwa Chala, lakini mradi huu hauna fedha za kutosha. Hivyo, niombe Serikali iwasaidie akinamama hawa, akinamama ambao wameifanya kazi kubwa sana katika uchaguzi huu kuhakikisha kwamba Chama Cha Mapinduzi kinaongoza Wilaya ile ya Rombo. Tuiombe Serikali ifanye haraka ili mradi huu ukamilike ili tuwatue akinamama ndoo ya maji katika Wilaya ya Rombo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichangie katika ukurasa wa 19 kuhusu sekta ya viwanda, Manispaa ya Moshi Mjini ina viwanda vingi ambavyo vimefungwa amejaribu kuchangia Mbunge wa Jimbo, lakini kama mkazi wa manispaa ile na kama mwanamke ambaye naiangalia Serikali ya chama changu kwamba inao uwezo wa kufufua viwanda vile. Viwanda vile vimefungwa kwa muda mrefu na ni viwanda vingi ambavyo vimekosesha ajira kwa

vijana, akinamama na wananchi wa Moshi kwa ujumla. Tuiombe Serikali sasa iwasaidie Manispaa ya Moshi, angalau ajira ziweze kupatikana, viwanda hivyo viweze kufunguliwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi katika Wizara ya Afya, kwanza niipongeze Serikali kwa kujenga vituo vya afya pamoja na hospitali za wilaya, lakini wilaya zetu hizo zinakuwa bado hazina dawa za kutosha. Tuiombe Serikali na Wizara ya Afya ijaribu kufuatilia na kupeleka dawa katika hospitali zetu za wilaya na vituo vya afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nyongeza ya hiyo, kuna changamoto katika Wizara ya Afya, kuna huduma ya mama na mtoto, huduma hii katika maeneo machache ya vijiji watumishi wetu wamekuwa sio waadilifu, kwa kuwa tunavyotambua kwamba huduma hii ya mama na mtoto chini ya miaka mitano inatolewa bure.

Hata hivyo, baadhi ya watumishi wetu wanakuwa wakiwatoza akinamama hata wanapooleka watoto wao kliniki na hata wanapoenda katika masuala ya kupima uzito tunaiomba Wizara ya Afya, ifuatilie ili iweze kubaini watu hao, watendaji hao ambao wanaichonganisha Serikali yao na wananchi kwa kuwa Serikali inatambua kwamba huduma hii inatolewa bure, wananchi wanakuwa wanajenga chuki na Serikali yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono hoja ya hotuba ya Mheshimiwa Rais. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Josephine Genzabuke atafuatia na Mheshimiwa Tumaini Magessa na Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge ajiandae.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuzungumza jioni hii ya leo. Kwanza napenda nimshukuru

Mwenyezi Mungu, mwenye wingi wa rehema kwa kunijalia afya na kunipa kibali cha kuweza kusimama ndani ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba niunge mkono hoja ya hotuba hii ya Mheshimiwa Rais. Ili kukuza uchumi pamoja na sekta ya uzalishaji ni lazima tuimarishe miundombinu ya barabara pamoja na nishati ya umeme. Tunamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. John Magufuli tumeshuhudia ndani ya utawala wake barabara zimejengwa na zinaendelea kujengwa, reli ya *SGR* inajengwa, bwawa la Nyerere katika Mto Rufiji linajengwa, hizi zote ni juhudi zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna imani miradi hii yote ikikamilika nchi yetu itaendelea kupaa, wananchi wataweza kuanzisha viwanda vikubwa na vidogo hivyo wataweza kusafirisha mazao yao katika maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa sababu usafiri utakuwa ni wa uhakika, lakini pia tutakuwa tumeweza kupata umeme wa uhakika. Kwa maana hiyo wataweza kukuza kipato chao na kuchangia pato la Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kuhusu kilimo, kilimo kimeajiri watu wengi sana takribani zaidi ya watu asilimia 58 ni wakulima wakiwemo wanawake. Hivyo basi, naomba niishauri Serikali, bajeti ya kilimo iongezwe kusudi iweze kufanya vizuri katika kilimo.

Ninyi wote ni mashahidi, mchana tulienda nyumbani kupumzika lakini tulirudi tukiwa tumepata chakula, chakula kinachotokana na kilimo. Kwa hiyo, naomba niwashawishi Waheshimiwa Wabunge, tuhakikishe bajeti ya kilimo inaongezwa ili wananchi wetu ambao wengi wamejajiri kwenye kilimo waweze kunufaika kuititia kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ikiongezeka tutaweza kupata pembejeo na dhana bora za kilimo, lakini kilimo cha umwagiliaji kitawea kufanya vizuri kwa sababu

miundombinu itakuwepo. Kwa mfano katika Mkao wetu wa Kigoma, tunalo bonde la Mto Lwiche, bonde nzuri sana, ambalo tunaweza kulima kilimo cha umwagiliaji tukalima kilimo cha mpunga, kikaweza kuwanufaisha wananchi kwa chakula, lakini pia wakizalisha mchele wanaweza kuuza hata nje ya nchi wakaweza kuongeza kipato chao na kuweza kuchangia pato la Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu zao la mchikichi; tunaishukuru sana Serikali kwa kulifanya zao la mchikichi kuwa zao la kimkakati, Serikali imeweza kutoa miche ya mbegu lakini bado haitoshelezi kwa sababu wananchi wameitikia kilimo hicho. Kwa hiyo, tunaomba Serikali iendelee kutusaidia kuongeza miche ili wananchi waweze kuzalisha zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu zao la mchikichi pamoja na alizeti vikiweza kulimwa na kutoa matunda, tutaepekana kuagiza mafuta kutoka nje ya nchi kwa sababu pesa nyingi tumekuwa tukizutumia kwenda kununua mafuta nje ya nchi, lakini tukizalisha sisi wenyewe tutaweza kunufaika kupitia kilimo chetu cha ndani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa naomba kuchangia kuhusu ushirika, katika ushirika bado hatujafanya vizuri kwa sababu wananchi kwanza hawana elimu, lakini hata Maafisa Ushirika wenyewe bado ni wachache. Kwa hiyo, elimu inayotolewa kwa Vyama vya Ushirika, SACCOS na SACCAS bado haitoshelezi, kwa hiyo, naomba niishauri Serikali iweze kuongeza juhudzi za kutoa elimu katika Vyama vya Ushirika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nimalizie kwa kuwashukuru wanawake wa Mkao wa Kigoma, walionichagua kwa kura nyingi, walifanya ya kwao lakini wakanichagua nikaweza kurudi ndani ya Bunge lako Tukufu, kwangu mimi Wajumbe wale ni wema kwangu sana. Nawashukuru sana lakini nakishukuru Chama changu Cha Mapinduzi kwa kuweza kunateua na kugombea hatimaye nikaibuka mshindi. Ahsante. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tumaini Magessa atafuatia na Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma ajiandae.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kunipa nafasi ya kuweza kuongea mbele ya Bunge hili. Nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Busanda kuititia Chama Cha Mapinduzi walionipatia kura za kutosha na leo nawawakilisha kama Mbunge ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepitia ya Bunge la Kumi na Moja, lakini katikati kulikuwa na *achievement speech*, ilikuwa katikati tarehe 16 Juni, kulikuwa na taarifa tena ndani ya Bunge hili ambayo Rais alionesa mambo yaliyofanyika. Mwezi Novemba tumekuwa na hotuba nyingine ambayo tunaizungumzia leo Bunge la Kumi na Mbili, Bunge letu la kwanza la Kumi na Moja lilionesha dira na falsafa ya Mheshimiwa Rais anakotaka kuipeleka nchi hii, lakini tarehe 16 Juni, alionesa yale yaliyofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wote ni mashahidi nikiwemo mimi kwenye taarifa hizi na kwa macho yetu, hakuna sekta alioizingumzia ambayo haikufanyiwa maboresho. Kama ni barabara, kiwango cha cha lami kimeongezeka, lakini kama ni barabara za *TARURA* zimeongenza, japokuwa zinaharibika kila mvua inaponyesha. Vituo vya afya vimeongezeka vimejengwa vipyta 1,769, katika hivyo zikiwepo hospitali za mkoa, ikiwemo vituo vya afya. Hii inaonesha wazi kwamba dira na falsafa iliyoukuwa imetolewa imetekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hotuba hii ya Bunge la Kumi na Mbili ambapo ndipo kuna kazi kubwa tunatakiwa kufanya sisi, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, yapo maono makubwa ambayo nimeyaona kwenye hotuba hiyo na wataalam kazi kubwa tuliyonayo sasa sisi kama Wabunge hasa nikiwemo mimi ni kwenda kuhamasisha yale yaliyoandikwa huko ndani yaweze

kutokea. Kwa sababu hotuba ni kitu kimoja lakini utekelezaji ni kitu cha pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sekta ya afya *page* namba 65 wameonyesha wazi kwamba sasa tunakwenda kwenye bima kwa wote. Mtego upo kwa Waziri wa Afya, tunapokwenda kwenye bima kwa wote kipi kilanza kati ya kuku na yai, ni kuku au yai? Inaanza kwanza huduma iwe bora ili watu wahamasike kuingia kwenye Bima ya Afya au bima ya afya kwanza ndijo huduma iwe bora? Kwa hiyo, kuna kazi fulani wataalam wanatakiwa kuifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesema kwenye ukurasa namba 44, *STAMICO* itaboreshwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wachimbaji wadogo wa madini wanasaidiwa. Kazi kubwa tulionayo ambayo naiona Rais ametuwekea mezani hapa, je, huduma hizi tunazotaka kuzifanya wataalam tulionao na sisi wenyewe tunazo *service level agreement* zetu? Kwa sababu inaonekana mwananchi anaweza kuwa huduma katika *level* yoyote, *service level agreement* ni ipi, kiwango gani cha huduma tunatakiwa tumpe, hapo ndijo kuna changamoto. Tunaye Afisa Kilimo je, anakwenda kwenye shamba darasa na haya mashamba tunayoyazungumza hapa ndani ambayo yanaonekana yatakuwa ni mikataba kati ya wanunuaji na wakulima wenyewe yapo, anaweza kuwa haendi kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatakiwa *service level agreement* na watu wetu nini wa *delivery*. Kwa sababu unamuuliza mtu anakwambia nimeingia kwenye *OPRAS*, nimeingia sijui wapi, anaonekana anafanya vizuri lakini ukimuuliza kuna shamba darasa mahali hakuna. Kwa hiyo, mimi najielekeza kama Mbunge kuingia kwenye maeneo haya kuona namna gani tutafanya ili viongozi sisi pamoja na wataalamu wetu waweze kutoa kile ambacho Mheshimiwa Rais anatarajia hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo mengi yaliyozungumzwa hapa ambayo nategemea yakifanyika tutakapokwenda kufunga Bunge hili tutakuta maendeleo

yetu yamekwenda kasi. Ninao mfano mmoja mdogo, nilipokuwa natoka kwenye kampeni nafika *airport* Dar es Salaam nilimwambia mtu mmoja usinipitishe Ubungo kwa sababu tukipita huko wanajenga ile *interchange* itatuletea shida. Akaniambia wewe inaonekana ni wazamani sana kumbe barabara ilishakamilika, tukapita pale juu na bahati mbaya alikuwa ni mwanangu ananiambia baba wewe umepitwa na wakati, tukapita juu tukashuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, yapo mambo makubwa yamekwishafanyika, tutowe nafasi sasa na akili zetu kuhakikisha kwamba yale yaliyosemwa yanaweza kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisitumie muda mrefu sana, naomba niunge mkono hoja, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Ali Mchungahela ajiandae.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha na mimi kuwa Mbunge katika Bunge hili lako tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa, niwashukuru kwa unyenyekevu mkubwa kina mama wa Tanga kwa kuniamini na kunifanya kuwa mwakilishi wao. Nami nawaahidi sitawaangusha na Mwenyezi Mungu anisaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii pia kuwapongeza Mawaziri wote ambao wameanza kufanya kazi zao vizuri kabisa. Kipekee niwapongeze Mawaziri ambao wameshafika katika Mkoa wetu wa Tanga ili kuweza kutatua changamoto zetu wakiwemo Waziri wetu Mkuu, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa na Naibu Waziri wa Maji ambaye amekuja kuwatua akina mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa, nimpongeze Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa hotuba nzuri ambayo ni mwendelezo na utekelezaji wa maono yake makubwa kwa taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 26 -28, Mheshimiwa Rais wetu amepanga kuimarisha miundombinu ili kukuza uchumi na sekta ya uzalishaji. Labda niseme kwamba Mheshimiwa Rais ana vipaumbele sahihi kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nathibitisha hili kwa usemi ama kauli ya Rais wa 35 wa Marekani, Rais John Kennedy mwaka 1961 aliwahi kusema kwamba: "*American economy is good because of its infrastructure and not infrastructure of America is good because of its economy*". Natafsiri kwamba uchumi wa Marekani ni mzuri kwa sababu ya miundombinu yake na siyo miundombinu ya Marekani ni mizuri kwa sababu ya uchumi wake. Kwa hiyo, yule aliyekuwa akidanganya wananchi kwamba vitu siyo maendeleo amuuilize John Kennedy tangu mwaka 1961 alisema kwamba miundombinu ndiyo mpango mzima na Mheshimiwa Rais amechagua vipaumbele sahihi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika suala la miundombinu, Mheshimiwa Rais amepanga kuendelea na upanuzi wa bandari zetu. Labda niseme kwamba bandari ya Tanga imekaa muda mrefu ikiaminika kwamba kuna mwamba usiweza kuvunjwavunjwa na kina chake kuongezwa. Kwa mapenzi makubwa ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ameweza kutenga takribani shilingi bilioni 172 na bandari ya Tanga imeongezwa kina chake tayari imekaribisha meli kubwa zimeweza kutia nanga. Watu wa Tanga tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa hilo na tumempa kura nydingi za kishindo lakini tutaendelea kumuombea kwa Mwenyezi Mungu ili maono yake yatimie katika Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spia, lakini katika suala la upanuzi wa bandari, naomba kuishauri Serikali. Kupanua bandari ni

jambo moja muhimu na zuri kwa kuwa bandari ndiyo uti wa mgongo wa taifa letu lakini ni lazima tujue kwa nini bandari zetu zinapoteza vina vyake.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hii ya kubanua bandari zetu imeligharimu taifa fedha nyingi sana. Miradi wa Tanga ni shilingi bilioni 172 lakini upanuzi wa bandari ya Dar es Salaam unaligharimu taifa shilingi bilioni 336, lakini kuongeza kina bandari ya Dar es Salaam takribani shilingi bilioni 200 na zaidi zitatumika.

Kwa hiyo, nashauri Serikali kama kweli inaamini bandari ndiyo uti wa mgongo wa taifa hili, ni lazima tufanye *study* kujuwa ni kwa nini kina cha bandari zetu kinapungua. Tunayo mataifa wahisani, *JICA* na *KOICA* tushirikiane nao ili kuhahikisha tunafanya *study* ya kina kujua ni kwa nini vina vyta bandari zetu vinapungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatekeleza miradi hii mikubwa lakini kiukweli hatuna wataalam wa *Port and Coastal Engineering* ambao watashirikiana na wahandisi washauri kuweza *ku-implement* miradi ile *accordingly*. Nliombe Serikali yetu pia kama kweli bandari ndiyo uti wa mgongo wa taifa letu tuhakikishe tunawekeza kuhakikisha tunapata wataalam wa *Port and Coastal Engineering* kwa sababu watu wanaichukulia bahari kama ni kitu cha asili kwamba ni mgodi usiomalizika, *this is very wrong concept*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma kidogo *port and cost engineering university of Tokya...*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili imeshangonga Mheshimiwa.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Mchungahela, Mheshimiwa Maimuna Pathan ajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi, Mwenyezi Mungu akubariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeziwezesha kusimama hapa. Kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kwa Bunge hili la Kumi na Mbili, nichukue nafasi hii kuwashukuru wanawake wa Morogoro walionipa kura za kishindo na za heshima yake. Nasema nawashukuru sana akina mama wa Morogoro, nakishukuru sana Chama changu cha Mapinduzi kwa kunileta humu Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru pia Mheshimiwa Rais kwa mambo yote aliyoafanya. Hotuba zake mbili ni nzuri sana, unaangalia ya kuongelea na kuacha unakosa, unatamani uwe na muda mrefu kusudi uongee kila kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na maji. Serikali imefanya vizuri kwenye maji ingawa siyo vizuri sana lakini imejitahidi. Nawashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri kwa upande wa maji. Mheshimiwa Rais jinsi alivyosema kwenye upande wa maji, naomba kila kitu kilichoongelewa kiweze kutekelezeka, kuna miradi ambayo imekamilika na mengine bado haijakamilika. Wananchi wanaomba na wanataka maji, kwa hiyo, miradi ambayo haijakamilika nashauri iweze kukamilika kusudi wananchi waweze kupata maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kubwa kwa hotuba ya Mheshimiwa Rais na jinsi anavyofanya hasa kwa kuchukua kutoka Ziwa Viktoria kuyaleta mpaka Tabora na tunategemea yatakuja mpaka Dodoma, hiyo tunashukuru. Mkoa wangu wa Morogoro una mito mingi lakini mpaka sasa hivi tuna shida ya maji. Mheshimiwa Waziri

na Naibu Waziri wanansikia muuangalie vizuri sana Mkoa wa Morogoro tuweze kupata maji ya kutosha na miradi ile kichefuchefu iweze kuisha kabisa twende vizuri na nikiwa Mwenyekiti wa Kamati naamini nitakuwa pamoja nanyi bega kwa bega. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa miundombinu, Mheshimiwa Rais ameongelea vizuri sana kwenye ukarabati wa reli ya kat, sasa hivi imekarabatiwa vizuri na ukarabati na ujenzi wa reli ya mwendo kasi. Sisi wananchi wa Morogoro kwa kweli tunafaidika vizuri sana na reli hii ya mwendo kasi. Kinamama, kinababa na vijana wote nawashauri muwe tayari kwa sababu ajira imepanda reli hii ikianza. Ila tunauliza ni lini reli hii itafunguliwa kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro ili wananchi waweze kuijweka vizuri kwa mwendo kasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo naweza kuliongelea ni kwenye uchumi. Mheshimiwa Rais amesema kwenye uchumi hasa ataangalia upande wa kilimo, mifugo na maji na hasa mifugo na uvuvi kwani ndiyo sekta zinazoleta ajira kwa wananchi wengi. Kwa upande wa kilimo unakuta asilimia 65.5 wanategemea kilimo na asilimia 100 inazalishwa na wakulima wa vijiji na kila mmoja anategemea chakula kutoka kijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, amesema ataangalia upande wa pembejeo, mbegu na mbolea. Nachoomba kwa Mawaziri wanaohusika ambao tupo pamoja waangalie sana upande wa mbegu. Mpaka sasa hivi hatujitoshelezi kwa upande wa mbegu, kwa hiyo, tuangalie jinsi ya kuzalisha mbegu hasa kwa upande wa taasisi hivi zinazozalisha mbegu pamoja na wananchi waweze kufundishwa na kuelekezwa jinsi ya kuzalisha mbegu tuweze kupata mbegu za kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia jambo lingine ambalo naomba kuliongelea ni kuhusu mbegu zetu za asili. Naomba sana tusidharau mbegu zetu za asili tuone jinsi ya kuziboresha kusudi ziweze kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu Maafisa Ugani. Nashukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ameanza kuwaita Maafisa Ugani na kuongea nao. Nashauri Maafisa Ugani wawe karibu na wakulima kusudi waweweze kuwapa elimu ya kutosha tuweze kuzalisha kwa wingi. Tukizalisha kwa wingi ndiyo tutaweza kupunguza umaskini na ajira kwa kila mmoja.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili tayari Mheshimiwa.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nimeongelea kitu kimoja kinatosha na kuwashukuru wanawake wa Morogoro, ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ally Mchungahela atafuatiwa na Mheshimiwa Maimuna Pathan tutamalizia na Mheshimia Haji Amour Haji.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nikushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi hii kwa sababu kuna wengi sana nafikiri watakosa kutokana na muda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kikipongeza chama changu kwa kuniamini. Pia nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi nyingi sana alizozifanya za kujenga taifa hili. Nawaomba ndugu Wabunge wenzangu kwa umakini kabisa tujitathmini sisi wenyewe, Wabunge hapa nina maana wote pamoja na Mawaziri na Naibu Mawaziri, sisi bado ni Wabunge pia. Kazi tunayoenda kuifanya hasa kwa mategemeo ya Mheshimiwa Rais ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mtizamo kama tutaichukulia kilegelege kwa kufikiria sana masuala ya kisiasa humu ndani nafikiri hatutaweza kufika. Tuna jukumu kubwa kufikisha ndoto hii ya Mheshimiwa Rais ya kuona nchi hii inafika

katika uchumi mkubwa wa viwanda. Kazi hii ni kubwa sana kama tutapoteza muda mwangi sana kufikiria masuala ya kisiasa kwa kweli naifikiri tutakuwa tunajikosea. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo, naomba nizungumzie suala la kilimo hususani wananchi wangu wa Jimbo la Lulindi wamenituma, wananchi hawa waliikopessa Serikali tangu mwaka 2017, walilima Miche ya korosho, hili jambo limekuwa kizungumkuti mpaka hivi leo. Tunapozungumzia suala zima la kutaka kufanya uchumi wa viwanda kwenda mbele sehemu mojawapo ni wakulima kwa sababu wanategemewa katika kuleta *raw materials* lakini pia kwa sababu kilimo ndiyo sehemu kubwa sana ya biashara. Hatuwezi kuzungumza biashara kubwa za kimataifa kama hapa kwenye kilimo hatutaweza kupafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali kwa moyo mkunjufu kabisa iwasaidie wananchi hawa amba waliikopessa Serikali Miche ya korosho tangu mwaka 2017, ni wengi sana. Jimboni kwangu na wilayani kwa ujumla wanafikia takribani watu mia tatu na zaidi lakini kwenye nchi nzima pia na nina taarifa kuwa kuna nane imeathirika kutokana na tatizo hili. Kwa hiyo, tunahitaji kwa namna moja au nyngine kuwaangalia wananchi hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, napenda kuunga mkono hoja. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Maimuna Pathan tutamalizia na Mheshimiwa Haji Amour Haji.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha siku ya leo kwa kunipia pumzi ya uhai na pia kupata nafasi hii ya Ubunge. Pia nawashukuru akina mama wa Mkoa wa Lindi kwa kuniamini na kunipa nafasi hii ya Ubunge ili niweze kuwatumikia miaka hii mitano. Vilevile nakishukuru chama change, Chama cha Mapinduzi na shukrani za pekee pia ziende kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuwa alitekeleza vizuri llani ya chama

chetu kuanzia mwaka 2015 mpaka 2020 jambo lilitopelekea kutubeba Wabunge wengi wa CCM kuingia humu ndani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia sana kwenye suala la maji. Ukurasa wa 34 Mheshimiwa Rais alisema kwamba atalipa kipaumbele sana suala la maji na pia alisema sehemu nyingi alipokuwa anazunguka kwenye kampeni wananchi wengi sana walikuwa wanalamika kuhusu maji hasa maeneo ya vijiji. Kwa kweli tunamshukuru sana Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli, amejitahidi sana kutekeleza suala la maji katika maeneo mengi. Kwa Mkoa wangu wa Lindi tunamshukuru sana ametusaidia akina mama kututua ndoo kwa asilimia kubwa sana. Sehemu zilizobakia na changamoto ya maji ni chache sana. Tunaomba Waziri wa Maji na viongozi wengine mnaohusika na suala hilo la maji mjitätahidi sehemu zile chache ambazo zimebakia ili nao wanachi wa vijiji waweze kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingine ambayo napenda kuchangia ni huduma ya afya. Tunashukuru sana Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi imejitahidi sana kuboresha huduma ya mama na motto. Kwa kweli imejitahidi sana ukiangalia kwenye Wilaya ya Nachingwea wamefanya maboresho kwenye jengo la akina mama na watoto, wodi ya wazazi imekuwa nzuri na inahuduma nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambao napenda kuchangia ni kilimo, ukurasa wa 19. Pia nako kwenye suala la kilimo Rais wetu mpendwa amejitahidi sana kutekeleza llani hiyo ila kuna changamoto chache tu ambazo tunaomba na zenyewe zitiliwe mkazo ili wananchi wafaidike na Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Lindi wanalima sana mbaazi, lakini bahati mbaya kidogo mwaka huu na mwaka jana bei ya mbaazi imeshuka sana na Akinamama wengi wameanzisha vikundi, wameungana na biashara yao kubwa ni kulima mbaazi kwa ajili ya biashara.

Tukifuata kwenye ukurasa wa 19, Mheshimiwa Rais amesema tufanye kilimo kiwe biashara, na akinamama wale walijitahidi sana kulima mbaazi lakini bahati mbaya soko kidogo limeshuka. Ninachoomba, Mawaziri husika wajitahidi kutafutia akinamama wa Mkoa wa Lindi masoko ya mbaazi ili na sisi tuinuke katika maisha yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Haji Amour Haji.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza napenda kushukuru kupata nafasi hii ya kuja kushiriki katika Bunge letu hili Tukufu ikiwa ni mara yangu ya kwanza.

Napenda kukishukuru Chama changu Cha Mapinduzi kwa kuweza kunichagua kwa kura nyingi sana katika Jimbo langu la Pangawe, Zanzibar. Pia napenda kuishukuru familia yangu kwa kunipa ushirikiano mzuri hadi kufikia hii leo na kushinda katika Uchaguzi Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kisha napenda kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, hasa katika hotuba yake hii aliyoitoa mwezi wa Novemba, tarehe 13 ambayo mimi naiita ni hotuba shirikishi, ni hotuba ambayo imetupa mtazamo ambao ni mkubwa sana katika nchi yetu kwa kipindi cha miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema kwamba hii ni hotuba ambayo inazungumzia masuala ya maono, yaani masuala ya programu ya miaka mitano kwa kipindi ambacho kimeanzia kipindi hiki, hasa ntazungumzia katika ushirikishi uliokuwa humo kwa upande wa nchi zetu mbili; Tanzania Zanzibar pamoja na Tanzania Bara, kazungumza mengi sana kiasi ambacho ametupa moyo sisi Wazanzibari ambao

tumeshiriki katika Bunge letu hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba hii pia, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizungumza vizuri sana katika kumpa ushirikiano Rais wetu wa Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, ambaye pia nampongeza kwa jitihada zake kubwa ambazo anazifanya na kwa weledi ambao ameupata kutoka katika Bunge hili na kwa fikra ambazo amezipata kwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nadhani kwamba huko kila mmoja anasikia kuwa kazi ambayo anaifanya Rais wetu wa Zanzibar, Dkt, Hussein Ali Mwinyi, ni nzuri sana na nampongeza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii imezungumzia suala la Kimuungano hasa katika masuala ya kiuchumi, ushirikiano wa uvuvi hasa katika Sekta ya Bahari Kuu ambayo ni sekta ya Muungano. Namshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake na ushirikiano wake mzuri na kwa kuona ule umuhimu wetu wa kuunganisha nchi zetu wa kusema kwamba atanunua meli nane ambazo nne zitakuwa kwa upande wa Zanzibar na nne zitakuwa kwa upande wa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tumeona jitihada na tunaona umuhimu wa meli zile katika hotuba ile na kipengele kile kimezungumzia suala la ajira 30,000. Tunatumai katika ajira hizo Wazanzibari labda tutapata ajira 15,000 na upande wa Bara zitakuwa ajira 15,000, itakuwa si haba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mengi hasa kuzungumzia suala la ajira. Nitazungumzia suala mtambuka la upande wa Muungano; tuna tatizo kubwa la ajira hasa ajira ambazo wakati mwingine tunazzungumzia kwamba ni ajira rasmi na kuna ajira ambazo siyo rasmi. Nadhani kwamba Waziri wa Ajira upande wa Tanzania yupo hapa; kuna suala ambalo limekuwa ni tatizo hasa linalohusiana na suala la ajira hizi za nje, *employment agencies*, ambazo hizi kwa upande mmoja kama tutaweza kuziwekea mkazo

hasa ni ajira ambazo wakati mwingine linaweza likaleta soko kubwa, hasa kwa vijana wetu waliomaliza na hawana kazi. Kwa sababu wakati mwingine tunazungumzia suala la ajira kwamba labda watu waende kwenye kilimo, waende wapi. Ukiangalia hasa kuna fursa kubwa kwa kwa upande wa Tanzania kwa fursa zinazotokea nje ya nchi ambazo wakati mwingine zinakuwa ni ajira ambazo nazo ni rasmi lakini zinahitaji kuangaliwa ule umuhimu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kuna ajira ambazo zipo katika Nchi za Kiarabu kule, wakati mwingine tunakuwa na ufahamu ambao ni hasi kuziona kwamba zile ajira wakati mwingine kama ni *human trafficking*, lakini zipo ambazo zinakuja katika hali ya urasmi na zinakuja kwa mpangilio maalum, hasa kwa mikataba maalum na kwa muda maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kinachosikitisha ni kwamba wakati mwingine zile ajira zinakuja. Zipo ajira karibu, kwa mfano kwa upande wa Zanzibar kipindi hiki niliona zimekuja ajira kwa Tanzania karibu 1,200. Kwa kampuni moja ambayo ni *Transguard* ambayo iko Dubai pale, lakini utakuta kwamba Watanzania fursa ile tunashindwa kuitumia na kushindwa kwetu maana yake ni kwamba inawezekana milango ime...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba dakika moja tu nifafanue kidogo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo linalokuja ni kwamba milango kwa upande wa Tanzania Bara ile milango imefungwa kwa kuwaruhusu wale vijana kwenda kufanya kazi kule nje, ile fursa ya kupewa vile vibali, lakini kwa upande wa Zanzibar ile fursa inatumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa namwomba Waziri mhusika kwamba hiyo fursa aitoe na tupange mipangilio mizuri itakayoweza kuwapatia ajira vijana wetu wa Tanzania kwa ujumla na zinapotokea zile fursa maana yake ziwe kwa wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine zile fursa kwa upande wa Zanzibar tunazitumia vizuri, lakini upande wa Tanzania Bara inakuwa kidogo kama kuna milango ambayo imefungwa kwa zile fursa kwa upande wa vijana wetu kwa upande wa huku. Sasa nahisi kwamba tufanye mipango mizuri kupitia Balozi zetu kuunganisha suala hili ili kwamba nayo iwe ni fursa kwa vijana wetu kupata ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kutokana na muda, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano. Ahsante sana. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana kwa michango yenu mizuri, Mawaziri wameshachukua hoja nyngi ambazo mmechangia hapa kwa hiyo ninawashukuru. Pia nina mambo matatu kwa haraka.

Moja; Mheshimiwa Jenista nikuombe sana kwa sababu idadi ya Waheshimiwa Wabunge ni kubwa na muda wetu wa maswali upo palepale, Mawaziri wanapokuja kujibu maswali watusaidie majibu yawe mafupi. Wataalam wanaandika majibu marefu sana yanamaliza muda wote, hata wa kuuliza maswali ya nyongeza. Kwa hiyo Wabunge wanapata changamoto kutumia muda ule ambao wangependa kushiriki kwenye hilo zoezi. Watusaidie majibu yawe mafupi.

Pia sisi Waheshimiwa Wabunge mengine tuijelimishe wenyewe, tujitahidi kuuliza maswali ya nyongeza kwa kwenda moja kwa moja kwenye swalii, ukileta maelezo marefu na kile kipindi kiko moja kwa moja, unakipa mtihani Kiti kuanza kukukatisha maana watu wako kule wanakutazama, watasema hajui kuuliza maswali na mambo

kama hayo. Kwa hiyo tujitahidi. Wewe mwenyewe weka swalii lako pale anza kuuliza ujue linakuchukua muda gani. Mtu wa swalii la nyongeza huwezi kupewa zaidi ya dakika moja, ukishaanza kujieleza parefu wakati unajiaandaa tayari ujue ni mtihani.

Kwa muktadha huohuo ndugu zetu wa Serikali wajitahidi pia kufanya hayo mazoezi yale majibu yao yasiwe marefu sana kwa sababu mpaka Wabunge wakishaanza oh, oh, unajua tayari hapa muda umeshachukuliwa na majibu yao.

Lingine ni matumizi ya lugha humu ndani; Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe, Bunge letu hili ni jipya, ni muhimu sana kila mmoja kuzingatia taratibu zilizopo. Kwa sababu kama ambavyo sisi huwa tunahamaki nchi yetu ikitajwa huko nje tofauti na matarajio yetu, ikitajwa kwa mtazamo hasi, ndivyo ambavyo nchi nyingine pia zinajisikia ama zinaona Bunge limebariki na watakaposema huko watasema Bunge liliijadili nchi yao kwa namna hasi.

Hapa Bungeni kwa taratibu zetu unaweza kutaja nchi fulani kama mfano mzuri, kwamba tujifunze kwao, lakini ukileta mfano hasi inakuwa changamoto hata ya kidiplomasia kwa sababu maana yake wao hawataangalia ni Mbunge amesema; Mbunge gani? Itaonekana Bunge la Tanzania limesema kwa sababu na wewe ni Mbunge na umesemea humu ndani. Kwa hiyo tutazame ile mifano ya nchi mahususi tunazozitaja tuisitaje kwa namna ambayo inakuwa hasi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mfano, ziko nchi nyingi kweli zinatamani Rais wetu angeenda kuwa Rais kwao. Ukiisema kwa ujumla ni sawa, lakini ukiitaja nchi mahususi kwamba nchi fulani wanamtaka Rais wetu; sasa ile nchi haina Rais kweli? Inaye. Kwa hiyo unaliweka Bunge katika mazingira magumu kidogo kwa sababu kule mjadala wa taarifa utakapoenda itakuwa ni Bungeni walikuwa wanaongea habari za Rais wao kuja kuongoza nchi yetu,

siyo. Kwa hiyo lazima tuwe makini tunapotaja ama viongozi wa nchi zingine au nchi zao.

Lingine linahusu Kanuni, staha; niwakumbushe kutoka, kuingia, vyote hivi viko Kikanuni, usinyanyuke tu kwenye kiti ukaendelea na safari, lazima uoneshe kwamba unatambua huku mbele halafu unaendelea na shughuli zako, ndiyo utaratibu. Watu wanacheka hapa. Pia kupita katikati ya mzungumzaji; amesimama Mbunge usikatishe katikati yake na kiti, Kanuni zinakataza. Sasa siku nyine utaambiwa rudi ukae, siyo jambo jema Waheshimiwa Wabunge kwa hiyo ni muhimu kuzingatia hilo. Ukiingia umechelewa angalia anayezungumza yuko wapi ili upite. Usipite katikati unaweza ukarejeshwa kwamba rudi kwa sababu anayezungumza yuko upande huu, kwa hiyo tujitahidi.

Jambo la mwisho kabisa ni la mawazi; na yenye we yako humu. Humu ndani huwa wanasimama Wabunge, anasimama Mheshimiwa Kuhusu Utaratibu, fulani hajavaa, sasa utakuwa unashangaa hujavaa vipi lakini maana yake hujavaa Kikanuni.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.58 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi,  
Tarehe 4 Februari, 2021, Saa Tatu Asubuhi)*